ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

		MHE. ZUBEIR ALI MAULID	**-**	**SPIKA**
1.	Mhe.	Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2.	Mhe.	Riziki Pembe Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake
3.	Mhe.	Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4.	Mhe.	Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5.	Mhe.	Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
6.	Mhe.	Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
7.	Mhe.	Balozi Ali Abeid Karume	-	Uteuzi wa Rais
8.	Mhe.	Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
9.	Mhe.	Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
10.	Mhe.	Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
11.	Mhe.	Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
12.	Mhe.	Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
13.	Mhe.	Amina Salum Ali	-	Uteuzi wa Rais
14.	Mhe.	Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
15.	Mhe.	Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
16.	Mhe.	Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
17.	Mhe.	Chum Kombo Khamis	-	Nafasi za Wanawake
18.	Mhe.	Haji Omar Kheri	-	Jimbo la Tumbatu
19.	Mhe.	Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
20.	Mhe.	Hamad Rashid Mohamed	-	Uteuzi wa Rais

21.	Mhe.	Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
22.	Mhe.	Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
23.	Mhe.	Haroun Ali Suleiman	-	Jimbo la Makunduchi
24.	Mhe.	Harusi Said Suleiman	-	Jimbo la Wete
25.	Mhe.	Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
26.	Mhe.	Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
27.	Mhe.	Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
28.	Mhe.	Issa Haji Ussi (Gavu)	-	Jimbo la Chwaka
29.	Mhe.	Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
30.	Mhe.	Juma Ali Khatib	-	Uteuzi wa Rais
31.	Mhe.	Juma Makungu Juma	-	Jimbo la Kijini
32.	Mhe.	Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
33.	Mhe.	Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	Jimbo la Donge
34.	Mhe.	Khamis Juma Mwalim	-	Jimbo la Pangawe
35.	Mhe.	Lulu Msham Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
36.	Mhe.	Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
37.	Mhe.	Mahmoud Thabit Kombo	-	Jimbo la Kiembesamaki
38.	Mhe.	Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
39.	Mhe.	Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
40.	Mhe.	Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando
41.	Mhe.	Masoud Abrahman Masoud	-	Jimbo la Bububu
42.	Mhe.	Maudline Cyrus Castico	-	Uteuzi wa Rais
43.	Mhe.	Mihayo Juma N'hunga	-	Jimbo la Mwera

44.	Mhe.	Miraji Khamis Mussa	-	Jimbo la Chumbuni
45.	Mhe.	Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Jimbo la Mkoani
46.	Mhe.	Moh'd Mgaza Jecha	-	Jimbo la Mtambile
47.	Mhe.	Mohammed Aboud Mohammed	-	Uteuzi wa Rais
48.	Mhe.	Mohamed Ahmada Salum	-	Jimbo la Malindi
49.	Mhe.	Mohammed Said Mohammed	-	Jimbo la Mpendae
50.	Mhe.	Mohammedraza Hassanaali Mohamedali	-	Jimbo la Uzini
51.	Mhe.	Mtumwa Peya Yussuf	-	Jimbo la Bumbwini
52.	Mhe.	Mtumwa Suleiman Makame	-	Nafasi za Wanawake
53.	Mhe.	Mussa Ali Mussa	-	Jimbo la Ole
54.	Mhe.	Mussa Foum Mussa	-	Jimbo la Kiwani
55.	Mhe.	Mwanaasha Khamis Juma	-	Jimbo la Chukwani
56.	Mhe.	Mwanaidi Kassim Mussa	-	Nafasi za Wanawake
57.	Mhe.	Mwantatu Mbaraka Khamis	-	Nafasi za Wanawake
58.	Mhe.	Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini	-	Jimbo la Dimani
59.	Mhe.	Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy	-	Jimbo la Chaani
60.	Mhe.	Nassor Salim Ali	-	Jimbo la Kikwajuni
61.	Mhe.	Omar Seif Abeid	-	Jimbo la Konde
62.	Mhe.	Panya Ali Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
63.	Mhe.	Rashid Ali Juma	-	Jimbo la Amani
64.	Mhe.	Rashid Makame Shamsi	-	Jimbo la Magomeni
65.	Mhe.	Saada Ramadhan Mwenda	-	Nafasi za Wanawake
66.	Mhe.	Said Omar Said	-	Jimbo la Wingwi

67.	Mhe.	Salama Aboud Talib	-	Nafasi za Wanawake
68.	Mhe.	Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
69.	Mhe.	Said Soud Said	-	Uteuzi wa Rais
70.	Mhe.	Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
71.	Mhe.	Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
72.	Mhe.	Shadya Mohamed Suleiman	-	Nafasi za Wanawake
73.	Mhe.	Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
74.	Mhe.	Shamata Shaame Khamis	-	Jimbo la Micheweni
75.	Mhe.	Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
76.	Mhe.	Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
77.	Mhe.	Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
78.	Mhe.	Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
79.	Mhe.	Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
80.	Mhe.	Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
81.	Mhe.	Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
82.	Mhe.	Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
83.	Mhe.	Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
84.	Mhe.	Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Dkt. Yahya Khamis Hamad - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Sita – Tarehe 08 Aprili, 2016

(Kikao kilianza Saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma dua

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea na michango kwa hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Orodha bado ninayo hapa mbele yangu, kwa hiyo, naomba sasa nimwite Mhe. Lulu Msham Abdalla.

Mhe. Lulu Msham Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii asubuhi hii. Napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu "*Subhanahu wa ta'ala"* kwa kunijaalia uzima wa afya na wale wanaoumwa Mwenyezi Mungu awape tahafifu.

Mhe. Spika, awali ya yote napenda kuishukuru familia yangu kwa kunisaidia na kuniunga mkono pamoja na wahisani wangu wale ambao wamenisaidia mpaka hapa nilipofikia.

Mhe. Spika, mimi katika mchango wangu wa hotuba hii ni kutilia mkazo katika masuala ya kodi. Katika masuala ya kodi kuacha tegemezi kutoka kwa wahisani na mataifa mengine ili kuhakikisha mapato yanaongezeka kwa kasi zaidi ya hivi tunavyokusanya.

Mhe. Spika, lazima tudhibiti ulipaji wa kodi kwa bidhaa zinazoingia nchini pamoja na biashara zinazofanyika nchini, kwa sababu kuna miaya mingi ya ukwepaji kodi hususan wafanyabiashara wakubwa na maarufu. Sisi viongozi wanasiasa pamoja na watendaji tuna haki ya kusimamia ili kuweza kuingiza mapato zaidi na zaidi.

Vile vile, hatuna budi kuhakikisha tuna buni mbinu mpya za ukusanyaji wa mapato ili tuweze kukidhi jitihada zile ambazo Mhe. Rais ameziandalia, tusiridhike tu na vyanzo tulivyozowea, naamini tukifanya hivi viongozi pamoja na wananchi tutarajie maumivu makali sana. Lakini hatuna budi kuwa wavumilivu kwa hilo kwani kufanya hivyo ndiko kutakakotuwezesha kufikia dira ya maendeleo ya mwaka 2020.

Mhe. Spika, hoja yangu ya pili. Napenda kumpongeza Mhe. Rais kwa ahadi yake aliyoitoa ya kuongeza mishahara na kuanza kima cha chini na kusema kwamba ataongeza kiwe laki tatu ifikapo mwakani.

Mhe. Spika, ningeomba serikali iharakishe suala hili la Bima ya afya kwa sababu pesa nyingi zinatumika katika matibabu ya familia. Kwa hiyo, hata kama tutawaongezea laki tatu basi pia iharakishwe na hiyo bima ya afya ikiwezekana hata huo mwaka unaofuata basi bima ya afya ianze kwa wafanyakazi wa serikalini. Pia, nimpongeze kwa kufanikisha katika Pencheni ya wazee na kuanza mwishoni mwa mwezi huu.

Mhe. Spika, sasa naingia katika elimu. Mhe. Rais, amesema mambo mengi kuhusu elimu, naomba kunukuu:

> "Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita serikali ilizingatia huduma ya elimu kuwa ni haki ya msinigi kwa kila mwananchi na nyenzo muhimu ya maendeleo ya kiuchumi na ya kijamii". "Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita serikali ilichukuwa hatua za kuimarisha ubora wa elimu iliyotolewa kuanzia ngazi ya elimu maandalizi, msingi, sekondari, elimu ya juu na elimu inayotolewa katika vituo vya mafunzo ya amali Vyuo vya Ualimu na Chuo kikuu cha SUZA"

Mhe. Spika, ni kweli na napongeza sana haya maneno, lakini Elimu ya Vyuo Vikuu inajengwa na msingi mzuri unaopatikana na Skuli za Sekondari. Naiomba serikali iongeze idadi ya walimu pamoja na vifaa vya kufundishia, hususan Sanyasi na Hesabu ili kuweza kuongeza wanafunzi watakaofauli vizuri na wataalamu nchini mwetu.

Mhe. Spika, mwisho kabisa napenda kuwapongeza wanawake wote kwa uwezo wao mkubwa katika kuchochea kasi ya maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii. Bila ya kuwasahau na kina baba pia kwani wao ndio wako pamoja na hao kinamama. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa mchango wangu mdogo naiunga mkono hotuba ya Mhe. Rais asilimia kwa mia. Tunaweza, tutimize wajibu wetu. (*Makofi*)

Mhe. Rashid Ali Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, awali ya yote kabisa nimshukuru *Allah Sub-hanahu wa ta'ala*, muumba mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake tukiwemo sisi waja ambao leo tumekutana hapa. Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa rehema zake nichukuwe fursa hii kushukuru sana familia yangu, familia ya baba na mama ambayo Mwenyezi Mungu bado kaiweka hai ipo na inaendelea kunitunza na naendelea kuchota kwao maarifa ambayo yanatokana na waasisi kabisa wa *Afro-Shirazi Party*.

Pia, nichukuwe fursa hii kumshukuru sana mke wangu, namshukuru chaguo pekee pamoja na familia yangu kwa kuweza kunitunza muda wote kwa mapigano hususan katika wakati wa uchaguzi kuwa mvumilivu na kuwa mwenye hekima na kuweza kunichangia kwa misaada yote ya hali na mali mpaka nikafikia leo kuwa mmoja katika Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Namshukuru sana mke wangu. (*Makofi*)

Nichukuwe fursa hii kuwashukuru sana viongozi wa Chama cha Mapinduzi pamoja na Chama cha Mapinduzi kwa ujumla wake, nguvu zao, jitihada zao na uwezo wao uliofikia mwaka 2016 kukizika kabisa Chama cha CUF, hatuna budi kukipa pongezi na shukurani za dhati kabisa kwa kazi kubwa waliyoifanya. (*Makofi*)

Niendelee kutoa shukurani zangu za dhati kabisa kwa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. John Pombe Magufuli. Natoa shukurani zangu za dhati kwa usimamo wake ambao anaendelea kuuonyesha, lakini kwa maneno maalum ambayo aliyatoa na kusababisha Zanzibar kubakia katika hali ya amani, utulivu na usalama ambao unapatikana kwa kauli yake ya kuweza kulinda kwa hali yoyote ile vugu vugu ambalo lingeweza kutoa wakati wa uchaguzi.

Nisimsahau kabisa Mhe. Rais wa Zanzibar, pongezi za pekee zimfikie Mhe. Rais wa Zanzibar kwa ushindi wake mkubwa alioupata katika uchanguzi wetu wa marejeo uliofanyika tarehe 20 Machi 2016 ushindi ule utakuwa ni tosha kabisa kuonesha uwezo aliouonesha katika hotuba yake na imani yake kwa wananchi wa Zanzibar.

Niendelee kutoa shukurani zangu za dhati kwa wanachama wa Jimbo la Amani kwa kuweza kunipigia kura pamoja na wananchi wengine ambao wanakaa Jimbo la Amani kwa kuweza kunipigia kura zao na kuniwezesha kuwa Mwakilishi wao katika Jimbo hili la Amani na nachukuwa fursa hii kuwaahidi kwamba wasubiri mema na maendeleo mazuri katika jimbo lao.

Mwisho kabisa nitoe shukurani zangu za dhati kwako wewe Mhe. Spika, pamoja na wale wote waliopata uteuzi akiwemo Naibu Spika, Wenyeviti wa Baraza hili pamoja na Wajumbe saba ambao tunaungana nao leo hii hususan Mhe. Soud Said, ambaye yupo hapa kwa michango yake mingi ambayo tutaitarajia kuipata. (*Makofi*)

Sasa niingie moja kwa moja katika mchango wa hotuba ya Mhe. Rais, ni wazi kwamba hotuba ya Mhe. Rais ina sifa zote imesheheni hali zote, imesheheni mambo ya kiuchumi, mambo ya kijamii, mambo ya kimaendeleo na sifa nyingi ambazo namna gani maendeleo yetu kwa miaka mitano ijayo tunaweza tukaifikia ambayo yameelezwa katika hotuba hii. Kusheheni kwa mambo mazuri sana yaliokuwemo katika hotuba hii isitoshe kuwa pekee ni mchango au sifa ambayo tunaweza tukaitoa na kutupa maendeleo ya dhati.

Lakini utekelezaji wa hotuba hii ni changamoto kubwa ambayo inatukabili kufikia mihimili yote mitatu. Muhimili wa Serikali, Mahakama pamoja na majukumu yetu sisi wana Baraza ambao ni muhimili wa kutunga sheria. Kwa kweli tuna kazi katika kutekeleza hotuba hii ambayo kwa Mhe. Rais ni dira ya maendeleo yake kwa miaka mitano. Ni wazi kwamba hotuba hii imeeleza mambo mengi mazuri na imetoa moto kabisa kwa wananchi wa Zanzibar, lakini ni jukumu la wananchi kubadilika na kubadilisha mawazo yao, yaani *mindset* za wananchi ndizo zitakazofikia kuithibitisha kwamba hotuba hii ina ubora na ni nzuri na kweli inatekelezeka na maendeleo ya wananchi yanaweza kuonekana.

Mhe. Spika, nianze kuchangia katika sekta ya uchumi, Mhe. Rais ameeleza wazi kwamba ndani ya mwaka 2015 pato la Taifa limekuwa kwa asilimia 6.6 na tarajio lake kwamba ifikapo mwaka 2020 uchumi utakuwa kwa asilimia 8.8 mpaka asilimia 10. Hili linawezekana ikiwa wenyewe sisi tutajidhatiti, tutajiamini na tutaamua kuufikisha uchumi wetu huo hapo tunapotaka ufikie.

Mhe. Spika, uchumi unaokuwa siku zote hutegemea sekta na vipaumbele vya sekta, ni wazi kwamba kwa muundo na jiografia ya kisiwa chetu hiki tunategemea sana sekta za huduma, biashara na kwa uchache viwanda. Lakini kilimo, Utalii pamoja na ajira kukuwa ni sekta muhimu sana zinaweza kuendeleza uchumi wetu.

Sasa nigusie kidogo sekta ya ukuaji wa mapato, ni wazi kwamba ili uchumi uwepo unahitaji mapato na sisi tuweze kutumia. Suala la mapato Zanzibar lina mfumo wa kipekee, Zanzibar yetu hii haiwezi kutegemea mapato yanayotokana na maendeleo ya viwanda kutokana na ukubwa na jiografia ya nchi yetu.

Lakini tukiamua kuendeleza biashara kwa dhati, tukiwa wakweli na tukifichua yale ambayo yamefichikana basi wazi biashara ndani ya kisiwa hichi itaukuza uchumi kutoka asilima sita tulipo sasa mpaka kufikia hiyo asilimia kumi tunayoitaka ndani ya sekta ya biashara peke yake. Imefika wakati sasa katika kuunga mkono hotuba hii Mhe. Spika, wafanyabiashara wajidhatiti kulipa kodi kwa hiari.

Tumeanza kuona mifano mingi kwa wenzetu, hiari imekuwa ngumu, kuna kazi ngumu ya kupasua majipu. Kwa hivyo, na Zanzibar ifikie wakati endapo hiari hatuitaki katika kulipa kodi, yaani *voluntary compliance* tunaiona ni ngumu basi na mikasi, visu, nyembe zitumike kwa walipa kodi ili nao walipe kodi ipasavyo. Katika kulipa kodi kuna makundi matatu muhimu; kuna kundi kubwa la walipa kodi wakubwa, kuna kundi la kati la walipa kodi wa kawaida na kuna kundi la walipa kodi katika sekta isiyo rasimi. Kwa nchi yetu hii ya Zanzibar ni ngumu sana kuelekeza nguvu zetu na sisi Wajumbe kusimamia kwa nguvu kabisa sekta isiyo rasmi, yaani *informal sector* kwa sababu jambo hili duniani kote ni kikwazo kikubwa katika ukusanyaji wa mapato.

Lakini endapo tutaweka mifumo bora ndani ya hii sekta ya biashara isiyo rasmi, yaani *informal sector,* basi ni wazi kwamba wafanyabiashara wa Zanzibar ni wengi na wakilipa kodi inayostahiki kwa ukubwa wa biashara zao, basi tunaweza tukafikia sehemu ambayo kodi itaongezeka mara dufu au mara tatu ya mapato yanayokusanywa sasa.

Mhe. Spika, labda nitowe mifano. Tuwaangalie wenzetu China. China wameleta mfumuko wa kubadilika katika sekta isiyorasmi katika biashara, wameweza kujenga *mall* kwa ajili ya biashara na kwa ajili ya aina ya biashara. Kwa mfano, ukienda Shenzhen wameweka ni mji wa *electronic*, mji ule unafanya biashara za aina zote za *electronic*. Ukifika pale ukitaka biashara rahisi ya kutumia siku mbili utaipata, ukitaka biashara ya kutumia miezi mitatu utaipata na ukitaka biashara madhubuti yenye bei kubwa ya kutumia kwa miaka na miaka utaipata. Hatuna budi katika hotuba hii yameelezwa wazi hayo ya kujenga *mall* na majumba makubwa ya biashara na sisi tujifunze mfumo wa kutumia *malls* hizo ambazo zitajengwa ili mapato yakuwe. *(Makofi)*

Mhe. Spika, niliwahi kutembelea kule nchini Beijing China, kuna *mall* yenye ghorofa sita, kila ghorofa ina mfumo wake wa biashara na biashara za pale ni *informal sector*, wanaita *bargaining market,* soko la mapatano. Unaweza ukabahatika ukenda pale shati ya shilingi 80,000/-, basi ukanunua kwa shilingi 10,000/- kwa sababu ya uwezo wa kupatana. Lakini kodi inayokusanywa pale kwa mujibu wa mauzo yote yanayouzwa, kodi yake inapatikana kwenye serikali, hivyo kuiwezesha serikali kudhibiti mapato ambayo yanatokana na *informal sector*, yaani biashara isiyorasmi, kuweza kuiwezesha serikali kupata mapato yake yote.

Mhe. Spika, ni wazi kwamba biashara ya kati ndio inayolipa kodi kweli, walipa kodi hawa wa kawaida wanalipa mapato kwa dhati. Wanachokihitaji sasa ni elimu ya kodi ili kuweza kukuza biashara zao, na ndani ya elimu hiyo waweze kulipa kodi bila ya mashaka yoyote.

Wafanyabiashara wakubwa. Mhe. Spika, mimi nafikiria kwamba uwe mkali sana katika kiti chako, wafanyabiashara wakubwa wa ndani ya nchi yetu hawajawa tayari kulipa kodi, ni watu ambao wanapenda sana misamaha. Misamaha ya kodi inayotolewa ndani ya nchi yetu kwa wafanyabiashara wakubwa, yakiwemo na mahoteli ya daraja la kwanza, wawekezaji wakubwa, inazidi thamani ya mapato yanayokusanywa ndani ya nchi. Kwa hivyo, tutakapodhibiti misamaha hiyo basi mapato yetu ni wazi kuwa yataweza kuongezeka mara mbili kutokana na walipa kodi wakubwa.

Mhe. Spika, walipa kodi wakubwa hupenda sana sifa katika kulipa kodi kwao, tuwape sifa zao wanapolipa kodi kikweli kweli, lakini tusiwache kuwasimanga wasipolipa kodi kisawasawa, huo utakuwa ni muarubaini kabisa. Mlipa kodi mkubwa unapomfichua, ukamtangaza na ukamuweka hadharani, basi inakuwa hakuna tofauti na kumtangaza 'kitangi', yaani muharibifu wa watoto na inapotokea hivyo, hawezi tena kuendelea kukwepa kodi. Kwa hivyo, naliomba sana Baraza lako liweze kukemea katika kuisimamia serikali ili kuona mapato ya wafanyabiashara wakubwa mchango wake uko mbali, biashara za kati mchango wake uko mbali na zile biashara zisizo rasmi zinakuwa namna gani, ili tuweze kuzikuza siku hadi siku.

Mhe. Spika, sasa niendelee kidogo kwenye suala zima la miradi ya sekta binafsi na sekta za serikali, yaani *PPP*. Mhe. Spika, huu ni mfumo ambao umebuniwa siku nyingi sana, lakini miradi ya sekta za serikali inaathiriwa sana katika suala zima la kukuza uchumi wetu huu wa nchi, pale tunapoongeza urasimu, pale tunapoweka tamaa na vipaumbele vyetu vya binafsi ndani ya kutekeleza miradi ile ambayo tunaingia nayo mashirikiano. Ni wazi kwamba Zanzibar ina fursa kubwa ya miradi mbali mbali. Lakini miradi mingi Mhe. Spika, kama ilivyoelezwa katika hotuba hii, kwamba imepangwa na imebuniwa itatekelezwa ndani ya kipindi cha miaka mitano, lakini bado inaonekana wazi watekelezaji ndani ya sekta za serikali, na wale ambao watapata nafasi katika serikali kuisimamia miradi hii, ni lazima wafike wakati sasa wa kusema tulichopata kinatosha na sasa tuidumishe serikali yetu nayo iingie katika uchumi wa kati. Kwa sababu ndani ya miradi kama hii, mikataba mingi haifiki kutiwa saini endapo makubaliano hayatafikiwa.

Mhe. Spika, tumeona mifano ya mikataba mingi kwa upande wa Tanzania Bara, tumeona mikataba ya umeme, tumeona *Escrow* kule, tumeona mikataba ya *Standard Charter* kule na maumbuko mengi tu ambayo yanapita. Lakini ni ukweli uliowazi kwamba tunashindwa kuwa na makubaliano ya dhati pale ambapo matakwa yetu hayafikiwi. Kwa hivyo, wasimamizi wajijuwe wazi kwamba miradi inapokuja wawe wepesi kuitekeleza, wairuhusu na waikubali ili Taifa hili lianze sura mpya ya maendeleo.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, umebakiwa na dakika mbili.

Mhe. Rashid Ali Juma: Ahsante sana Mhe. Spika. Mhe. Spika, kama nilivyosema hotuba hii imesheheni mengi ya kilimo, uvuvi na mazao ya biashara. Hatuna budi Mhe. Spika, kutilia mkazo katika biashara za bahari kuu. Nchi yetu hii imezungukwa na bahari, nchi yetu ni kisiwa, kwa hivyo, bahari kuu lazima itumike ipasavyo ili kuokoa pato la Taifa.

Mhe. Spika, kilimo cha mwani ni kilimo ambacho kimeingizwa kwa utamaduni mkubwa, lakini bado ni kilimo kinachodumaza wananchi wa ulimaji wa mwani. Mimi kule kwetu kijijini ninapotoka, walimaji wa mwani ndio watu duni kuliko watu wa aina yoyote na ndio wameletewa mradi ili uwakuze wawe wana uwezo kidogo. Kwa hivyo, napenda sana rasilimali vitu na rasilimali fedha za mikopo ziende kwenye vikundi vya wavuvi wa mwani, ili waweze kuongezewa na wao uwezo kupatiwa zile thamani na kupatiwa mikopo ili kilimo hiki kikuwe. Hiki ni kilimo kikubwa sana na Zanzibar kinaweza kutuokoa.

Mhe. Kabisa Mhe. Spika, nizungumzie kidogo suala la nishati ya mafuta. Mhe. Spika, kweli na iwe kweli, kijiko tukiite kijiko hata kama kitakuwa kikubwa namna gani katika muundo wake tusije tukakiita pauro. Nasema hili Mhe. Spika, tuna imani ndani ya nchi yetu Zanzibar kuna mafuta, na kila penye mafuta sheria yake gesi lazima ipatikane, sio lazima kwenye gesi kuwa na mafuta. Ndio maana wenzetu Tanzania Bara wanapata gesi, lakini mafuta inawezekana kuwa bado. Kwa rasilimali hii tuliyokuwanayo Baraza hili naomba tusimamie viongozi wetu wa serikali, hususan wale watakaochaguliwa ambao tutakuwa tunao, tunaomba sana wapewe hii sekta ya nishati, ili mafuta kabla ya kufikia mwakani yachimbwe, uondoke urasimu. *(Makofi)*

Huu uchumi tunaouzungumzia wa kupata mapato, haya ni mapato yaliyowazi na ni mapato ya dhahiri, tuwe na mifumo tu, tusijisahau tutakapochimba mafuta kudumisha mazingira kwa yale mafuta yatakayochimbwa. Kwa sababu tunaweza tukachimba mafuta hapa tukaja tukaachiwa mashimo na matokeo yake tukashindwa pakukaa na kisiwa chetu kikiwa si cha matumaini.

Mwisho kabisa Mhe. Spika, nilikuwa nina hamu sana ya kuelezea kazi za ajira, lakini tusiwasahau vijana. Vijana ni tegemeo letu, kinamama ni tegemeo letu, watoto ni tegemeo letu na ajira ndio uchumi. Ikikuwa ajira na uchumi unakuwa, tuweke kipaumbele ajira.

Mhe.Spika, kwa dakika moja nataka nikuambie wazi kwamba mipango ya muda mrefu na muda mfupi ndani ya sekta zetu za serikali ni lazima itumiwe, *Scheme of Service* lazima zifanywe, hata kwa wafanyakazi ni lazima zifanywe...

Mhe. Spika: Mhe. Rashid Ali Juma, samahani nina wasi wasi muda wako utakuwa umekwisha.

Mhe. Rashid Ali Juma: Ahsante namalizia Mhe. Spika...

Mhe. Spika: Mchango wako ni mzuri lakini katika mazingira ya kawaida unaweza hata ukachangia kwa maandishi.

Mhe. Rashid Ali Juma: Kwa hivyo, mwisho kabisa Mhe. Spika, napenda sana katika hili suala la ajira...

Mhe. Spika: Mhe. Rashid Ali Juma, nakushukuru sana.

Mhe. Rashid Ali Juma: Naunga mkono hotuba hii nzuri, nahakikisha na Baraza hili kwa pamoja tukisimamia ipasavyo tunaamini tutafika na Mhe. Rais atafika pahala pazuri.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Rashid Ali. Naomba sasa nimwite Mhe. Shaib Said Ali, atafuatiwa na Mhe. Jaku Hashim Ayoub, nafikiri yupo namuona. Mhe. Riziki Pembe, ajiandae.

Mhe. Shaib Said Ali: Mhe. Spika, kwanza sina budi kukushukuru wewe kwa kunipa fursa hii adhimu na mimi kuichangia hotuba ya Mhe. Rais. Mhe. Spika, kabla ya yote kwa vile leo hatujaonana tokea asubuhi kwa baadhi ya wajumbe humu, basi niseme *Asalaam Aleykum Warahmatullah Taalla Wabarakatu.*

Jambo la pili, Mhe. Spika, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wote wazima na tukafika katika ukumbi huu kwa salama na amani na tukaweza kuendelea na shughuli zetu. Mhe. Spika, kwa shukrani zote kabisa tuseme *Alhamdulillah* na zile kubwa tuseme kwamba yale ambayo tumekatazwa tuyawache na yale mema tuyaendeleze.

Mhe. Spika, baada ya shukrani hizo nikupongeze wewe kwa dhati kabisa kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi, pamoja na timu yako kamili akiwemo Naibu Spika, na Wenyeviti. Pia, Mhe. Spika, nimpongeze kwa dhati kabia Dkt. Ali Mohammed Shein kwa ushindi aliopata wa kishindo. *(Makofi)*

Aidha, nimpongeze kwa kumchagua tena Mzee wetu Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kuwa Makamu wa Pili wa Rais. Baada ya hapo niwapongeze wapigakura wangu walionichagua mimi katika uwakilishi huu. Katika Jimbo langu la Chonga kuanzia Mtimbu hadi Tundauwa. Mhe. Spika, jimbo langu limefika katika bahari. Ukienda Mashariki limepakana na bahari na ukienda Magharibi limepakana na bahari, kwa hivyo, tuko katikati ya bahari Mheshimiwa. *(Makofi)*

Vile vile, Mhe. Spika, nimpongeze kwa dhati Mhe. Rais kwa uteuzi wake au nawapongeza Watanzania wote wapenda amani walioichagua CCM kuirudisha tena madarakani. Pia, nawapongeza kwa kumchagua Mhe. John Pombe Magufuli kuwa Rais wa Tanzania. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nikiendelea na pongezi zangu na shukrani zangu nataka niwapongeze Wawakilishi wakongwe ambao tumewakuta katika Baraza hili, kwa moyo wao na ujasiri wao na walivyotupokea, wametuonesha dhahiri kwamba tutakuwa kitu kimoja watatusaidia pale ambapo tutakwama tutakuwa nao, na pale ambapo tumekosea watatufunza. Kwa hivyo, Mhe. Spika, kwa hayo nawashukuru sana wawakilishi wako. *(Makofi)*

Mhe. Spika, niingie katika michango mingineo ndani ya hotuba hii. Lakini kuna msemo unaosema kwamba "ukimstahi mke ndugu basi huzai nae". Mhe. Spika, wawakilishi kutoka Pemba tumeipokea hotuba hii kwa mikono miwili pamoja na wawakilishi wenzetu wa Unguja. Lakini nataka niseme Mhe. Spika, kwamba wawakilishi kutoka Pemba tutakuwa na kazi kubwa ya kutimiza malengo ya hotuba hii kutokana na hali yetu ya kisiasa iliopo Pemba. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hivi sasa kuna kulia na kuna kushoto, wabunge wenzetu tunawajua na wawakilishi ndio sisi. Tunataka kuleta maendeleo katika majimbo Mheshimiwa, lakini wenzetu kutokana na siasa yao huwenda wakatukwamisha. Sasa namuomba Mheshimiwa, atusaidie katika taasisi zetu ziliopo Pemba tushirikiane ili kuitekeleza hotuba hii.
Mhe. Spika, taasisi ziliopo Pemba zina majipu yanakaribia kuoza, wawakilishi kutoka Pemba tunayajua hayo. Tumeshayapeleka majipu hayo kwa Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, kwa Mhe. Rais, Mhe. Mohammed Aboud, ni shahidi na wawakilishi wote kwamba taasisi zetu ziliopo Pemba baadhi zina majipu ya kutumbuliwa kabisa. Kama majipu hayo hayatatumbuliwa basi hii hotuba ya Mhe. Rais hatutofikia lengo la kuitekeleza.

Mhe. Spika, nataka nikuambie kwamba utendaji wetu wa kazi sisi wawakilishi wa kule ni lazima tushirikiane na taasisi ziliopo Pemba. Lakini Mhe. Spika, kutokana na majipu kuna mifano iliyokuwa dhahiri tulipokuwa tukipiga kampeni, tukienda katika taasisi nyengine wana-CCM tulikuwa hatuwezi kuingia katika taasisi hizo. Mkuu wa taasisi hiyo akiambiwa huyo anayekuja ni mwana-CCM,basi anawaambia watumishi wake mwambieni sipo au mwambieni nina kazi aje baadae, ukienda hayupo. Kwa maana hiyo, tunamuomba Mhe. Rais, majipu yaliopo Pemba katika taasisi ayaondowe mara moja ili tufanikishe kazi hizi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya hapo niingie katika kuchangia sasa. Mhe. Spika, mimi nachangia sana kuhusu masuala ya kilimo, kwa sababu mimi jimbo langu ni fani yangu. Mimi niliahidi kwa wananchi wangu nikawaambia naomba munichaguwe, lakini hususan mchaguweni Mhe. Rais wangu ili aongoze tena, yaani CCM irudi tena Tanzania. Mimi niliwaambia niko radhi musinichaguwe nikalimie tena mihogo yangu na migomba yangu, lakini CCM ikamate madaraka iongoze nchi, kulikoni kunichagua mimi kuwa Mwakilishi, lakini badala yake nikiondoka hapa nakwenda Mtendeni nikakune ndevu, nikawaambia siwezi. Kwa maana hiyo Mhe. Spika, wananchi wangu wamenituma, kwa vile ni wakulima wameniambia nikija hapa suala la kilimo nilisemee kwa nguvu zangu zote. Wawakilishi kutoka Pemba watakuwa ni mashahidi kwamba kijiji cha Pujini, Chonga, Mgelema ndivyo vinavyokaribia kulisha asilimia 80 ya mazao ya Pemba yanakotoka. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nilisema kwamba kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa letu, lakini nina wasi wasi kwamba bado hii dhana hatujaifikia. Mhe. Spika, nimeondoka Pemba hivi karibuni tu, lakini tayari wananchi wameshalima, sasa hivi hakuna pembejeo, mbolea, wala dawa. Hii dhana itafika wapi. Kwa hivyo, naomba Mhe. Spika, atakayekamata wizara hii ya kilimo, basi ahakikisha kwamba hii dhana imefikiwa. Nimeondoka mimi Sheha mwenye watu 3,000 anapewa polo tatu za mbolea, atazigawaje hizo polo tatu. Anapewa paketi moja ya dawa ya kuulia magugu yenye vibomba 12, atawezaje kuvigawa hivyo. Kwa hivyo, bado nasema kwamba hii dhana ya kilimo naomba Mheshimiwa, atakayepewa dhamana hii aishughulikie ili wananchi wetu waondokane na kubakisha kutaka kutegemea ajira za serikali.

Mhe. Spika, Pemba kilimo tayari ni uti wa mgongo wao, wanautegemea kwa hali na mali. Kwa hivyo, naiomba hii waziri atakayehusika na hili ajuwe kwamba kilimo ndio kitakachotunyanyua.

Baada ya hayo Mhe. Spika, nije kwenye masuala ya viwanda. Tumeambiwa kwamba kutajengwa viwanda vingi sana. Lakini naomba basi na kule Pemba hutokea mazao na baadae yakatupwa ovyo. Mhe. Spika, Pemba hulimwa mazao halafu baadae yakatupwa. Kwa mfano, tungule. Nasikia tungule zina *jam* nzuri sana kama zitapata kiwanda, kwa nini hatujengi kiwanda cha *jam* kule Pemba ili zikafanyiwa *jam* zile tungule za Pemba tukawacha kuagizia *jam* kutoka nje. Vile vile, maembe yanaozeana bure wakati wa msimu wa embe. Naomba masuala haya ya viwanda japo kimoja kijengwe Pemba cha kusindika masuala haya.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo nije katika suala la afya. Ndugu zetu wa kike na hata wa kiume wanaathirika. Mfano unapokwenda hospitali hupati ufumbuzi na ukenda Mahakamani hupati ufumbuzi. Kwa hivyo, naiomba Wizara ya Afya au serikali kwa jumla chombo hiki cha *DNA* kinunuliwe kwa haraka, kwa sababu ndugu zetu wanaathirika na wanadhalilika, na unapokwenda hospitali au Mahakamani unachoambiwa ni kwamba ushahidi haupo.*(Makofi)*

Mhe. Spika, naiomba Wizara ya Afya kwamba chombo hiki kinunuliwe, kwa sababu ni chombo ambacho kitasaidia kupunguza angalau huu msokotano uliopo wa ndugu zetu wa kike kuharibiwa.

Mhe. Spika, baada ya hapo, sasa naomba nizungumzie kuhusu vyombo vya habari. Mhe. Spika, vyombo vya habari wataalamu wanatuambia kwamba mauaji ya Rwanda yalichangiwa na kalamu, yaani waandishi wa habari ndio waliochangia mpaka watu wakauana kiasi kile.

Mhe. Spika, sasa huu uhuru wa vyombo vya habari uko wapi, kwa sababu mbona vyombo vya habari vyengine vinatangaza masuala ya uchochezi, kwa nini haviitwi angalau tukaona kama ni magazeti kwa ajili ya kuonywa, kwa sababu Mhe. Spika, masula haya yote asilimia 70 mpaka 80 yamechangia na vyombo vya habari. Kwa mfano, wakati mwengine utakuta gazeti linaandika hata hayapo katika ulimwengu huu, lakini *heading* utaikuta pale ipo imeandikwa. Mhe. Spika, naomba Waziri wa Habari atakayeteuliwa safari hii ayashughulikie masuala haya.

Mhe. Spika, kwa vile ni mara yangu ya mwanzo leo, basi nasema nikate utata tu. kwa hivyo, nasema hotuba hii nitaifanyia kazi katika jimbo langu. Lakini Mhe. Spika, namuomba Mhe. Rais wa Zanzibar haya majimbo yalioko katika taasisi za Pemba ayaondoe haraka sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa niaba ya wapiga kura wangu wa Jimbo la Choka na wana-CCM wote tunaiunga mkono hotuba hii kwa asilimia 100 na kama kuna ziada basi asilimia 110. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Shaib Said Ali, ahsante sana kwa mchango wako ambao ni mzuri. Sasa naomba nimwite Mhe. Jaku Hashim Ayoub, atafuatiwa na Mhe. Riziki Pembe Juma na Mhe. Khamis Juma Mwalim, ajiandae.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, awali ya mwanzo kabla ya yote nichukue fursa hii kwa dhati kabisa kumshukuru Mwenyezi Mungu *Allah Subuhanahu Wataala* aliyeniwezesha kusimama hapa na kuweza kuvuta pumzi na huu sio ujanja wangu, wala akili yangu, ama uwezo wangu au maarifa yangu, isipokuwa ni neema yake Mwenyezi Mungu.

Hivi sasa wangapi wanakata roho, wangapi wanazaliwa, wangapi wako *ICU*. Kwa kweli, hakuna neema kubwa Mhe. Spika, kwa binadamu au utajiri alionao kuliko afya, yaani afya ni neema kubwa kuliko kitu chochote kile Mhe. Spika. Hivyo, hizi pumzi za kujivunia kwa muda mfupi na maisha ya kweli na ya kudumu yako akhera na dunia ni mzoga tu Mhe. Spika. *(Makofi)*

Baada ya hapo nichukue fursa hii au nitakuwa mtovu wa adabu wa mwisho kama sitowashukuru wananchi wa Jimbo la Paje, baada ya Mwenyezi Mungu, wapili ni wao kunirejesha humu.

Kwa hivyo, niendelee kuwashukuru wananchi wa jimbo la Paje kwa kuniamini kwao katika majimbo mapya yaliyokatwa na hapo mwanzo lilikuwa Jimbo la Muyuni, ikiwemo Shehia ya Jozani, Kitogani, Muungoni, Paje, Bwejuu na ninasikia imeongezwa mpya ya Michamvi. Mhe. Spika, niendelee kuwashukuru kwa dhati kabisa kwa kuniamini kwao tulikuwa wengi kidogo na wakaniamini mimi kunipa shughuli hii. *(Makofi)*

Mhe. Spika, niendelee kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein kwa dhati hasa katika sekta ya afya. Kwa kweli, nimezungumza mwazo kwamba kila kiumbe hai huhitaji afya, yaani amechukua jitihada kubwa sana katika sekta hii Mhe. Rais wetu wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mchango wangu hautakuwa mkubwa sana. Lakini nazungumzia suala la afya kutokana na umuhimu wake, kwa sababu Mhe. Spika, wewe mwenyewe unahitaji afya na mimi pia ninahitaji. Sekta hii imekuwa na matatizo makubwa sana hasa katika hospitali yetu kuu inayotegemewa kuitwa rufaa na bado haijafika rufaa pamoja na jitihada alizozizungumza Mhe. Rais wa Zanzibar kwamba kilomita tano hufiki utakuta hospitali, lakini nini kinachofanya kuitwa hospitali, ni vifaa pamoja na madawa. *(Makofi)*

Kwa mfano, kipindi kilichopita nilizungumza kuhusu suala la *ICU* na nilipata mtihani mkubwa Mhe. Spika, lakini kwa Mhe. Rais wetu wa Zanzibar kuwa makini hivi sasa tunayo *ICU* ya kujivunia na wala *Aga Khan* hana hivi sasa, yaani ni ya kileo kabisa. *(Makofi)*

Lakini hivi sasa hospitali ile inavuja kwa mvua hizi, pia *X-Ray* mtihani isipokuwa ni *mobile* tu inachukuliwa huku na kupelekwa kule na ukitaka kupiga *X-Ray* mwili wote mzima huwezi kupata, *film* na *CT-Scan* mtihani. Kwa kweli, kwa sekta hii waziri atakayekuja kupata bahati na naibu waziri, lakini mimi Mwenyezi Mungu asijeakanijaalia na Ijumaa hii, achukue jukumu kubwa sana la kuiangalia sehemu hii, kwa sababu afya ni utajiri wa kila mtu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, niendelee tena kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar, kipindi kilichopita aliwaambia mawaziri pamoja na manaibu waziri wanapoulizwa maswali kama watakuwa hawana majibu nayo, bora wajibu kwa maandishi. Kutokana na hali hiyo, niombe sana wale watakaobahatika ikiwa waziri au naibu waziri atakapoulizwa swali na mjumbe na akiwa hana jawabu la kuridhisha basi bora achukue muda na baadae aje kujibu kwa maandishi. *(Makofi)*

Rais wetu wa Zanzibar yuko makini sana kwa saula hili na jitihada anazozichukua. Lakini kama kuna kitu kilichonivutia katika hotuba ya Rais wa Zanzibar ni kwenye ukurasa wa tano na ninaomba kunukuu Mhe. Spika, na kwa umuhimu wake ameigusa sehemu mbili.

Ukurasa wa tano unaeleza hivi:

> " …Waheshimiwa Wawakilishi na wananchi wote, ni kuwa tuendeleze umoja wetu na mashikamano kwa maslahi ya wananchi wote bila ya ubaguzi wa aina yoyote kwani sote ni wamoja…"

Mhe. Spika, hakuishia hapo, kutokana na uzito wake lipo tena kwenye ukurasa wa 73 na naomba kunukuu.

Ukurasa wa 73 unaeleza hivi:

> "…mshikamano, umoja na mapenzi baina yetu Zanzibar bila ya kujali rangi, kabila, dini na itikadi ya kisiasa."

Mhe. Spika, narejea tena jimboni kwangu sitombagua yeyote na huu ndio ulikuwa msimamo wangu tokea mwanzo. Mhe. Spika, kuna hadithi inasema hivi; "*laa tahasadu, wala tabadhu, wakunu ibadilahi ikhiwani*". Kwa hivyo, maana yake ni kwamba tusihusudiane, wala tusioneane choyo na tuwe wamoja katika uislamu. Ya nini kubaguwana kwa sababu ya mambo ya kupita tu haya ya siasa. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, mimi naendelea tena na ninaahidi walionipa kura na wasionipa kura nitawatumikia bila ya ubaguzi Mwenyezi Mungu akinijaalia na hilo namuomba Mwenyezi Mungu anijaalie. Kwa kweli, haya ni mambo ya kupita tu. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba nizungumzie kuhusu barabara. Mhe. Spika, barabara ya Mkunazini kuelekea skuli kule ile barabara imefungwa kwa muda mfupi na yale ni mateso makubwa kwa wananchi, serikali iangalie na wala hatuwezi kupangiwa muda wa kupika chakula chetu au pika hapa chakula chako, akatoke mtu Uingereza na kukwambia chakula kile usikile na huu ndio ukoloni tunaoukataa. Kwa kweli, barabara ile kuna kanisa, pia kuna misikiti karibuni mitatu mikubwa, kuna benki, sasa leo kuna watoto walemavu wanakwenda skuli watafika vipi skuli. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, nadhani serikali ikakae ikaliangalie huu ni usumbufu, kama ni msongamano wa magari basi tutafute utaratibu au mpango mwengine. Mhe. Spika, niiombe serikali kwamba kule kuna kanisa, pia, misikiti mikubwa karibu mitatu ya Ijumaa, skuli, benki. Sasa leo mtu au mteja anapeleka fedha zake benki akaja akaibiwa au akapigwa risasi, ni vyema Mamlaka ya Mji Mkongwe ukaliangalie suala lile.

Vile vile, ninajua kabla ya kujiunga Mji Mkongwe kuna sheria zenu munapeleka kule, ile ni kufungwa kiini macho. Kwa hiyo, serikali iangalie barabara ile kwa jicho la huruma kabisa, kuna watu walemavu wanakwenda skuli pale na wanahitaji huduma za benki, kuna kanisa ni kivutio cha biashara ya utalii, hivyo, njia ile serikali ikakae iangaliwe. Kwa kweli, yale ni usumbufu na mateso makubwa sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sasa naomba niende kwenye ukurasa wa 36 kuhusu mazingira. Kwa kweli, kipindi kilichopita nilipiga kelele sana kuhusu Mji Mkongwe kutumia mawe mazingira yanachafuka na leo nashukuru Mhe. Rais ameliona hili, kwa hili serikali iliangalie kwa sababu mazingira yanazidi kuchafuka.

Jambo jengine la kusikitisha kama hatujawa tayari katika sekta ya michezo ule uwanja wa Mao Tse-Tung ni hatari na kwa nini tumeuvunja na bado hatujawa tayari kuujenga, kwa mfano gari zikajakutumbukia mule ndani na Mwenyezi Mungu aepushe na hilo, kwa kweli kama hatujawa tayari kutengeneza uwanja tungeuacha.

Mhe. Spika, hivi sasa kuna haja serikali hata kuutia waya kwa kuuzungusha, kwani kupishana na gari njia mbili ni mtihani na leo ni karibu miezi sita au saba uwanja umekaa vile vile na wala hatuwezi kwenda kwa namna hiyo, yaani huwezi kuachia tawi kama hujakamata tawi. Sasa tumevunja uwanja ule na umekuwa mtihani pale kuja kutokea ajali na gari hazipishani na imekuwa shimo moja kwa moja.

Mhe. Spika, kwa kumalizia nimuombe sana waziri atakayekuja kupata Wizara ya Ardhi, Maji, kwa kweli tokea dunia kuanza Michamvi hawajapata maji matamu. Ninawashukuru wafadhili wetu wa *Ras Al Khaimah* kwa kuchimba kisima kule Michamvi, yaani kisima kipo lakini huduma haipo na wala sitaki kujisifu kwa hapa na Mwenyezi Mungu anajua kama nimetoa kwa mkono wa kulia au kushoto lakini hapa si pahali pake, lakini kuna siku nitakuja kuzungumza kama nitakuwa hai, lakini tokea dunia kuanza wananchi wa Michamvi hawajapata maji na kule kuna mahoteli karibu 6 au 8.

Kwa hivyo, waziri atakayekuja hizi ni salamu zangu, kwanza aangalie kisima kimeshachimbwa, lakini kwa hili ni mtihani na nitakuwa sijawafanyia haki wananchi wa Michamvi kwa hili. Mhe. Spika, nimuombe waziri atakayekuja nimuombe kwa heshima kabisa suala hili aliangalie, wananchi wanaumia na kipindi cha mvua ni hatari kipindupindu na hivi sasa tayari Jozani, Muungoni na Kitogani, kuna Kambi imeshafunguliwa sasa hivi kuhusu maradhi ya Kipindupindu na sababu ni kutokana na hali ya maji yalivyo na Mwenyezi Mungu atuepushe na balaa hilo.

Mhe. Spika, kwa mchango huo nafikiri nimalizie hapa na ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Jaku Hashim Ayoub, ahsante sana. Waheshimiwa Wajumbe, nimeombwa niwatangazie kwamba kwa baadhi yenu ambao bado hamujapiga picha za vitambulisho ambavyo wenzenu wengine watakuwa wamevivaa, basi munaombwa mufike katika chumba cha kusomea maktaba kwa ajili ya kupiga picha hizo. Kwa hivyo, ninaomba kwa utaratibu tu, yaani musiende watu wengi wengi isipokuwa aende mmoja au wawili, ili wengine wapate nafasi ya kuendelea kuchangia, ahsanteni.

Sasa baada ya hapo, naomba nimuitwe Mhe. Riziki Pemba Juma, atafuatiwa na Mhe. Khamis Juma Mwalim na Mhe. Suleiman Makame Ali, ajiandae.

Mhe. Riziki Pemba Juma: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipatia nafasi kuweza kuchangia kuhusu hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar aliyoitoa juzi katika Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, kwanza kabisa nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema uzima na kuweza kunifikisha hapa hadi sasa na kuweza kusimama mbele ya Baraza lako tukufu.

Vile vile, napenda sana kuishukuru familia yangu kwa malezi mazuri ambayo wamenipatia, elimu, pia, katika kuniunga mkono kwao katika hizi harakati za kisiasa tokea nilipozianza hadi hivi sasa ninaendelea nazo. Kwa kweli, ninawashukuru sana na ninawaomba wazidi kuniunga mkono kwa kila pale ambapo wanahisi ipo haja ya kufanya hivyo. (*Makofi*)

Mhe. Spika, niwashukuru walimu wangu wote wakiwemo walimu wa madrasa, skuli msingi, sekondari hadi vyuo vikuu, ambao wao wametoa mchangu mkubwa sana kwangu hadi mimi kuweza kufika hapa nilipo, ninawashukuru sana na Mwenyezi Mungu *Inshallah* atawalipa. *(Makofi)*

Pia, niwashukuru sana wanawake wa Mkoa wa Kaskazini hasa kupitia hilo kundi la wasomi, ambao wamenipa ridhaa zao kuweza kuwawakilisha ndani ya chombo hiki. *(Makofi)*

Nikiendelea na pongezi pamoja na shukurani, sasa naomba niwashukuru Baraza Kuu la UWT, ambalo wao walimalizia kazi ya kunipa ridhaa zao kuweza kuwawakilisha na kuweka ile imani kwa wale vijana wa vyuo vikuu kuona kwamba wale waliowapeleka walikuwa wanafaa na tunashukuru kwamba tunafaa sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba nianze kuchangia hotuba hii ya Mhe. Rais wa Zanzibar. Kwanza kabisa napenda nimpongeze sana Mhe. Rais wa Zanzibar kwa hotuba yake nzuri sana, ambayo nitasema imezungumzia mambo mengi ambayo kama wananchi wangependa kuona serikali yao inayafanya. Lakini pia ni mambo ambayo nadhani katika Ilani yetu

ya CCM ya Uchaguzi ni mambo ambayo pia yamegusiwa. Hivyo, napenda sana nimshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar kwa hilo. *(Makofi)*

Naomba nianze mchango wangu katika sekta ya elimu, kwa sababu kuna mambo mengi ambayo yamezungumzwa. Napenda niipongeze sana Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa maendeleo makubwa ya kielimu ambayo hadi sasa yapo. Mhe. Spika, nasema hivi kwa sababu tunaona kwamba kuna skuli nyingi sana zimejengwa, vyuo vingi, hivyo, haya yote ni maendeleo katika sekta ya elimu. Lakini maendeleo haya yanazidi kuchangiwa zaidi na pale Mhe. Rais aliposema kwamba atahakikisha anajenga skuli katika kila eneo ambalo kuna upungufu na msongamano wa watu, nimpongeze sana kwa hili. *(Makofi)*

Lakini ili hili liweze kufanya kazi vizuri ni kwamba tuzingatie hawa walimu ambao watakaokwenda kusomesha katika hizi skuli. Nidhahiri kwamba maendeleo ya skuli hayawi kama walimu hawako vizuri. Kwa hivyo, naiomba sana serikali iweze kuyaangalia yale mazingira ya walimu, na mazingira yenyewe yaangaliwe kwenye maslahi ya walimu. *(Makofi)*

Kwa kweli, tunamshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar ameweza kupandisha kiwango cha mshahara cha walimu wake, lakini bado kazi ya uwalimu ni kubwa sana na pia tunamuomba sana afikirie katika kuwaongezea maslahi zaidi, ili kuona ule ufanisi wao wa kazi inafanyika vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, jambo jengine ni kuhusu suala zima la vitendeakazi, tunazo skuli nyingi nzuri na zinapendeza isipokuwa kuna uhaba mkubwa sana wa vitendeakazi vikiwemo vitabu. Kwa hiyo, tunaiomba serikali na hasa kwa yule ambaye atapewa dhamana aweze kulisimamia vyema hili suala la vitendeakazi katika hizi skuli zetu, kwa sababu bila ya vitabu hata ule ufanisi hautakuwa mzuri sana. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, haiwezekani kwamba mwalimu ana darasa la wanafunzi 80 halafu wanafunzi wana vitabu vitano, yaani hata ile kimgawanyo wa makundi itakuwa hayawi. Kwa hiyo, kwa suala hili naomba sana serikali ijitahidi, inafanya kazi nzuri, isipokuwa ijitahidi zaidi. *(Makofi)*

Vile vile, kuna suala zima la kompyuta, serikali naona inaandaa mpango kwamba kila skuli kuwa na *computer lab*, na jambo hili limeanza kufanyika sana katika skuli nyingi za Unguja na Pemba. Lakini kuna tatizo moja miundombinu ya baadhi ya skuli sio mizuri, unaweza kukuta skuli hata umeme hauko vizuri, kwa hiyo, hii *computer* hata ikiwepo pale haitoweza kufanya kazi.

Mhe. Spika, licha ya huo umeme, hicho chumba ambacho kinatarajiwa kiwe cha *computer* hata saruji hakina, hasa mazingira kama hayo sio mazuri. Lakini mbali na hayo, unakuta skuli ambayo ina wanafunzi 700 au 800 mpaka 1,000 ina *computers* mbili. Kwa hiyo, sidhani kama tutakuwa tunafanya jambo ambalo kweli tunataka mwelekeo au lile lengo liweze kufanikiwa, kwa sababu lengo kila mwanafunzi angalau aweze kutumia *computer* na sio aitumie kwa ajili ya kucheza *games*, isipokuwa kutumia kwa masomo yake.

Lakini *computers* mbili ndani ya skuli nzima bado itakuwa hatujafanya kazi. Mhe. Spika, kwa hili naiomba serikali itakayokuja, maana yake nakusudia waziri ajitahidi sana katika kuhakikisha suala hilo linafanikiwa.

Nikiendelea na mchango wangu katika sekta ya elimu. Mhe. Spika, tuwaangalie walimu katika fursa mbali mbali, kama vile fursa za masomo na hata yale mafunzo ya muda mfupi, yaani *short training*. Tunajua kwamba kuna nchi nyingi ambazo zinakuwa zinatoa hizi *short courses* kwa ajili ya taasisi tofauti, na taasisi hizi labda elimu kidogo inakuwa inawekwa kando, nasema inawekwa kando kwa sababu katika walimu waliopo wote labda walimu 5,000 ukienda kuuliza walimu wangapi wamepata hizi fursa labda unaweza kupata watano, lakini hao watano ukiuliza wamezipataje hizo fursa kwa kweli anajua mwenyewe kwa njia gani aliyoitumia.

Mhe. Spika, naomba sana hizi fursa na walimu waweze kupewa, ili waweze kujifunza, kwa sababu njia moja ya kusoma ni kule kutembea, sasa mwalimu akipata fursa na kutoka nje basi anajifunza mengi zaidi kule kwa wenziwe kunafanywa nini, ili na yeye aweze kuboresha ile kazi yake. Lakini hata kisaikolojia mtu anapotoka katika eneo lake la kazi na kwenda nje kidogo hata kama ni wiki moja basi akili yake inakuwa ni nzuri zaidi kwa ajili ya kufanya kazi upya, kwa hili naomba tulifikirie.

Vile vile, suala la masomo walimu wanaomba fursa ya kusoma ndani ya nchi hii na wala sio nje, lakini bahati mbaya sana mwalimu anaambiwa asubiri mpaka baada ya miaka mitano, jambo hili linasikitisha sana, sana, labda pengine ni kwa watendaji siwezi kujua. Mhe. Spika, kwa sababu tunavyofahamu sekta nyingi za Serikali wafanyakazi wake wanakwenda kusoma na mtu mfano anarudi kusoma anaweza kukaa mwaka mmoja akafanya kazi kwa sababu lazima kile ambacho amekisoma akifanyie kazi.

Sasa mfanyakazi mwaka mmoja au miaka miwili baadae anakwenda kusoma, lakini mwalimu kasoma *Certificate* anataka kwenda Diploma anaambiwa akae muda wa miaka mitano, hee jamani, lazima tumhurumie huyu mwalimu na yeye kwa nini akae miaka mitano wakati anamuona mwenziwe katika Wizara nyingine anakaa mwaka mmoja anafanya kazi baadae anakwenda kusoma, hili linavunja moyo sana walimu wetu, kwa sababu tunataka maendeleo ya elimu. Lakini kama mwalimu hatujampa fursa, ule ufanisi wake hautokuwa mzuri, tumuendeleze mwalimu ili aweze kufanya kazi nzuri zaidi ya kutusomeshea vijana wetu, lakini tukimwambia akae miaka mitano ndio akasome Diploma, hee, baadae miaka mitano mingine akasome *Degree. Are we serious?* Lazima hili tulione na Serikali naomba ilikazie. Na waziri ambae atakuja kupewa hii dhamana naomba aje awe mkali kwa hili, asione tu kwamba baadhi ya walimu wanapewa na wengine wananyimwa.

Lakini jengine kuhusu posho za likizo za walimu, mwalimu anakwenda likizo mpaka anasahau kama alikwenda likizo ndio anakuja kupewa ile pesa yake, kwa hivyo, kidogo na hapa napo tuwafikirie sana hawa walimu, kwa sababu mwalimu baada ya mshahara hana zaidi ya hicho, hana posho, hana usafiri, hana chochote, kwa hivyo, angalau ile pesa yake ya likizo badi apewe kwa wakati ule ambao unatakiwa isiwe kucheleweshwa.

Mhe. Spika, jengine bado nipo katika elimu katika vyuo vikuu. Tunaishukuru sana Serikali yetu kwa kuanzisha vyuo vikuu kwa sababu zamani ilikuwa ni hasara, watu wanaokwenda kusoma Chuo kikuu wanakwenda Dar-es-Salaam, lakini ndani ya Zanzibar wanaweza kuchaguliwa watu watano tu, ilikuwa ni jambo la kusikitisha sana, lakini Serikali yetu baada ya kuona umuhimu wa hili wametuanzishia Chuo kikuu ndani ya Zanzibar, kimeanza SUZA, lakini mbali ya SUZA hata ile Tunguu nayo ingawa sio ya Serikali lakini bado inatoa fursa kwa vijana wetu kupata nafasi ya kusoma Chukwani, sasa hivi kuna *IPA*, kuna Chuo cha Habari na vyenginevyo vinatoa hizi fursa za kusoma. Lakini ndani ya vyuo vikuu hivi kuna changamoto zake, kwa sababu chuo kama chuo kinajitegemea chenyewe, kwa maana maamuzi yote yanayotoka ndani ya Chuo yanatoka ndani ya chuo chenyewe, kwa hivyo, ina maana hapa wizara iko mbali, Serikali kidogo iko mbali na hili jambo.

Kwa hivyo, ni kwamba hapa napo tupaangalie, ndani ya vyuo kuna walimu, kuna wanafunzi, kuna wafanyakazi, walimu hawa wanakuwa na mambo mengi na wao ambayo yanawasumbua wanashindwa kuyafikisha kwa sababu akiamua mkuu ni kile chuo chenyewe, kwa hivyo, kama kitashindwa maana yake hana sehemu nyengine ya kwenda, kwa hivyo, tunamuomba labda Mhe. Rais aandae utaratibu wowote kwa sababu yeye ni mkuu wa vyuo vyote tuna imani na hilo, kwa hivyo, aandae mazingira japo mwaka mara moja awe anaonana na wafanyakazi na wale walimu wa vyuo ili kuweza kuona kuna changamoto gani ambazo zinawakabili. Au pia anaweza kumtumia waziri ambaye atakuwa anahusika na hili jambo kufanya hivyo kwa niaba yake.

Mhe. Spika, katika vyuo pia kuna suala la mikopo, Serikali imejitahidi sana katika kutoa mikopo kwa wanafunzi wake ingawa kwamba ni vijana wengi ambao wanakwenda kusoma, kwa hivyo, ina maana hata huu mkopo kidogo unakuwa *sometimes* unagwaya gwaya kwa sababu vijana ni wengi, kwa hivyom tunaiomba sana Serikali iwaongezee bajeti yake ile bodi ya mikopo ili iweze kuwapa fursa ya kuwapatia mikopo wanafunzi wengi zaidi ili waweze kujiendeleza.

Mhe. Spika, nikitoka hapo nakwenda katika suala la mafunzo ya amali. Serikali imejitahidi sana juu ya hili na tunamshukuru sana Rais wa mwanzo wa Zanzibar Marehemu Karume alipoweza kuanzisha kile Chuo cha Karume kwa lengo zuri tu kwamba vijana waweze kupata yale mafunzo ya ufundi na mpaka leo tunaona kile chuo kinanakwenda vizuri, lakiini katika kuendeleza jitihada hizi Serikali pia imeamua kuanzisha ile mamlaka ya mafunzo ya amali, kwa hivyo, ni kazi nzuri sana na nadhani lengo lako ni kwamba kuwasaidia vijana wetu

wakimaliza pale waweze kujiajiri wao wenyewe, ila bahati mbaya sana mafunzo ya amali yanakabiliwa na changamoto nyingi nayo, ikiwemo suala la vitendea kazi.

Mhe. Spika, vitendea kazi ni vichache na sijui niseme bajeti finyu, siwezi kusema sana juu ya hilo, lakini kwanza ile mamlaka yenyewe ya amali, yaani jengo linalotumia ni jengo la kukodi, kwa hivyo, kama inakodi ina maana gharama nyingi zinakwenda katika kulipia kodi ya lile jengo. Tuiombe Serikali ifanye namna yoyote ya kuweza kuwapa jengo la kudumu, kwa sababu Serikali ina majengo mengi, inaweza ikawapatia jengo ikawa ni la kwao la kudumu, wanaweza kuliboresha tu lakini likawa ni la kwao, kwa hivyo, ile gharama ya kukodi ikaondoka.

Kwa hivyo ile bajeti iliyokuwa inakwenda kwa kulipia kodi ikaweza kufanya kazi nyengine za ike mamlaka, kwa hivyo, ruzuku yake maana yake waweze kuongezewa na hilo jengo pia waweze kupatiwa. Lakini katika hili tujitahidi kama Serikali tunapeleka vitendea kazi vya kutosha kwa ajili ya vile vyuo vya amali, kwa mfano kama kile chuo cha amali cha Mkokotoni, kipo chuo vijana wanakwenda lakini ufanisi wake bado sio mzuri sana, kwa sababu kijana anaweza kumaliza pale bado akategemea ajira kutoka Serikalini na ilikuwa lengo la kile chuo ni kwamba amalize pale aweze kujiahiri mwenyewe kama ambavyo wanafunzi wa Karume tunaona wanavyojiajiri, pengine ndani yetu humu yapo matunda ya Karume ambayo yamo humu ndani ama nje ya humu lakini yapo na yanaonekana na yanaweza kujiajiri. Kwa hivyo, nao hawa tuweze kuwafikiria.

Mhe. Spika, nikitoka katika suala la elimu, niende suala zima la utamaduni. Mhe. Rais aligusia sana masuala ya utamaduni na sisi kama sisi Wazanzibari lazima na sisi tujithamini, tujielewe na tuuthamini utamaduni wetu. Katika utamaduni kuna suala zima la lugha, lugha yetu adhimu ya Kiswahili ambayo ni sehemu ya utamaduni. Mhe. Rais katika hotuba yake, naomba nimnukuu alisema kwamba; "Tutaendelea na jitihada za kuimarisha lugha ya Kiswahili na kuzifanya lahaja za Zanzibar kuwa ni chimbuko la Kiswahili fasaha".

Kwa hivyo, tukizingatia hilo tuone fahari kwamba lugha yetu ya Kiswahili ni lugha adhimu sana, wanatoka watu katika mataifa mbali mbali wanakuja Zanzibar kwa ajili ya kujifunza lugha yetu ya Kiswahili, kwa hivyo, nini tufanye ili tuboreshe zaidi zaidi mambo haya. Ni kwamba katika maktaba ambazo tunaweka basi tujitahidi sana kuweka masuala yetu ya utamaduni zile maktaba za makumbusho maana yake, masuala ya utamaduni yawepo likiwemo na suala zima la lugha ya Kiswahili, Kiswahili kimeandikiwa na watu wengi sana zamani na hadi sasa, kwa hivyo, ni vizuri maktaba hizi zikaweza kuweka zile kumbukumbu zao ili hata wale wageni wanapokuja waweze kuona Kiswahili chetu ili tuweze kujivunia zaidi.

Lakini pia kupitia Kiswahili vijana wetu wanaweza kujiajiri kwa ajili ya kufanya kazi za kufundisha wageni hii lugha ya Kiswahili na hiyo ikawa tayari ni ajira tosha kwao ya kuweza kujiajiri, kwa hivyo, tuuenzi zaidi utamaduni wetu basi tutaweza kuandaa fursa za ajira kwa vijana wetu.

Mhe. Spika, nije katika vyombo vya habari, tunaishukuru sana Serikali kwa kufanya Shirika la *ZBC* kuwa ni shirika letu kubwa na zuri na linafanya kazi vizuri, hapa tulipo shirika hili ndio ambalo linatuonyesha. Lakini shirika hili naomba Serikali iliangalie sana kuhusu suala zima la vitendea kazi, vitendea kazi ni vichache, unaweza kukuta kwa mfano kuna jambo limetokezea leo, baada ya siku mbili ndio linakuja kuonyeshwa kwenye Shirika la *ZBC* au linasikika ndani ya redio, hii yote inatokana na uhaba wa vitendea kazi.

Kwa hivyo, tunaiomba sana Serikali ilisaidie hili shirika kwa sababu bado halijakua sana, kwa hivyo, ilisaidie ili liweze kupata vitendea kazi vizuri iweze kufanya kazi zake vizuri zaidi ili habari isitoke ikawa imeshapitwa na wakati, yaani habari ikishapita siku mbili inakuwa imeshapitwa na wakati. Lakini tukio limetokea leo habari tuweze kuiona leo leo na hili linawezekana sana kama hili litazingatiwa, lakini vile vile kama maslahi ya wafanyakazi pia nayo yataboreshwa, kwa sababu mwana habari ni sawa sawa na alivyo mwalimu, alivyo daktari, wana kazi kubwa sana na kazi zao hazina hata *weekends,* kwa hivyo, tuwafikirie sana maslahi yao ili waweze kufanya kazi vizuri zaidi...

Mhe. Spika: Mheshimiwa, umebakiwa na dakika mbili.

Mhe. Riziki Pembe Juma: Na katika hili Rais aligusia suala zima la Sheria ya Makosa ya Matumizi ya Mitandao, naomba suala hili nalo tulifanyie kazi kwa haraka sana ili labda hili suala la udhalilishaji wa viongozi wetu katika mitandao ya kijamii liweze kuondoka, tunaona aibu sana wakati mwengine kwenye *WhatsApp* inaweza ikarushwa picha ya kiongozi wa nchi namna anavyodhalilishwa, kwa kweli inachukiza sana, lakini sheria bado haijapita kwa Zanzibar, kwa hivyo, tukilifanyia haraka hili jambo basi itaweza kuwadhibiti watu na viongozi wetu wataweza kustirika.

Lakini mwisho kabisa naomba nimalizie kwa kusema kwamba Rais katika hotuba yake aligusia suala zima la wanawake na watoto, sisi viongozi tunasema kwamba tutasimamia hizi haki za wanawake na watoto, ushirika wa wanawake ili kuona maendeleo ya wanawake yafikiwa zaidi na wanawake wanakuwa mbele zaidi kuliko ambavyo tulivyo sasa, kwa hivyo, naomba sana Mhe. Rais awe na imani kwa hilo kwamba tutashirikiana nae, tutafanyakazi kwa nguvu moja.

Mwisho kabisa na mimi naomba kwa niaba ya wanawake hasa kupitia Mkuu wa Vyuo Vikuu naomba kuungana na hotuba ya Mhe. Rais kwa asilimi mia moja, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Khamis Juma Mwalim: Ahsante Mhe. Spika, awali ya yote na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia leo hii kuwa mzima wa afya na kuniwezesha pia kusimama hapa mbele ya Baraza lako hili, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu nikushukuru na wewe Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi hii na mimi niweze kuchangia hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein ambayo aliitoa tarehe 5 April, 2016.

Mhe. Spika, itakuwa si busara, si hekima na vile vile si vizuri kwa kutowashukuru wananchi wa Jimbo la Pangawe, nachukua fursa hii Mhe. Spika, kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Pangawe kwa kujenga imani na mimi na kunichagua kuingia katika Baraza hili kwa kura nyingi sana ili niweze kuyasema yale ambayo yanawasibu au yanawatatizo katika jimbo lao, na vile vile matatizo mbali mbali yanayowatatiza wananchi wa Zanzibar. Fursa hii naitumia kwa kuzitaja Shehia ambazo walishiriki kikamilifu kunichagua katika Jimbo langu la Pangawe, naomba kuitambua na kuitaja na kuishukuru Shehia ya Kinuni, Muembe Majogoo, Mnarani, na namalizia Shehia yangu ya nne katika jimbo langu la Pangawe ambayo ndio iliyochukua jina langu la Pangawe.

Mhe. Spika, baada ya kutoa shukurani hizo, sasa na mimi niweze kuchangia hotuba hii ya Mhe. Rais iliyoletwa mbele yetu, nami moja kwa moja nitakwenda kwenye masuala yanayohusiana na uchumi katika udhibiti wa ubora wa karafuu ya Zanzibar. Naipongeza Serikali ya Zanzibar kwani kwa muda mrefu sasa hivi imejitahidi kuhakikisha kwamba zao la karafuu linapatiwa udhibiti ndani na nje ya nchi. Lengo la Serikali ni kuinua kipato cha nchi kwa kudhibiti zao hili la karafuu.

Mhe. Spika, naelewa kwamba mambo mbali mbali au hatua mbali mbali kufikia huu udhibiti wa ubora wa zao la kafaruu yameshafanyika, kwa mfano katika hotuba ya Mhe. Rais alielezea masuala ya kupata udhibiti bora katika *TBS* tayari umeshafanikiwa na katika *TANCET* vile vile wameshafanikiwa kupata hivyo vidhibiti au vyeti hivyo.

Mhe. Spika, kwa masikitiko makubwa na hii naiomba Serikali kwamba zoezi la kutafuta udhibiti wa ubora wa karafuu limekuwa la muda mrefu sasa, kwa kumbukumbu zangu za haraka haraka nakumbuka mwaka 2011 Serikali ya Zanzibar kwa kushirikiana na Shirika la Mali la ubinifu ulimwenguni, yaani *World Intellectual poverty organization* ilipeleka wataalam wafanyakazi watano kutoka Serikali ya Zanzibar kwenda nchini Ethiopia ili kujifunza wenzetu namna gani wame-*brand* kahawa yao ili nasi tuweze kupata mafunzo yale tuyatumie kuyaleta kwetu ili tuweze kui-*brand* au kufanya udhibiti wa ubora wa karafuu yetu.

Mhe. Spika, mwaka 2011 hadi sasa hivi 2016 ni kipindi kirefu sana na udhibiti huu wa karafuu hadi sasa nje ya nchi bado haujafanikiwa, kwa hivyo, naiomba Serikali suala hili liwekewe mkazo husasun katika wizara husika. Katika vipaumbele vya wizara husika kwa maana Wizara ya Biashara na zile wizara ambazo zinasaidiana ili kufanikisha hili ziweze kuweka vipaumbele vyao katika suala hili la udhibiti wa ubora wa karafuu ya Zanzibar ili iweze kupata soko huko nchi za nje.

Mhe. Spika, tunapoipeleka bidhaa yetu nchi za nje na ikapata udhibiti na ubora, bila ya shaka ule utaratibu wa karafuu yetu kwa kuchanganywa na karafuu nyengine utapungua, ule uchakachuaji wa karafuu yetu ya Zanzibar na kuchanganya karafuu za nchi nyengine pia utapungua na hatimae karafuu yetu kama itakuwa tayari imeshakuwa *branded* moja kwa moja tunaweza kupeleka nchi za nje na kupata soko kubwa zaidi.

Kwa hivyo, naomba waziri atakayechaguliwa hivi karibuni ajue kwamba suala hili lipo na lina muda mrefu, kwa sababu tunapochelewa kui-*brand* karafuu yetu, vile vile tunachelewa kupata mapato zaidi, kwa sababu mara tu tutakapoweza kui-*brand* karafuu yetu nchi za nje bila ya shaka kipato chetu kitaongezeka, na vile vile hata wakulima wetu wa karafuu nao watafurahi zaidi kuliko hapo walipo sasa hivi ambapo wanavyofurahi kwa maana kwamba kiwango chao cha malipo kitakuwa zaidi.

Mhe. Spika, nikitoka hapo, sasa naomba kwenda katika masuala ya barabara, nashukuru tena Serikali ya Zanzibar katika masuala ya miundombinu, tukiangalia barabara zetu sasa hivi kutoka mashamba hadi mjini tunatelea tu sasa hivi, kwa sababu zamani inawezekana unatoka Makunduchi baada ya kuchukua saa moja kama sasa hivi unavyokwenda katika muda wa kawaida zamani unaweza kuchukua masaa mawili.

Mhe. Spika, nakumbuka nilipokuwa mdogo barabara zilivyokuwa mbovu kijijini petu pale Muyuni, kijiji cha Muyuni ni maarufu sana katika uzalishaji wa boribo, kwa kuwa barabara mbovu kipindi hicho inachukua siku mbili hadi tatu boribo zetu au boribo za Muyuni zinashindwa kupelekwa mjini, wakati mwengine wanatoka watu Muyuni wanaingia gari ikipita kwenda Makunduchi wanaingia kabisa ili wakakae kwenye gari waweke foleni ili ikipita pale Muyuni waweze kupata nafasi ya kupakia boribo zao. Lakini nashkuru Mwenyezi Mungu kwamba Serikali yetu ya Zanzibar imejitahidi vya kutosha kuhakikisha kwamba miundombinu ya barabara mijini na vijijini imeimarika.

Mhe. Spika, katika utekelezaji wa suala hili, naiomba Serikali vile vile inapoangalia zile barabara za mjini au vijijini vile vile isisahau kuziangalia barabara za ndani. Kuna barabara inayotoka kwa Mabata kwenda Kinuni, barabara hii ina matumizi ya watu wengi, wakaazi wa Jimbo langu la Pangawe kwa maana ya wakaazi wa Kinuni na wakaazi ambao hawakai Jimbo la Kinuni lakini wanatumia barabara ya Kinuni. Mhe. Spika, barabara ya Kinuni ni mbovu ikiwa jua kali barabara hiyo ina mavumbi, ina mabonde na kipindi hiki cha mvua Mhe. Spika, barabara hiyo sasa hivi unaweza kuingia ndani ya gari lakini gari inavyotembea wakati mwengine maji yanaweza kukurukia ndani ya gari kwa mashimo, barabara iko katika hali mbaya sana na usalama wa watu wangu wa Jimbo la Pangawe unakuwa ni mdogo sana kwa sababu wanapokuwa na safari ya kwenda mjini wanakuwa wanafikiria mara mbili mbili, mashimo yamejaa kwenye barabara, inawezekana katika mashimo yale gari inapoingia kwenye mashimo wanaweza wakavunjika mbavu na hatimaye afya yao ikaanza kuzorota. Kwa hivyo, naiomba serikali pamoja na barabara nyengine ambazo zinaendelea kujengwa na hii barabara ya kutoka kwa Mabata kwenda Skuli ya Kinuni waweze kuiangalia.

Mhe. Spika, sambamba na barabara hii kuna barabara ambayo inayotoka Kituo cha Polisi Kijitoupele kwenda Kimara, halikadhalika barabara hii ina watumiaji wengi na ni kero kwa wananchi wangu wa Jimbo la Pangawe kwa sababu barabara hii iko katika hali mbaya.

Mhe. Spika, nikiendelea naomba kuchangia hotuba hii katika masuala ya ardhi. Masuala haya ya ardhi yamekuwa ni mazungumzo makubwa kwa maana migogoro ya ardhi. Baada ya migogoro ya ardhi kila tunapokwenda iweze kupungua lakini upo uwezekano kwamba kila tutavyoendelea mbele migogoro ya ardhi itazidi kuongezeka. Kwa hivyo, nini kifanyike? Serikali ijitahidi kutoa elimu ya matumizi bora ya ardhi kwa wananchi wake. Lakini jengine

kubwa zaidi kwa sababu katika hotuba hii ya Mhe. Rais alizungumzia kwamba kuna baadhi ya viongozi katika Serikali hii ya Zanzibar wanashiriki kikamilifu katika kuanzisha migogoro mbali mbali ya ardhi. Sasa basi kwa kuwa Mhe. Rais anawaelewa ni vyema kuwachukulia hatua haraka iwezekanavyo, bila ya kujali ukubwa wao, nguvu zao au hadhi yao katika serikali au katika jamii. Tutakapofanya hivi migogoro ya ardhi itaweza kupungua, kwa sababu inavyokuwepo migogoro ya ardhi mapenzi baina ya wananchi kwa wananchi yanapungua, mapenzi baina ya wananchi na serikali yao yanapungua. Lakini vile vile Mhe. Spika, migogoro ya ardhi itakapopungua ule uwepo wa kesi nyingi Mahakamani zinazohusiana na ardhi vile vile zitapungua.

Mhe. Spika, nikitoka hapo naomba niende katika masuala ya vyama vya ushirika na masuala ya *SACCOS*. Naelewa kwamba serikali imekuwa mstari wa mbele kuhakikisha kwamba wananchi wake wanajikwamua katika hali duni ya kiuchumi waliyonayo kwa kuanzisha vikundi mbali mbali vya ushirika.

Naiomba serikali isichoke kutoa elimu kwa vikundi hivi, unapotoa elimu kwa vikundi hivi, bila shaka ule uzalishaji wao utakuwa una tija zaidi. Lakini sambamba na hili hivi vikundi ni vyema vikapewa umuhimu wa usajili, kwa sababu unapokuwa na kikundi bila ya kukisajili unakikosesha haki yake. Kwanza kikundi kile kitakosa haki yake ya kutambuliwa serikalini kwamba hicho kikundi kipo, na vile vile inapotokea fursa ya kupata mikopo kikundi kama hakina usajili kinakosa mikopo. Kwa hivyo, ni vyema serikali kuhakikisha kwamba elimu inatolewa katika vikundi vyote.

Sambamba na hili katika elimu Mhe. Spika, napenda kutoa mfano mdogo, mimi niliwahi kufanya kazi katika ofisi moja inashughulika na masuala ya usajili wa biashara. Kuna siku alikuja mjasiri amali pale akaniambia nimekuja hapa naomba unisaidie, nikamwambia karibu hiyo ni kazi yangu tupo hapa kwa ajili ya kuwahudumia wananchi. Alinambia mimi mjasiri amali sina kitu chochote ni mnyonge nimeamua kufanya kazi yangu ya ujasiri amali, lakini baada ya kufanya kazi yangu hiyo alikuwa anafanya kazi ya sabuni ana *packaging* yake nzuri tu, hata ile kuingiza sabuni kwenye boksi ameweka vizuri sana. Lakini mjasiri amali huyu anasema kwamba kazi yangu nimefanya kama miaka miwili, lakini kuna mtu anafanya bidhaa hii ya sabuni hizi hizi na anatumia alama yangu. Kwa hivyo, yeye anapata zaidi kuliko mimi.

Mhe. Spika, kama hapo pangekulikuwa na elimu ya kutosha wajasiri amali wetu bila shaka mama huyu asingeweza kuja akaanza kusikitika kwamba yeye kuna mtu anaiga ile bidhaa yake…

Mhe. Spika: Una dakika mbili Mheshimiwa.

Mhe. Khamis Juma Mwalim: Mhe. Spika, cha msingi hapa wajasiri amali wetu wanapokuwa na ubunifu wa kuandaa kitu chochote ni vyema ile alama ambayo wanaitumia waende ofisi inayohusika, na kwa sasa hivi kuna ofisi inaitwa Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali, hii ndio ofisi ambayo *responsible* katika masuala ya kusajili alama za biashara. Kwa sababu kama huyu angeweza kusajili alama za biashara asingeweza mtu mwengine kutumia alama ile.

Mhe. Spika, dakika mbili sitoweza bila shaka kuendelea na kuchangia hotuba hii, lakini kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Pangawe naikubali hotuba ya Mhe. Rais, asilimia mia kwa mia. Ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Spika, ahsante. Awali ya yote kwanza napaswa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kutuamsha tukiwa wazima wa afya kwa kutumiza majukumu yetu.

Mhe. Spika, natoa shukurani zangu za dhati kwako kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Baraza hili la Wawakilishi. Pia shukurani zangu za dhati nazipeleka kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein kwa ushindi mnono alioupata kupitia uchaguzi wa marudio.

Vile vile, natoa shukurani zangu za dhati kwa mzee wangu Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa kuchaguliwa tena kuwa Makamu wa Pili wa Rais, namuombea kila la kheri aweze kutimiza majukumu ipasavyo.

Pia, sitokuwa mwema kama sitowashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Ziwani; Shehia zote sita ikiwemo Ndagoni, Wesha, Kwale, Michungwani, Ziwani na Mbuzini kwa kujitokeza kwa wingi kwenda kunichagua kuwa

Mwakilishi wao wa Jimbo lao la Ziwani, pia kukichagua Chama cha Mapinduzi ili kuhakikisha kwamba kinashika dola na kuendelea. (*Makofi*)

Mhe. Spika, mimi nasema hotuba hii ya Mhe. Rais ni sawa na mtoto mchanga, haina kasoro hata kidogo, ni hotuba nzuri iliyokamilika kila kitu.

Mhe. Spika, mimi nijikite kwenye suala la uvuvi. Mhe. Rais alizungumza hapa katika hotuba yake kuwapatia wavuvi vihori vya kulimia mwani, wakulima wa chaza, na ufugaji wa majongoo kwa ajili ya kuwapatia mikopo hawa.

Mhe. Spika, uvuvi nalo ni suala ambalo kwamba ni ajira kwa wananchi wetu wanaotegemea suala la uvuvi, ni suala lenye kipato kabisa, hili ni kwamba waziri atakayeteuliwa aliweke mstari wa mbele kabisa, kwa sababu tunategemea karafuu katika uchumi wetu wa Zanzibar na utalii. Lakini kuna majongoo haya majongoo yana faida sana, kwa kuongeza kipato cha nchi yetu. Mhe. Spika, kuna majongoo yanafika hadi kilo 100,000/=, kuna mengine ni 180,000/= hayashuki thamani sana. Kwa hiyo, Mhe. Spika, nadhani hili jongoo nalo lingepewa kipaumbele na hawa wafugaji wa majongoo wakapewa mitaji ya uhakika ili kuendeleza pato hili.

Mhe. Spika, suala jengine ni la afya. Kutokana na hotuba hii ilivyo nzuri mimi nadhani hakuna sababu tena ya mwananchi yeyote wa Zanzibar hii kwenda katika hospitali ya serikali akaambiwa nenda kanunue dawa. Ukiangalia *dispensary* zile unakuta dawa zile unanua lakini kwa bei iliyokuwa ya juu, sasa huku kwenye serikali iweje zikosekane dawa zile huku kwenye *dispensary* ziwepo. Kwa hiyo, Mhe. Spika naomba waziri atakayeteuliwa kwenye Wizara ya Afya awe makini na hilo ili wananchi wetu wasisumbuke kwenye masuala ya ununuaji hata kidogo.

Mhe. Spika, niende kwenye suala la uwajibikaji. Mhe. Rais alizungumza humu katika hotuba yake kwamba uwajibikaji nao ni suala la kupewa kipaumbele. Mhe. Spika, mimi nalikubali hilo suala la uwajibikaji kwa sababu hivi sasa kule kwetu Ndagoni katika Mkoa mzima wa Kusini Pemba, sehemu inayoongoza kwa suala la migomo ni Ndagoni. Wananchi wetu hususan wanachama wetu wa Chama cha Mapinduzi wakipanda gari wanashushwa na kuambiwa madereva nenda kaoshe gari yako umepakia mbwa. Kwa hiyo, naomba Mhe. Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa walioko katika Wilaya ile walitizame suala hili na kulifanyia kazi haraka ipasavyo, kwa sababu wale wananchi wetu wananyanyasika, wanateseka na wanaonewa hasa kusema la ukweli. Kwa hivyo, naomba suala hili Mhe. Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa wasingoje waziri kuteuliwa anayeshughulikia masuala haya, ikiwezekana hata ruti ya ile Ndagoni ifutwe kabisa kama ni kukosa wakose wote.

Kwa hiyo, Mhe. Spika, mimi sitaki niseme mengi, kwa sababu hii ni mara yangu ya kwanza na namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kusimama hapa.
Kwa hiyo, Mhe. Spika kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Ziwani walionichagua na wasionichagua naunga mkono asilimia mia moja, na kama kuna nyengine ya zaidi pia naongezea kuiunga mkono hotuba hii Mhe. Spika.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Mhe. Spika, ahsante kwanza na mimi sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema na salama na tukaweza kufika katika kikao hiki pakiwa na amani nchini.

Mhe. Spika, pia sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu na kumtakia rehema Mtume wetu Muhammad (*S.A.W*) kwa kuweza kunipa nafasi hii adhimu ambayo nimekuwa nikiitafuta kwa muda mwingi kuweza kuwatumikia wananchi wa jimbo langu la Mgogoni.

Mhe. Spika, pia napenda kumpongeza Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein na Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli pamoja na Makamu wa Rais Balozi Seif Ali Iddi kwa kuweza kuchaguliwa kuiongoza nchi ikiwa na amani kabisa.

Mhe. Spika, pia sina budi niwashukuru wananchi wa jimbo langu hasa wa CCM pamoja na wale wapenda amani na maendeleo kwa kuweza kuniamini, kunipa kura kwa wingi hadi kufikia asilimia 95.6 katika jimbo langu. Ambapo kuwa fursa hii isingepatikana kama kungelikuwa hakuna utulivu katika nchi.

Pia, niwashukuru na niwapongeze mke wangu Bi. Asha Abdalla Ali ambaye alikuwa mvumilivu pamoja na watoto katika kipindi cha kampeni iliyokuwa kubwa na katika mazingira magumu. Aliweza kunituliza na kunipa moyo

kwamba niendelee, na mimi nikaendelea na mapambano mpaka leo *alhamdulillah*. Pia nikishukuru Chama changu cha Mapinduzi na Halmashauri Kuu ya Taifa kuniteua nikaweza nikasimama tena kwa mara ya pili katika ulingo huu. Aidha na Jumuiya ya Wazazi nisiisahau pia. (*Makofi*)

Mhe. Spika, niendelee kumshukuru Mwalimu wangu Maalim Mbarouk Ali, Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa kwa wazo lake la kuweza kunishawishi na kuweza kuingia hapa na nikamkubalia, nashukuru sana na nampongeza sana.

Kabla sijaendelea na michangio katika hotuba ya Mhe. Rais aliyotuwasilishia naiunga mkono kwanza asilimia mia moja na hamsini, na ninaiomba serikali hotuba hii ipelekwe katika mawizara na taasisi zote za Unguja na Pemba, kwani ni dira ambayo itatufikisha tunapokwenda kama tutabadilika, na tubadilike.

Mhe. Spika, baada ya hayo naomba nichangie katika suala zima la elimu na hasa nikizingatia kama vile ni mzazi, naanza na Skuli za Maandalizi. Elimu hii ni muhimu kupewa kipaumbele, katika kitabu hiki imezungumzwa kwamba kuna mazuri yanatendeka lakini nilivyoiangalia hotuba hii zinaangaliwa sana zile skuli za serikali.

Mhe. Spika, ninakotokea huko Pemba mimi ni kiongozi wa Skuli za Maandalizi ambazo zimeanzishwa na jamii baada kushawishiwa na kuanzisha skuli za jamii na Shirika la *Aga Khan Foundation*, na tukalikubali tukaanzisha skuli hizi. Lakini skuli hizi hadi leo hii zimekuwa zikijitahidi sana katika kutoa wanafunzi wazuri, ukisikia mwanafunzi ametoka katika michepuo basi anatokea skuli za maandalizi tena kule kwa jamii nao wanapiga hatua kubwa sana.

Vile vile, wanafunzi hao wanadiriki kufikia elimu ya Chuo Kikuu, lakini sasa hawa waliowaandaa hawa walimu hawana matunzo mazuri kwa sababu ni skuli za jamii malipo yao ni machache. Mwalimu anafika hadi kupokea 20,000/= kazi ambayo ni kubwa na ya ulezi kulichukua jiwe mpaka ukaweza kuliambia geuka likageuka, ni kazi waliyonayo walimu wa maandalizi. Ni kazi ambayo inawarahisishia walimu wa skuli za msingi kupata mwanafunzi kuendelea naye, ni tofauti kabisa mwanafunzi ambaye hajapata kupita skuli za maandalizi na yule aliyekwenda moja kwa moja skuli za msingi inakuwa tofauti kupokea kwao kwa elimu.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Rais Wizara hii ya Elimu atakapoipangia waziri na hili aliangalie, wale walimu hawana mshahara basi angalau waweze kupatiwa ruzuku kwa kila mwezi nao ziweze kuwasaidia kwa kuwatia motisha, miaka 15 kiasi hivi hawajarudi nyuma.

Mhe. Spika, nikiendelea kwenye elimu mimi naipongeza serikali kwanza kuanzisha mfuko huu wa elimu ya juu. Elimu ya juu ni elimu ambayo ni muhimu sana katika nchi yetu, lakini tuna malengo hapa kwamba itapofika 2020 itafanywa wafikie 22,404. Mimi naipongeza hii lakini tuangalie kufika idadi hii tu mimi nisingependelea kwamba ifike idadi tu lakini pia iboreshwe. Kwa sababu leo Bodi ya Mikopo ya Zanzibar inapotoa mkopo kwa mwanafunzi hapati hata asilimia 50 ya mahitaji yake. Matokeo yake mzigo ule unamrudia kwa mzazi ambaye ni mkulima wa kawaida, ni vigumu kusoma mwanafunzi yule katika mazingira mazuri. Kwa hiyo, naiomba serikali pamoja na kuongeza idadi lakini bora tufanye idadi chache lakini watakaosoma na kukamilisha bila tabu. Hili ni ushauri naiomba serikali iangalie vizuri.

Mhe. Spika, nirudi katika suala jengine kwa kuchangia hotuba hii katika uimarishaji wa miji Zanzibar. Kwanza anasema Mhe. Rais katika hotuba hii kama amenifilisi mimi, maana kabla kuingia katika chombo hiki nilikuwa najiuliza ni lini serikali au mtu yeyote akatokezea aimarishe miji yetu hii kama vile Marehemu Karume Rais wa Kwanza wa Zanzibar. Kwa sababu tunaangalia muda mchache alipoanzisha majengo haya kama vile Michenzani na Wete kule Pemba na mengineyo watu wengi wameweza kukaa pahali pamoja na ardhi ikabakia.

Sasa jambo kama hili leo limetokezea hapa naona kwetu ni faraja, kwani ardhi yetu ni chache lakini wananchi ni wengi. Kumbukumbu inasema kwamba wakati inafanyika Mapinduzi Unguja na Pemba tulikuwa kama watu 350,000 leo tupo 1,500,000 pengine. Ni vyema kuitazama ardhi hii ambayo kuwa kila siku inabomoka kwa bahari na leo tukaitumia vizuri, tutakapojenga miji hii ardhi itakayobakia tutafanya kwa shughuli nyengine za uzalishaji maji na kuboresha uchumi.

Mhe. Spika, baada ya hapo nirudi niende sehemu ya kilimo. Kilimo na biashara karibu vinakwenda sambamba, kama tunavyosema kuwa kilimo ni uti wa mgongo na kilimo mimi nasema ni ibada. Kwa sababu hapa tuliokalia humu ndani vingi vinatokana na kilimo, tukataka tusitake.

Mhe. Spika, ni vyema suala hili tukalipa kipaumbele kama itavyowezekana hasa ninaposemea ni pale tulipozungumza kwenye masuala ya biashara kwamba serikali itaongeza vipaumbele katika hali ya mazao ya kibiashara. Sasa hivi serikali inatafuta ajira na ajira ziko za serikali na watu binafsi, hivyo ni vyema katika kuongeza yale mazao ya viungo tukaongeza zao la *vanilla* ambalo mimi mwenyewe nimelianza hilo zao na pia zao la hiliki. Kama tutatumia mashamba yetu ya mikarafuu tutakuwa tunatumia ile dhana ya kilimo mchanganyiko, mikarafuu yetu itaweza kunawiri na wakati huo huo ardhi yetu ndogo tunaitumia kwa mambo mengi. Ni vyema suala hili wizara itakayopewa jukumu hili basi iliangalie vyema na elimu itolewe kwa wajasiriamali na wananchi wetu wote.

Mhe. Spika, baada ya hapo nizungumze kwenye wajasiri amali. Wajasiri amali nashukuru kwamba wametajwa katika kitabu hiki kwa kweli nao wana mchango mkubwa katika Taifa katika kuimarisha uchumi wetu, lakini nao wanahitaji kutafutwa. Ni imani yangu sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tunaotoka majimboni tuwatafute ili tuwape changamoto zao tuisaidie serikali katika hili ili na wao watoe mchango mkubwa wa kuweza kufanya vile ambavyo vinatakiwa, lakini tusisahau kwamba lengo la kubadilika liwepo tubadilike.

Mhe. Spika, mimi naona kwa leo niweze kufikia hapa na nishukuru sana, naiunga mkono tena hotuba hii kama nilivyosema asilimia mia moja na hamsini kwa mia. Ahsante.

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia hotuba ya Mhe. Rais, lakini kabla ya kuchangia kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu muumba mbingu na ardhi ambaye yeye ametuwezesha kufika hapa leo hii.

Pia, niwashukuru wananchi wote wa Jimbo la Chukwani kwa kunichagua mimi kuwa Mwakilishi katika Baraza lako hili Tukufu.

Vile vile, shukurani zangu za dhati nazipeleka kwa familia yangu kwa kuniunga mkono katika kipindi chote cha harakati za uchaguzi, lakini pia nisiwe mwizi wa fadhila nataka niwashukuru wale wote waliojitolea kwangu kwa hali na mali kuhakikisha Jimbo la Chukwani kuwa ni jimbo la CCM kupitia mimi Mwanaasha Khamis. Nawashukuru sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika, lakini pia nitoe shukurani zangu na pongezi za dhati kupitia kwako Spika, Naibu Spika naWenyeviti wa Baraza pamoja na Rais wa Zanzibar kwa kuwateua Wajumbe saba, nampongeza sana. Pia pongezi zangu za dhati nampongeza Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa kuwa Makamu wa Pili wa Rais katika miaka hii mitano ijayo. Nawapongeza sana.

Mhe. Spika, narudi tena katika hotuba ya Rais, wachangiaji wengi wamechangia vizuri na hotuba ya Rais ni nzuri imegawika katika kila sekta, imewahusisha vijana, wanawake, watu wenye ulemavu na jamii zote kwa jumla. Mimi nilitaka nigusie kidogo katika suala zima la elimu.

Mhe. Spika, suala la elimu hotuba hii imezingatia sana masuala mazima ya upatikanaji wa elimu na fursa zote zimetolewa katika elimu, lakini nilitaka nizungumze suala hili la elimu kwa watu wenye ulemavu. Watu wenye ulemavu ni masuala mtambuka hayawezi kushughulikiwa katika sekta moja ni sekta ya kila sehemu na walemavu wanahitaji msaada katika kila eneo ambalo limezunguka nchi yetu. Tuanze kwenye suala zima la elimu.

Katika kipindi kilichopita serikali iliweka elimu mjumuisho katika skuli maalum ambazo ziliwekwa kuwasaidia watu wenye ulemavu, lakini bado kuna changamoto. Sasa naiomba serikali kupitia hotuba hii ya Mhe. Rais aliyoitoa juzi liangaliwe suala la changamoto ambazo zinawakabili watu wenye ulemavu katika skuli ambazo zilichaguliwa maalum kuwa wanafunzi wenye ulemavu wawepo katika skuli zile. Kwa hiyo, bado kuna changamoto nyingi kuhusiana na vifaa vya watu hao au visaidizi. Naiomba serikali ilichukue hili na iliangalie ili watu wenye ulemavu wapate fursa ya kusoma kwa ile hali waliyokuwa nayo.

Pia, nilitaka kuzungumza kuhusu suala la afya. Naomba serikali iangalie kuhusu afya ya mama na mtoto bado kuna changamoto nyingi katika mahospitali yetu na nyingi huwa zinawakumba akinamama waja wazito. Kwa hiyo, naiomba serikali kupitia hotuba hii ya Rais, waziri atakayeteuliwa basi aangalie sana watoto na akinamama waja wazito ili wapate ile haki stahiki wanapokwenda mahospitalini.

Vile vile, katika hotuba hii nimefurahishwa sana kuwa ametoa kipaumbele kikubwa kuhusu wanawake, lakini kabla ya hotuba hii Baraza lako Tukufu tayari Wajumbe waliomo humu waliona kuwa wanawake wana fursa sawa au haki ya kuingizwa katika maendeleo ya kiuchumi na nyadhifa mbali mbali katika Baraza hili. Niwapongeze Wajumbe wote ambao wamefanikisha kwanza kukuchagua wewe mwenye jinsia ya kiume na wakamchagua Naibu Spika mwanamke. Halikadhalika wenyeviti wa Baraza hili ni wawili, lakini pia imezingatiwa *gender* kuna mwanamke na mwanamme nawapongeza sana.

Mhe. Spika, suala jengine ninalotaka nizungumze ni kwamba mengi yamezungumzwa lakini nilikuwa nataka nizungumze kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Chukwani kukukaribisha wewe katika Jimbo hili ambalo upo. Hapo upo juu ya kiti chako ni maeneo yetu ya kujidai nikiwemo mimi Mwakilishi wa Jimbo la Chukwani karibuni sana, na Waheshimiwa Wajumbe wote katika Jimbo hili kwa niaba ya wananchi tunakukaribisheni. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mwisho kabisa kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Chukwani tunaiunga mkono hotuba hii ya Mhe. Rais kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Mohamed Ahmada Salum: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii adhimu na mimi kuchangia hotuba ya Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein. Awali ya yote sina budi na mimi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na leo kuweza kusimama katika Baraza lako Tukufu na kutoa mchango wangu kwa ajili ya kuchangia hotuba hii ya Mhe. Rais.

Kwanza natumia nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia fursa hii adhimu ambayo watu wengine waliitaka hasa katika Jimbo langu la Malindi hawakuweza kuipata. Kwa hiyo, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru wananchi wa Malindi kwa kuniwezesha kunipa kura za kishindo kuweza kuingia katika Baraza hili ili niwawakilishe katika kupiga hatua mbele zaidi za maendeleo kwa nchi yetu.

Pili, nachukua nafasi hii kukushukuru wewe Mhe. Spika kwa kupata ushindi wa kishindo na kuweza kukaa katika kiti hicho kitukufu cha muhimili mkubwa wa nchi yetu. Vile vile, bila ya kuwasahau Naibu Spika na Wenyeviti wake wawili, wote nao nawapa hongera sana kwa ushindi wao wa kishindo.

Vile vile, nitakuwa mwizi wa fadhila kama sitompongeza mwalimu wangu wa siasa Balozi Seif Ali Iddi kwa kuteuliwa tena kuwa Makamu wa Pili wa Rais. Kusema kweli wananchi wamejenga imani kubwa sana kwake yeye na kuwa sisi sote kwamba ile kasi ya maendeleo aliyoitaka Rais wetu Dkt. Ali Mohamed Shein tutaifikisha pale tulipoikusudia hasa katika kuitekeleza dira ya 2020.

Mhe. Spika, moja kwa moja sasa nianze kuichangia hotuba ya Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, kama tunavyojua kwamba hotuba hii ni shamba darasa kwetu sisi, ambalo shamba hili lina rutba kila aina na mimea tofauti ambayo sasa kama tutaitumia vizuri basi wananchi wote watatoshelezeka na mimea hiyo na baadae kupata neema, na nchi yetu ya Zanzibar kuendelea kuwa mbele kimaendeleo.

Nikianza katika sekta ya uchumi sekta ambayo ni muhimili mkubwa katika Taifa letu. Mimi kidogo ningependa kuchangia katika kupanua vyanzo vya mapato. Sote tunajua kwamba uchumi wa Zanzibar ni uchumi wa visiwa ambao unategemea sana huduma, sasa ili kuziendeleza huduma hizi tunahitaji tuwe na watu wabunifu sana katika sehemu yetu hii ya mapato. Kwa hiyo, mimi ningeshauri sana kufichua wigo wa kupanua vyanzo vya mapato hasa katika mambo ya kuanzisha, wenyewe wanasema benki za ufukweni na vile vile katika kutilia mkazo zaidi watu wangesema hii *free port.*

Mhe. Spika, najua kwamba wazo hili lilianza zamani sana toka kipindi cha Dkt. Salmin Amour Juma lakini kwa bahati mbaya tunaweza kusema kwamba kuna vikwazo ambavyo mbele yetu vinaweza kusababisha hili lengo tulilokusudia kulitekeleza mpaka sasa lisitekelezeke. Nina imani kubwa kwamba Mwenyezi Mungu akitujaalia tukiweza kuchimba mafuta na gesi basi kwa kiasi kikubwa uchumi wetu utakua sana.

Sote tunajua kuwa nishati ya gesi asilia na mafuta ni nishati ambayo inawavutia sana wawekezaji duniani kote kama vile *UAE*, Qatar, Bahrain zimeweza kuendelea sana kutokana na nishati ya gesi asilia na mafuta. Mimi nitachoomba Baraza lako Tukufu litunge sheria ambazo zitaweza kutetea maslahi ya wananchi wa Zanzibar katika gesi na mafuta. Sote tunajua kwamba mafuta na gesi asilia ni nishati ambayo ina hatari zake, wanaweza kuja wawekezaji wakawekeza lakini baadae wananchi wasifaidike. Nina imani kwamba chini ya uongozi imara wa Dkt. Ali Mohamed Shein mambo haya hayatafikia kwa Zanzibar, na Zanzibar itaneemeka sana na kuwa zaidi ya Singapore, Brunei au Mauritius *In Shaa Allah*.

Mhe. Spika, nikitoka hapo naamua kuzungumzia uwekezaji. Kama tunavyojua tuna maeneo mengi tu ya uwekezaji kama Micheweni, Fumba, ambayo mpaka hivi sasa mengine yamefikia hatua nzuri sana kama Fumba, lakini Micheweni kwa kipindi kirefu bado eneo hili halijaendelezwa kwa sababu hamna mtaji wowote pale au mradi ambao uko mpaka sasa hivi. Mimi ningetoa wito kwamba serikali ya Dkt. Ali Mohamed Shein atakayoiunda ihakikishe kwamba tunayatangaza maeneo haya huru kwa wawekezaji kutoka nje ili waje kuwekeza, kwani nina imani kubwa kama ilivyokuwa Mauritius na Seychelles walivyopata wawekezaji, na sisi iwapo tutayatangaza vizuri maeneo hayo basi watu wengi kutoka nje ambao wana uwezo wa kuwekeza watakuja. Kama nilivyosema sekta ya biashara ni sekta muhimu sana katika uchumi wetu wa Zanzibar.

Kwanza mimi napenda kuwashukuru wafanyabiashara wote ambao wanachangia pato la Taifa kwa kulipa kodi kihalali kabisa. Kwa hiyo, mimi napenda kutoa wito zaidi kwa wafanya biashara wajue hii Zanzibar itajengwa na Wazanzibari wenyewe, wajitahidi sana kulipa kodi kwani watapolipa kodi ndio watasaidia huduma nyingi za kijamii na kiuchumi kuweza kufanikiwa kwa wananchi wetu wa Zanzibar.

Vile vile, kwa ufupi tu napenda kuzungumzia masuala ya miundombinu. Sote tunajua kwamba miundombinu yetu sasa hivi imepiga hatua kubwa kimaendeleo, lakini licha ya hivyo bado kuna changamoto ambazo zinatukabili katika kukamilisha miundombinu hasa barabara na vile vile masuala ya bandari. Kwa hiyo, mimi ningewashauri sana wataalamu wetu waliopo ndani na wale ambao watapata nafasi ya kuwakilisha katika sekta hizi kupitia mawaziri wahakikishe wanakuwa wabunifu, kwani miundombinu hii utakuta kwamba ina gharama kubwa sana, tunaifanya miundombinu lakini baadae unakuta haifuatiliwi katika kuimarisha na kuikarabati.

Mhe. Spika, mfano mzuri utakuta njia nyingi zimejengwa lakini bahati mbaya magari yanayopita pale yanazidi kiwango kile cha barabara kinachotakiwa, zinapita gari zaidi ya tani kumi ambazo hizo zinafanya uharibifu na baadae inakuwa gharama kubwa zinatakiwa katika kutengeneza tena miundombinu. Kwa hiyo, mimi ninanasihi sana kwamba tuweke vigezo maalum vya kuhakikisha kuwa miundombinu hii inaendelea kudumu kwa muda mrefu, na vile vile kuwa magari yanayotumika katika barabara hizo yanalingana na kiwango cha barabara au uzito unaotakiwa kupita pale.

Mhe. Spika, kwa ufupi mimi ningependa kuzungumzia suala la afya. Sote tunajua kwamba afya ni muhimu kwa binadamu lakini inasikitisha sana kuona maradhi ya kipindupindu yameenea sana hasa Wilaya ya Magharibi 'A' na 'B'. Watu wanasema kwamba Uislamu ni nadhifu na tujinadhifishe. Kwa hiyo, maradhi ya kipindupindu wasomi au wataalamu wa afya wanasema kwamba yanatokana na uchafu.

Mimi kwa bahati nzuri huwa natembelea sana maeneo ya Kinuni, Mtopepo na mengine mengi utakuta kwamba mazingira yake sio ya kuridhisha sana, kuna nyumba nyengine hazina vyoo, nyengine zinatiririsha maji machafu na nyumba nyengine wanasubiri siku za mvua wasafishe vyoo vyao na kumwaga maji nje na kusababisha tatizo la kipindupindu kuendelea Zanzibar hata kipindi cha kiangazi.

Mimi nashauri sana Halmashauri hasa Wilaya ya Magharibi wafuatilie sana suala hili la kuhakikisha kwamba nyumba zote zinakuwa na vyoo ambavyo vina mashimo na maji machafu hayatoki nje. Kwa hivyo, nina imani kubwa sana iwapo tutaweza kufanya ufuatiliaji basi maradhi haya ambayo ni ya uchafu yataondoka Zanzibar.

Mhe. Spika, kusema kweli mimi nimefurahishwa sana na Mhe. Rais kutwambia kwamba katika awamu hii kipimo cha *DNA* kitafanyiwa kazi na kununuliwa. Kusema kweli hili ni suala ambalo huwa linaniumiza sana kuona watoto wadogo na wanawake wakidhalilishwa na ndugu zetu kwa sababu ya tamaa zao za nafsi. Utawakuta watoto wadogo wanaharibiwa lakini wakienda hospitali wanaambiwa kwamba chombo cha kuthibitisha kuwa mtoto huyu kafanyiwa udhalilishaji hakipo.

Mhe. Spika, mimi nina imani kuwa tukiiga ubunifu wa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. John Pombe Magufuli alioutoa alipokuwa akizungumza na wananchi wa Dar-es-Salaam alipotoa wazo kwamba kuna mambo mengine hata sisi wenyewe kama viongozi tunaweza kuchangia.

Mimi nahisi kwamba kipimo cha *DNA* hakizidi shilingi 300, milioni iwapo sisi Wawakilishi na viongozi wengine wa serikali tutatoa kwa mwezi japo shilingi laki tano basi nina imani kipimo hiki kitapatikana kwa haraka sana hata kabla ya Bajeti ya Serikali haijaamua. Zanzibar ni yetu itajengwa na Wazanzibari wenyewe, na vile vile kama tutajitolea nina imani kuwa tutakuwa na moyo wa kujitolea, bora kuwa na kidogo tukagawana kuliko kuwa na kingi tukaanza kugombania.

Mhe. Spika, katika kuendelea kuchangia vile vile ningependa kuchangia suala la kilimo. Kilimo ni uti wa mgongo na tunajua asilimia 31 ya pato la Taifa linategemea kilimo. Sasa mimi natoa ushauri, tuna upungufu sana wa mabwana shamba na mabibi shamba. Lengo la ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015-2020 ni kuhakikisha kwamba katika kila shehia sehemu ya kilimo tunakuwa na bwana shamba au bibi shamba ambao watawasaidia wakulima. Sasa ili kulifikia lengo hili mimi nashauri sana Vyuo vyetu hivi vya Amali na Vyuo Vikuu vihakikishe kwamba vinasomesha somo la kilimo, na vile vile tuhakikishe kwamba kama inawezekana tuweke dirisha dogo la kuwa na kama kijibenki kile cha kilimo kama walivyo nchi zilizoendelea kama vile Vietnam na China, kwani bila ya kupata mitaji mikubwa hawa wakulima wataendelea kutumia kilimo cha kienyeji na hivyo hata pato lao kuwa dogo.

Vile vile, nachukua nafasi hii kuwashukuru sana wakulima wa kilimo cha biashara hasa matikiti maji hapa Zanzibar. Kusema la kweli kilimo hichi kimewainua wananchi wengi wa kipato cha chini, na hivi sasa wamekuwa wanaisifu sana Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, isipokuwa tu wanasema kwamba wapatiwe wataalamu ili yale matikiti maji wanayoyazalisha yawe bora kama yale yanayozalishwa na wenzetu Tanzania Bara.

Vile vile, nitazungumzia kidogo kuhusu mifugo, sote tunajua kwamba Zanzibar ni kisiwa lakini hata hivyo wenzetu Botswana na Afrika ya Kusini wameendelea sana katika mifugo kwa kutumia eneo dogo lakini kwa utaalamu wa mifugo. Kwa hivyo, wanazalisha ngombe ambao ng'ombe wale wanatoa nyama nyingi na vile vile wanatoa maziwa mengi. Sote tunajua kwamba mfanyabiashara Bakhressa kafungua kiwanda cha maziwa, lakini kwa bahati sana maziwa yanayopelekwa pale na wakulima wetu hayatoshelezi kabisa, unakuta anaagizia maziwa kutoka Bara. Hivyo, kumtilia gharama zaidi za uzalishaji.

Mimi ningeshauri hawa mabwana mifugo nao waendeleze zaidi ili kuhakikisha kwamba Zanzibar tunakuwa na wataalamu wengi ambao watarahisisha kupata mifugo bora na ambayo itatoa kiwango kikubwa zaidi cha maziwa na nyama.

Mhe. Spika, vile vile, ningezungumzia mazao ya habarini, sote tunajua kwamba wenzetu China sasa hivi wamepiga hatua kubwa sana katika uvuvi huu wenyewe wanasema uvuvi wa kutumia mashamba ya kufuga chaza na kufuga kamba. Sote tunajua kwamba chaza na kamba ni biashara kubwa sana ambayo inaweza kutuingizia pato kubwa sana kwa nchi yetu na vile vile kwa wananchi wa kawaida.

Mimi ningeshauri sana tuendelee kutoa utaalamu kwani sasa hivi tuna mashamba mengi si haya ya ufugaji na mengine nimeyakuta Pemba Gando kule yako Bumbwini na sehemu nyengine nyingi tu. Tuendeleze wataalamu wetu kwa kuwapa elimu ya kutosha ili kuhakikisha kwamba tunakuwa na mashamba mengi zaidi ambayo yatasaidia wananchi wetu wa kipato cha chini kuondokana na umasikini.

Kwa haraka zaidi vile vile ningependa kuzungumza suala la elimu. Sote tunajua kwamba hivi sasa tuna Vyuo Vikuu vingi tu lakini Vyuo Vikuu hivi haziwezi kuwa na tija ikiwa hatutotoa wataalamu bora. Mimi nashauri sana Vyuo hivi viendelee kutoa fani tofauti hasa fani ya Sayansi na uhandisi, kwani kama tunavyojua ulimwengu unaendelea kutokana na teknolojia, na teknolojia hiyo haiwezi kupatikana isipokuwa katika masomo ya Sayansi. Kwa hiyo,

mimi nahimiza sana vyuo vikuu vyetu hivi viangalie zaidi sekta ya Sayansi na Teknolojia na vile vile sekta ya udaktari.

Mhe. Spika: Mheshimiwa umebakiwa na dakika mbili.

Mhe. Mohamed Ahmada Salum: Ahsante sana Mhe. Spika. Kwa kuwa muda wangu umekuwa mchache na leo ni siku ya Ijumaa nitamalizia kwa kutoa nasaha zaidi kwa wananchi wote wa Zanzibar.

Kwani Mhe. Rais wetu amesema kwamba amani na utulivu. Atahakikisha kwamba anavilinda kwa nguvu zake zote. Mimi nawaambia tu wananchi wote wa Zanzibar kwamba Mwenyezi Mungu anatushurutisha kwamba tumtii yeye na Mtume wetu na viongozi ambao sisi wenyewe tumeshawachagua.

Kwa hivyo, nitawaomba sana wananchi wa Zanzibar wamuunge mkono Dkt. Ali Mohamed Shein na wasikubali kusikiliza maneno ya chokochoko. Huyu ni Rais ambaye amechaguliwa kwa kishindo, kwa asilimia 91.4 na wananchi wa Zanzibar. Kwa hiyo huyu Rais amepata ridhaa ya mola wetu mtukufu, kwa hiyo nao wanatakiwa wamuunge mkono. (*Makofi*)

Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema:

"*Waataswimuu bihabillahi jamian walaa tafarraquu, wadhkuruu niimatallahi alaykum, idhkuntum aadaan faallafa baina quluubikum faas-bahtum biniimatihii ikhwaana, wakuntum alaa shafaa hufratin mina-nnar faanqadhakum min-haa"*

Kwamba " tushikamane na kamba ya Mwenyezi Mungu kwani hapo mwanzo tulifarikiana, lakini kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu akatukusanya pamoja". Kwa hiyo, tusiache kuichezea shilingi shimoni, hakika tukiichezea shilingi shimoni ikianguka hatutoipata tena.

Amani ya nchi yetu ni muhimu kwetu sote, na nina imani kubwa wananchi wote wa Zanzibar kupitia vyama vyao vya siasa na itikadi zao na madhehebu tofauti ya dini watamuunga mkono daktari Ali Mohamed Shein kuhakikisha kwamba amani na utulivu unapatikana. (*Makofi*)

Mwisho kabisa kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Malindi na mimi mwenyewe binafsi naiunga mkono hotuba ya Mhe. Rais kwa asilimia mia. Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi adhimu. (*Makofi*)

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia leo kusimama katika ukumbi huu wa Baraza la Wawakilishi kwa mara ya kwanza kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa hilo. Pili nikushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hiyo.

Mhe. Spika, kwanza niishukuru familia yangu kwa kuniwezesha wakati wa kampeni za uchaguzi kwa kunipa mashirikiano mazuri na mpaka Mwenyezi Mungu kajaalia nimefanikiwa. (*Makofi*)

Mhe. Spika, napenda zaidi niwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Bububu hasa shehia ya Bububu, Shehia ya Dole, Shehia ya Mbuzini, Shehia ya Kizimbani na Shehia ya Kijichi kwa kunipa mashirikiano mazuri na kunipa kura kwa asilimia 91, nawashukuru sana.

Mhe. Spika, pia nimshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapindizi kwa kupata kura za kishindo na kuwa Rais wetu wa awamu ya sita wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, nashukuru sana kwa hilo.

Mhe. Spika, pia nimshukuru sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kumteua Mhe. Balozi Seif Ali Idd kuwa Makamu wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Wananchi wengi wapenda amani

wa Zanzibar walikuwa wanafikiria nani atakuwa Makamu wa Rais, lakini tumpongeze sana Mhe. Rais wetu kumrejesha tena katika kazi hii ya kulitumikia Taifa letu la Zanzibar.

Mhe. Spika, pia nimshukuru Rais wa Zanzibar kwa uteuzi wake wa Wawakilishi saba ambao katuwekea au katuongezea hesabu yetu ndani ya Baraza letu hili. Wawakilishi hawa ni wazuri, wana uwezo, Mwenyezi Mungu awajaalie watusaidie watuongoze katika kuongoza Baraza letu hili la Wawakilishi. (*Makofi*)

Mhe. Spika, pia niushukuru uongozi wangu wa Chama cha Mapinduzi kuanzia ngazi ya Tawi mpaka ngazi ya Taifa kwa kulipitisha jina langu kuwa Mwakilishi wa Jimbo jipya ya Bububu nawashukuru sana.

Mhe. Spika, niende moja kwa moja kwenye hotuba ya Mhe.Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliyotutolea hapa katika ukumbi wetu huu wa Baraza la Wawakilishi.

Kwanza nimpongeze kwa suala zima alilolitilia mkazo suala la kilimo. Wenzangu waliosimama hapa walisema kilimo ndio uti wa mgongo wa Taifa letu, na ni kweli ni asilimia 31 tunategemea sana kuwa wakulima wa nchi hii. Niseme wenzangu walizungumzia suala la pembejeo na mimi nataka niseme kuwa suala la pembejeo bado serikali inajitahidi kugharamia, lakini upatikanaji wake unaonekana bado ni mdogo. Mwenzangu kasema kipolo kimoja cha kilo 50 wanagawana wakulima watatu, hiyo ni kweli na mimi kwenye mabonde yangu ya Bumbwi Sudi na maeneo mengine bado unakuta kipolo kimoja cha mbolea wanagaiwa wakulima wanne. Tunasema sasa hivi tunataka ukulima wenye tija, kweli kipolo kimoja cha kilo hamsini mgawane wakulima wanne kutakuwa na tija kwenye kilimo.

Naomba sana serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hasara au gharama ambayo inatugharamia wakulima ifanywe iwe ya ukweli, ihakikishwe kila mkulima anapata mbolea kwa mujibu wa mahitaji yake, kuna watu wanalima heka tatu za kilimo cha umwagiliaji ukimpa kipolo kimoja bado hakijamtosheleza. Naomba sana serikali ili kilimo hiki kiwe na tija tujitahidi sana ili wakulima wetu wapate mbolea ya kutosha.

Pia, niende kwenye suala la ajira kwa vijana. Mhe. Spika, Mhe. Rais kasema atalipa kipaumbele sana suala la ajira kwa vijana. Ni kweli vijana walio wengi sasa hivi wanamaliza masomo lakini ajira serikalini zinakuwa ni ndogo. Ningeomba sana serikali itilie mkazo kuweka vyuo vya Amali kwa sababu watakapotoka vijana kwenye vyuo vya Amali wakishaelimishwa maana yake wapewe elimu sasa hivi maeneo mengi inaonekana kijana hata akitoka kwenye Chuo cha Amali anasubiri ajira serikalini. Kwa hiyo, tuwaelimishe ili vijana wawe wanapata mikopo wanajiari wao wenyewe.

Nikiondoka hapo niende kwenye masuala ya Ushirika. Ni kweli vikundi vya ushirika vipo vingi Zanzibar lakini baadhi ya vikundi bado havina usajili na vikundi vyengine vimepata usajili. Lakini wakati wa kupata mikopo au ruzuku yoyote kutoka serikalini aghalabu vinakuwa vile vikundi ambavyo labda vina muheshimiwa ana jina kubwa katika serikali hii ndio ambao wanapata mikopo.

Ningeomba sana kuwa mikopo hii itoke kwenye majimbo yote, ikiwa kutakuwa na vikundi 100 ambavyo vitapewa mikopo basi kila jimbo lipate vikundi viwili ili sote tuwe tunafaidika sawa sawa, lisiwe eneo moja tu pengine la Mhe. Haroun Ali Suleiman vikundi vyake 50 vyote vinapata mikopo, lakini kwenye jimbo la Mhe. Masoud Abrahman Masoud kwake hakuna kitu. Naomba sana suala hili tulitilie mkazo ili sote tufaidike kwa pamoja.(*Makofi*)

Suala la Mapato ya Serikali Mhe. Spika, bahati nzuri mimi nilikuwa mwenyekiti wa Halmashauri ya wilaya ya Magharibi. Kwa hivyo, naona jinsi gani mapato vile yanavyokusanywa. Ningeomba sana serikali iweke mkazo sana kwenye suala la mapato. Mapato ya serikali yakidhibitiwa vizuri basi serikali hii tunaweza tukajitegemea bila ya kutegemea serikali za nje kutusaidia. Kwa hiyo, naomba sana tutilie mkazo suala la mapato ya serikali.

Suala la amani na utulivu, Mhe. Rais kalisisitiza sana suala la amani na utulivu, bahati nzuri mimi hapa nina miaka karibu hamsini sasa hivi. Lakini toka nimezaliwa mpaka leo hii hatua niliyofikia nilisikia tu kuwa kuna vita vya Kagera, lakini hapa Zanzibar mimi sijaona kama kuna vita. Ningeomba sana Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kupitia vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vinapoona viashiria vya kuhatarisha amani ya nchi yetu, visiregee kusubiri ushahidi kamili. (*Makofi*)

Bahati nzuri sisi sote hapa tutakuwa mashahidi. Muamsho ulianza kidogo kidogo lakini ikawa serikali bado inawapuuzia mpaka ikawa sasa hata serikali hawaiheshimu. Lakini serikali ilipoamua sasa kufanya kazi yake kama serikali, kwa sababu serikali haitakiwi iregee, ilipoanza kuamua kufanya kazi kama serikali tumpongeze sana Mhe. Balozi Seif Ali Iddi suala lile liliondoka mara moja. Kwa hiyo, naomba sana suala la amani na utulivu katika nchi yetu bado serikali ikiona viashiria vinaanza viweze kudhibitiwa mara moja. (*Makofi*)

Mhe. Spika, niendelee kwa kulizungumzia suala ambalo kalizungumzia Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi suala la migogoro ya ardhi.

Suala la migogoro ya ardhi iko Zanzibar na itaendelea kuwepo na suala hili aghalabu huwa wanapelekewa masheha, madiwani pamoja na halmashauri, wenyewe Idara ya ardhi wanajifanya sio. Naomba sana migogoro hii ingekuwa haitokei kama ardhi yote imepimwa.

Ardhi, ikiwa imepimwa huwezi kwenda kuvamia eneo ambalo limeshapimwa na serikali. Lakini sasa ardhi zinaachwa kiholela watu wanajenga kiholela hatima yake serikali inakuja kupata kazi ngumu ya kupapatua. Mfano eneo la Kwa Nyanya, serikali iliweka mabango ya kuzuia kufanya shughuli zozote pale za wananchi. Lakini serikali hiyo hiyo inaangalia wananchi wanaanza kuchimba msingi, wanajenga mpaka wanahamia, halafu serikali hiyo hiyo inaenda kupiga X watu wahame.

Lakini kama serikali ingekuwa iko makini eneo lile wananchi wakiamua kujenga wanaondoshwa, mbona maeneo ya Jeshi watu hawavamii. Kwa hiyo, naomba sana serikali ipime ardhi yote, ili kila panapohitajika kufanyika shughuli za maendeleo basi tuweze kupatiwa ili kila mmoja ajue kile anachokifanya.

Mhe. Spika, nataka niseme tu kuwa nimpongeze sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ujenzi wa vituo vingi vya afya na vituo ambavyo sasa hivi viko katika kiwango. Bahati nzuri katika Jimbo la Mhe. Machano kule Bumbwi Sudi kuna kituo cha afya kizuri sana tu kimejengwa. Lakini nataka niseme tu kuwa tujitahidi sana vile vituo vipelekewe madaktari ambao wana uwezo. Kwa sababu viko vituo ambavyo sasa hivi unaweza ukakaa kutoka asubuhi saa mbili mpaka saa sita unaambiwa daktari hajafika. Kwa hiyo, wale waliopo hawana uwezo wa kuhudumia wananchi. Kwa hivyo, tujitahidi kama wenzangu walivyosema tusomeshe vijana wetu, ili vituoni wapelekwe madaktari wenye uwezo.

Pia, Mhe. Rais nakumbuka katika ziara yake katika Jimbo langu la Bububu muna kituo cha afya tulijenga halmashauri cha Mbuzini. Mhe. Rais alisema kile kituo kitakuwa kituo cha Wilaya, lakini toka alipotoka Mhe. Rais pale mpaka leo hakuna kilichofanyika. Ningeomba sana Waziri atakayebahatika kuteuliwa basi suala lile wakati ahadi ya Mhe. Rais ishughulikiwe ili liweze kutekelezwa. (*Makofi*)

Mhe. Spika, naipongeza hotuba ya Mhe. Rais aliyozungumzia sana suala la mikopo. Ningeomba sana hii mikopo Mhe. Mohamed hapa kasema kuwa wananchi wengi sasa wakulima wadogo wadogo wanalima matikiti na mboga mboga na mambo mengine, lakini bahati mbaya wanajitegemea wao wenyewe. Ningeomba sana wale vijana ambao wamejiamulia kujiajiri kwenye suala la kilimo na wao mabenki angalau yawape mikopo japo midogo midogo ili waweze kujiwezesha kuendeleza kilimo chao kidogo kidogo.

Mhe. Spika, mwisho, nimuombee dua na kumtakia kila la kheri Dkt. Ali Mohamed Shein katika kutuongoza serikali yetu ya Mapinduzi Zanzibar. Mwenyezi Mungu amjalie ampe umri mrefu ili atuongoze kwa salama na amani.

Mwisho wa yote niseme naipongeza hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Bububu tunaiunga mkono kwa asilimia mia. (*Makofi*)

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa nikiwa katika hali ya uzima.

Pia, nimshukuru mume wangu kwa kunipa ushirikiano pamoja na familia yangu kuanzia mwanzo mpaka hivi sasa. Pia niwashukuru wanachama wa Chama cha Mapinduzi wa Jimbo la Kiwengwa pamoja na wananchi wote kwa jumla kwa kunichagua kuwa Mwakilishi wa Jimbo la Kiwengwa. Kwani wameona kwamba ipo haja ya kuchagua mwanamke katika jimbo ili kuwaletea maendeleo katika maeneo tofauti. (*Makofi*)

Na hivi tumeona kwenye Baraza hili la Tisa kuna wanawake wa majimbo 7 na kumchagua Naibu Spika, kuwa mwanamke, hili nawapongeza sana.

Pia, Mhe. Spika, nikupongeze wewe binafsi kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Baraza la Wawakilishi. (*Makofi*)

Nami niungane na Wajumbe wenzangu waliotangulia mwanzo kuiunga mkono hotuba hii ya Mhe. Rais. Wao wamezungumzia mambo mengi sana yaliomo ndani ya hotuba hii, lakini mimi ningeweza kuchangia mambo mawili. Suala la maji safi na salama na suala la udhalilishaji wa wanawake na watoto.

Nianze na suala la maji safi na salama. Mhe. Rais katika hotuba yake alizungumzia kuendeleza huduma hii ya maji safi na salama katika maeneo ya mijini na vijijini. Suala hili ni kweli kwamba wananchi wengi wa Zanzibar wana usumbufu wa maji safi na salama, kwani maji haya ni suala zima la kiafya linalotukabili sisi wananchi wote kwa jumla. Mhe. Spika, katika maeneo mengi kuna visima vingi vimechimbwa lakini hadi hivi sasa bado havijamalizika.

Mhe. Spika, katika jimbo langu la Kiwengwa mpaka hivi sasa wananunua maji dumu shilingi 500. Mhe. Spika, naiomba serikali kwa kushirikiana na sisi viongozi ambao tumechaguliwa, tushirikiane tuweze kumaliza tatizo hili la maji kwa asilimia mia moja.

Mhe. Spika, wanaohangaika sana ni wanawake, wanawake wana majukumu makubwa katika familia, na ndio maana na sisi tukaamua kuja kusimama hapa katika vyombo vya kutoa maamuzi ili na sisi tuweze kuwatetea. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba nizungumzie suala la udhalilishaji wa wanawake na watoto. Suala hili Mhe. Rais katika hotuba yake amezungumzia kwamba ataendeleza kampeni ya kupambana na suala hili ili liweze kuondoka kabisa katika jamii yetu. Ni kweli katika Mkoa wetu wa Kaskazini, kuna Mahakama ambayo alikuja kuweka jiwe la msingi Mhe. Rais hivi juzi tu, mahakama ile itatoa huduma kwa kesi hizi za udhalilishaji wa wanawake na watoto. Naiomba serikali kwa kupitia vyombo husika, kesi hizi zinarundikana sana na zinachelewa kutolewa maamuzi kwa kutumia muda mrefu sana. Kwa hivyo, naiomba serikali kushirikiana na vyombo husika, kesi hizi zinapocheleweshwa basi wanawake ndio wanaopata udhalilishaji zaidi, kwa sababu wao ndio wanaochukua jukumu la kufuatilia kesi hizi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mwisho nimshukuru sana mlezi wangu Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, kwa kuteuliwa kwake kuwa Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Pia nimshukuru kwa kunilea kwa muda wa kipindi cha miaka 15 nikiwa Katibu wake wa Tawi, lakini na hatimaye nikawa Diwani wa Wadi ya Upenja, wakati huo yeye alikuwa Mbunge wa Jimbo la Kitope na hatimaye hivi sasa tukagawana jimbo lile na mimi nikagombea kuwa Mwakilishi wa Jimbo la Kiwengwa. *(Makofi)*

Namuomba Mwenyezi Mungu anijaalie niweze kuwahudumia wananchi wangu wa Jimbo la Kiwengwa na kuitumikia nchi yangu ya Zanzibar katika kipindi chote nitakachokaa madarakani. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nitoe shukrani zangu za dhati kwa Chama cha Wanasheria Wanawake Zanzibar (*ZAFELA*), kwa kunipa mafunzo na kuhakikisha hii leo naweza kusimama mbele ya umati huu kuzungumza na kuweza kuchangia hotuba hii ya Mhe. Rais.

Mhe. Spika, ahsante sana na mimi naungana na wenzangu kuiunga mkono hotuba hii ya Mhe. Rais kwa asilimia mia moja. Ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na mimi niungane na wenzangu kumpongeza Mhe. Rais wetu Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi.

Pia, na wewe Mhe. Spika, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, Naibu Spika, Wenyeviti pamoja na wawakilishi wenzangu wote. Lakini bila ya kuwasahau wananchi wote na hasa wanachama wa Chama cha Mapinduzi wa Jimbo la Mwanakwerekwe. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi nitazungumzia kidogo habari ya utalii na utendaji wa Halmashauri zetu. Mhe. Spika, mimi sio mtaalamu sana wa mambo ya utalii, lakini hapa nimevutiwa na takwimu ambazo ziko kwenye kitabu cha Mhe. Rais. Zimetajwa takwimu za wageni ambao wameingia kwenye nchi yetu. Kuna wageni 132,836 mwaka 2010 na mwisho wake tukawa tuna 311,891.

Mhe. Spika, kama nilivyosema mwanzo sio mzoefu sana wa mambo ya utalii, lakini ningependa muhusika yeyote atakayekuja au waziri atakayekuja wa mambo ya utalii, basi angetuainishia, katika watalii hawa 311,891 ni wepi ambao wamekwenda kwenye hoteli za nyota tano, ni wepi hoteli za nyota nne na ni wepi ambao wamekwenda kwenye hoteli za nyota tatu.

Mhe. Spika, hii itatusaidia kujua ni kiasi gani cha mapato, na mapato pia itabidi tujulishwe na baadae itatusaidia ni wageni wa aina gani kwetu sisi wanatufaa kwa utalii katika nchi yetu. Wasi wasi wangu kwenye fukwe za bahari huko kuna kila aina za hoteli, na wengine mwisho wake vyumba vitatu, na wanawakaribisha watu kuwaweka wageni au watalii tunashindwa. Kwa hivyo, naomba yeyote atakayehusika na haya basi aje kutuchambulia.

Mhe. Spika, jengine tumesema tunakuza utalii, lakini kuna mambo kama hatukuyashughulikia basi yanaweza yakatupa mashaka. Kwa bahati nzuri nina uzoefu wa maeneo ya Kusini, Jambiani, Paje, Bwejuu, Michamvi sio sana. Katika maeneo haya, watu wetu au wananchi wetu wazawa wanashirikiana sana na wageni wa nje kujenga nyumba ambazo baadaye ikifika wakati wa utalii, basi wale wageni wanaleta watalii ama wanaleta wageni, bila taarifa kwa serikali au wizara inayohusika kujua. Kwa maana hiyo serikali haipati mapato yoyote ya watu hawa, lakini huku kuna idadi ya wageni ambao au watalii wameingia kwenye nchi. Habari hizi zinapatikana mwisho kwamba kuna wageni wameingia, badala ya mzawa hunyang'anywa na mgeni. Kwa hivyo, mara nyingi inakuwa hakuna mikataba inayofanywa. Mzawa akishakunyang'anywa ndio hapo tena baadae anakwenda kwenye Afisi za Mkuu wa Wilaya, Afisi ya Mkuu wa Mkoa na hatimaye unakuwa ugomvi, aondoshwe wee aondoshwe.

Mhe. Spika, maoni yangu hasa kwa watu wa utalii, Shirika la Utalii au wizara inayohusika, *ZRB* na Uhamiaji watusaidie katika kuondosha haya ili kukuza utalii wenye tija na wenye maana, kuliko kuwa na wageni ambao hatima yake wanachokifanya hatukijui katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, jengine nitazungumzia kuhusu Halmashauri zetu, lakini kabla ya kuzungumzia basi ningependa kwa ruhusa yako kusoma maneno ya Mhe. Rais yaliyokuwepo kwenye ukurasa wa 19 kuhusiana na utendaji wa wafanyakazi wetu wa Halmashauri zetu. Naomba kunukuu;

> "Kupitia Baraza hili Tukufu, nataka niwahimize viongozi wa manispaa, Mabaraza ya Miji, Halmashauri za Wilaya, Mamlaka ya Mji Mkongwe na taasisi zote zinazoshughulika na usafi wa mji na usimamizi wa biashara, waongeze jitihada katika kuimarisha usafi wa miji na kusimamia sheria na nidhamu ya uendeshaji wa shughuli za biashara. Usafi ni jambo la lazima katika maisha yetu, na hapana mbadala wake. Kwa hivyo, wale wote waliopewa dhamana ya kusimamia usafi katika mji yetu, wajue kwamba wanachukua dhamana kubwa na watawajibishwa endapo watashindwa kutimiza wajibu wao katika ipindi hiki".

Mhe. Spika, mimi natoka Jimbo la Mwanakwerekwe, kwenye soko kubwa sasa hivi kwa mji wetu wa Zanzibar au kwa Unguja. Lakini Mhe. Spika, bila kificho ni sehemu moja chafu kuliko zote za Unguja na Pemba. Uchafu wa Mwanakwerekwe hasa nje umekithiri, pananuka, pachafu, kuna sehemu ya kuegeshea magari mengine yameelekea huku, mengine yameelekea huku, na mule ambapo munahusika kuwekwa gari basi mnauzwa samaki, mnauzwa ndizi na mnauzwa kila aina ya biashara. Sasa imefikia wakati kipindupindu kinacheza rusha roho.

Mhe. Spika, kuna mjumbe mmoja alizungumza hapa, kwamba Wilaya ya Magharibi kipindupindu ndio kimetawala A na B, sio muongo hali ni chafu tena sana. Hapo pana benki ambapo watu tofauti wanakuja, katika maeneo hayo kuna watalii ama wageni wanaokwenda kwenye maeneo ya Kizimkazi, Makunduchi, Jambiani, Paje, Bwejuu na Michamvi wanaondokea pale. Kama nilivyosoma kitabu cha hotuba ya Mhe. Rais, kuna watu wamewekwa kwenye mamlaka za kusimamia kazi hizo, lakini nadhani kikubwa zaidi ni kudhihaki Mamlaka ya Serikali. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Mhe. Said Soud Said, jana alisema; naomba umkabidhi mifunguo mitatu aanze kutumbua majipu mpaka kipatikane kiini akabidhiwe Mhe. Balozi. Maneno yaliyozungumzwa humu ni maneno ya Mhe. Rais, na ndio ambayo toka juzi tunayajadili. Kinachofanyika Mwanakwerekwe nje, ukienda na gari imekaa vibaya, kwa yule mnyonge wanakuwekea mnyororo wanakuchukulia pesa basi.

Mhe. Spika, kwa kupitia Baraza lako Tukufu naomba sana, watu hawa kazi imewashinda. Watafutwe watu ambao wanaweza kufanya kazi kwa kunusuru mji wetu na kunusuru afya yetu. Ingekuwa tuna muda, basi ningekwambia Mhe. Spika, tuchukue timu yako tuelekee Mwanakwerekwe nje ya soko ukaione hali ilivyo ni aibu.

Mwisho kumeandikwa si ruhusa kuuza samaki, basi wamefuta na wameandika ni ruhusa kuuza samaki. Hapo pana wafanyakazi na askari wa Halmashauri, ukienda Halmashauri na nguo zao za manjano wanadai pesa mule. Sasa Halmashauri hii kesho kutwa sheria zikikaa sawa wanatakiwa kuwa manispaa.

Je, kuna manispaa gani duniani ambayo itaendeshwa namna hiyo. Kwa ufupi hali ni mbaya, ninachoomba wanaohusika kuwachukulia nidhamu watu. Basi hiyo kazi ifanyike, na kwa kufuata *guideline* ya Mhe. Rais, vyenginevyo kinachoendelea ni aibu, wale wazungu au wageni wanapiga picha, kwa sababu ukienda sasa hivi wote wameshughulika, na sio wazungu tu hata sisi wenyeji tumeshughulika. Toka jana wanajitahidi nadhani baada ya kusikia habari ya mikasi ya kutumbuatumbua basi wanatoa matangazo, kwamba sijui watu waondoke lakini wako pembeni.

Mhe. Spika, kwa hivyo narudia tena kwa kupitia Baraza hili, kwa yule yeyote ambaye kazi imemshinda tuondoshe ugonjwa ama hii rushwa ya muhali. Vyenginevyo tutamaliza miaka mitano tutakuwa tunakuja hapa hakuna kimoja kinachofanya kazi. Ahsante sana.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe Abdalla Ali Kombo, sasa naomba nimwite Mhe. Omar Seif Abeid. Simuoni Mhe. Omar Seif Abeid, kwa hivyo, nafasi hiyo naomba nimpe Mhe. Hassan Khamis Hafidh, na yeye hayupo. Naomba sasa nimwite. Naam, zungumza Mheshimiwa ...

Mhe. Omar Seif Abeid: Nipo. Omar Seif Abeid.

Mhe. Spika: Aah, *ok.*

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, aliyenijaalia leo mimi hapa kwa mara yangu ya kwanza nikaweza kusimama na kutoa mchango wangu kwenye Baraza hili Tukufu la Wawakilishi.

Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu na kumtakia rehma Mtume wetu Muhammad (*S.A.W*), pia sina budi kutoa pongezi zangu za dhati kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Rais wetu mpendwa Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa ushindi wake mkubwa wa kishindo alioupata wa asilimia 91.4 katika uchaguzi wa marudio. *(Makofi)*

Mhe. Spika, pia sina budi kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe Mhe. Spika, pamoja na viongozi wako wote waandamizi; Naibu Spika, Wenyeviti wa Baraza na wote tuliowachagua kuliongoza Baraza hili.

Ni imani yangu kwamba timu uliyonayo Mhe. Spika, ni timu ya kazi na yenye muelekeo wa mwendo wa kazi. Kwa hivyo, ni matumaini yangu kwamba Baraza lako litakuwa Baraza la aina yake kwa mara hii.

Mhe. Spika, vile vile, sina budi kutoa shukrani zangu za dhati kwa kiongozi wetu wa shughuli za Baraza la Wawakilishi Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, nampongeza kwa uteuzi wake huo na nampongeza Mhe. Rais kwa busara aliyoionesha ya kumuamini Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, akaweza kumrejesha kuwa Makamu wetu wa Pili wa Rais.

Ni imani yangu kwamba uamuzi wa Rais ni wa busara, kwani kiongozi huyu sisi kila mmoja wetu anafahamu mchango wake alioutoa kwenye uchaguzi uliopita wa marudio, na jinsi gani tumeweza kukirejesha Chama cha Mapinduzi kushika hatamu ya dola.

Mhe. Spika, pia sina budi kutoa shukrani zangu za dhati kwa wapiga kura wangu wa Jimbo la Konde, hasa wa Wadi ya Konde, Msuka, Makangale na Kifuni kwa moyo wao walionionesha wa upendo juu yangu mimi na Chama changu cha Mapinduzi kwa kunipa ushindi wa asilimia 89.25. *(Makofi)*

Vile vile, Mhe. Spika nitakuwa ni mwizi wa fadhila ikiwa nitawasahau viongozi wangu wa Chama cha Mapinduzi wa ngazi zote, kuanzia ngazi ya taifa, mkoa, wilaya pamoja na jimbo kwa imani yao waliyonionesha pamoja na ushauri wao wakati wote kwa kuendesha kampeni ambayo imesababisha mimi kupata ushindi pamoja na Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, napenda kutoa shukurani zangu za dhati na dua maalum kwa waasisi wa taifa letu, ambapo jana tuliungana nao pale Afisi Kuu ya CCM Kisiwandui kumuombea dua Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema peponi, muasisi wa taifa letu mzee wetu kipenzi chetu Marehemu Mzee Abeid Amani Karume Mwenyezi Mungu aipumzishe mahala peme peponi amin. *(Makofi)*

Pia, shukurani za pekee ziiendee familia yangu yote, ambao wamenionesha mapenzi makubwa na kuniliwaza wakati wa kampeni. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya shukurani hizo sasa naomba nianze kuchangia hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar kidogo kidogo, ambapo wenzangu wengi wamesema mengi mazuri. Mimi sina haja ya kumaliza ladha ya mambo yaliyozungumzwa kwenye hotuba hii, kwa kweli hotuba hii ni dira, sukani ambayo itatuongoza kufikia malengo ya dira 2020. *(Makofi)*

Kwa hiyo, imani yangu kwamba sisi Wawakilishi tuliochaguliwa na wananchi na viongozi ambao Mhe. Rais wa Zanzibar atawapa dhamana ya uwaziri, tutashirikiana vyema, ili kulisukuma mbele gurudumu la maendeleo, na tutaenda nalo kwa kasi kwa ushirikiano wetu kama Mhe. Rais wetu alivyotuelekeza katika dira yake ya hotuba hii ambayo tuliyonayo na tunaichangia. *(Makofi)*

Mhe. Spika, moja kwa moja nataka nijikite katika suala zima la uwekezaji. Kwa kweli, hatuna budi kumpongeza kwa dhati Mhe. Rais wetu mpendwa kwa hatua na juhudi kubwa alizozifanya katika kuimarisha sekta hii ya uwekezaji. Kwa hiyo, kama ilivyoelezwa katika hotuba ya Mhe. Rais ni kwamba wawekezaji wameonesha imani yao kwa Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuleta mitaji yao kuwekeza katika miji kama alivyoitaja, baadhi ya miradi hiyo ni Mradi wa *Fumba Town Development* uliopo Nyamanzi, Mradi wa *Fumba Satellite City* pamoja na Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Kupumzikia (*Fumba Uptown Living*). *(Makofi)*

Mhe. Spika, imani yangu kwamba miradi hii ina fursa kubwa kwa Wazanzibari hasa vijana, ambapo itatoa ajira nyingi ambazo zitaweza kusaidia kupunguza umasikini na kukuza pato la Taifa.

Mhe. Spika, ninao ushahidi wa kutosha kuhusu miradi hii, kwamba ina nia ya kuendeleza hali ya kukuza uchumi wa visiwa hivi. Kwa mfano, kama Mradi wa *Fumba Town Development*, mradi huu utakapokamilika utakuwa umeshatoa ajira zaidi ya 300 kwa vijana wa Kizanzibari, na hii ni habari nzuri sana kabisa. Kwa hivyo, wito wangu kwa wawekezaji wa nje na ndani kuunga mkono dhamira ya serikali yetu iliopo ya kuwekeza, ili kukuza pato la Taifa la nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu sasa napenda kidogo nizungumzie kuhusu suala la utalii. Mhe. Spika, suala la utalii kama ilivyoelezwa katika hotuba ya Mhe. Rais, jambo hili ni la kutia moyo sana, kwani ni miongoni mwa mambo yanayoingizia taifa kipato. Kwa hiyo, sisi Wawakilishi pamoja na viongozi ambao watapewa dhamana ya kuliongoza taifa hili, ni wajibu wetu kushikamana kwa pamoja kuhakikisha kwamba sekta ya utalii inapiga hatua kubwa kwa ajili ya kuinua pato la Taifa.

Mhe. Spika, kuhusu utalii kwa kweli sina budi kumpongeza tena Mhe. Rais katika sekta hii ya utalii, kwani katika Jimbo langu la Konde nimepata bahati ya kuwa mmoja wa wawakilishi wenye mahoteli katika majimbo yao, pia nimepata bahati ya kuwa na msitu mkubwa wa Ngezi ambao ni tegemezi katika taifa letu, kwa ajili ya kukuza uchumi, kijamii na kimazingira. *(Makofi)*

Vile vile, katika jimbo langu nimebahatika kuwa na ufukwe mkubwa maarufu sana unaoitwa ufukwe wa Vumawimbi, yaani ufukwe huu ni maarufu kwa ajili mapumziko. Watu wote kutoka Pemba akifika siku za Jumamosi na Jumapili utakuta magari yanapita yanaelekea Vumawimbi kupumzika. Kwa kweli, hii ni habari nzuri ambayo wageni wanapokuja wakaiona mandhari ya msitu wa Ngezi na ufukwe wa utalii wa Vumawimbi, basi wageni wengi wanavutika na eneo hilo.

Mhe. Spika, pamoja na hilo kuna changamoto kidogo ambazo zinahitaji kupatiwa ufumbuzi. Kwa hiyo, changamoto ambayo iliopo kwa sasa ambayo ninaiona katika sekta hii ya utalii hasa kwa Jimbo langu la Konde ni kwamba kuna baadhi ya wawekezaji wengi ambao tayari wameshazuia maeneo bila ya kuyaendeleza. Kutokana na hali hiyo, ninaiomba taasisi inayohusika juu ya suala hili la uwekezaji, kwamba wale wawekezaji wote ambao wamepewa maeneo na wameshindwa kuyaendeleza, basi ni vyema kabisa kwa serikali kufuata sheria na kuyafuta na ikawapa wawekezaji wengine, ambao wana nia sahihi ya kuleta maendeleo ya Taifa hili, kuliko kuendelea kuwaachia watu kuyamiliki bila ya kuyaendeleza. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ninazungumza hivi kwa sababu gani, kwa kweli mpaka sasa katika eneo langu kuna jumla ya hoteli tano tu, ambapo eneo hilo lina zaidi ya viwanja 30 vilivyopimwa kwa ajili ya uwekezaji. Hali hii haileti taswira nzuri kwetu sisi na serikali.

Mhe. Spika, kwa hiyo kinachotakiwa kufanywa naomba kutoa ushauri kwa Idara ya Utalii pamoja na Idara ya Uendelezaji Vitenga Uchumi (*ZIPA*) waweze kuwaita hawa watu ambao wana maeneo katika maeneo ya Makangale na ambayo hawayajaendeleza, basi wafuate taratibu wawaite kama sheria inavyosema, na baadaye iwape onyo kama watashindwa kuendeleza, na hatimaye kama watashindwa basi sekta inayohusika iweze kuchukua hatua ya kufuta umiliki wa maeneo hayo na kuwapa watu wengine. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, unazo dakika mbili.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Spika, sasa naomba nizungumzie kuhusu kilimo. Kama nilivyosema kwamba sitaki nizungumze sana, kwa sababu wenzangu wamechangia sana tena ni mambo mazuri, mwalimu wangu, pia Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed amezungumza mengi mazuri. Kwa hiyo, mimi sipendi kuongeza au kuja kuharibu ile ladha ya yale mambo yaliyokwishazungumzwa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kuhusu suala la kilimo sina budi kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein kwa mpango wake madhubuti pamoja na mkakati wake juu ya suala hili la kilimo kwa maana ya kilimo cha chakula na kile cha biashara.

Mhe. Spika, mengi yamezungumzwa kuhusu kilimo na wenzangu walitangulia wamezungumza kuhusu upatikanaji wa pembejeo, uhaba wa mabwana shamba na mimi sina budi kuungana nao juu ya suala hili. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kuna jambo moja ambalo nalipenda naomba nilikumbushe kuhusu suala la kilimo cha mwani. Kwa kweli, kilimo cha mwani ni kilimo ambacho kama kingepangiwa mipango mizuri basi kingeweza kuwanufaisha Wazanzibari wengi. Kwa mfano, katika jimbo langu ninazo sehemu mbili kuu ambapo wananchi wake wanaishi kwa kutegemea kilimo hicho cha mwani, bei ya kilimo cha mwani haina kiwango maalum.

Kwa kweli, kama vile leo unaweza kukuta shilingi 800, kesho 700, na kiasi miezi miwili iliyopita nyuma niliuliza bei ya mwani nikaambiwa ni shilingi 300, kwa kweli ni jambo la kusikitisha kwamba watu wanafanya kazi ngumu kama ile na baadaye tayari wameshategemea kupata kitu, unakuja kusikia mwani unanunuliwa kilo shilingi 300, ni jambo la kusikitisha sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, muda wako umeshamalizika.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Spika, pamoja na mambo yote naunga mkono hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar kwa asilimia mia moja na ahsante sana.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, ahsante sana kwa mchango wako. Waheshimiwa Wajumbe, muda tulionao haumtoshi mchangiaje anayefuata kuweza kuchangia. Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe naomba nitoe maelezo kidogo kwamba wachangiaji tulionao mpaka hivi sasa ambao bado hawajachangia ni wengi kwenye orodha niliyonayo hapa, lakini na muda ambao tutakuwa nao jioni hautatosha kuwakidhi watu wote.

Kutokana na hali hiyo, ninashauri wangetumia hiyo njia ya pili ya kuchangia kwa maandishi baadhi yenu, hapa sasa nitawataja wale ambao watapata nafasi ya kuchangia wakati wa jioni kabla ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar hajaanza kusoma hotuba yake ya kulifunga Baraza.

Waheshimiwa Wajumbe, tutakaporudi jioni mchangiaji wetu wa mwanzo atakuwa Mhe. Ussi Yahya Haji, atafuatiwa na Mhe. Hassan Khamis Hafidh, atafuatiwa na Mhe. Mtumwa Peya Yussuf, na baadaye atafuatiwa na Mhe. Chum Kombo Khamis, na mchangiaji wetu wa mwisho kwa sababu bado hatujawa na serikali naomba nafasi hiyo nimpe Mhe. Mwanasheria Mkuu Said Hassan Said, ili yeye sasa atoe mchango wake kwa niaba ya serikali kabla hatujamruhusu Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kuanza shughuli ya ufungaji wa Baraza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, kwa matangazo hayo, sasa naomba nichukue nafasi hii kusitisha shughuli za Baraza la Wawakilishi mpaka saa 11:00 za jioni ya leo.

(Saa 05:50 asubuhi Baraza liliahirishwa mpaka saa 11:00 jioni)

(Saa 11: 00 Jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Ussi Yahya Haji: Mhe. Spika wa Baraza la Wawakilishi, ndugu Zubeir Ali Maulid, kwanza awali ya yote nimshukuru kwa dhati Mwenyezi Mungu mwenye wingi wa rehema aliyetujaalia kufika hapa leo na kutupa uhai na kuwa tunazungumza.

Pili, nikushukuru kwa dhati kabisa ndugu yangu kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Baraza hili kwa kura nyingi sana za kihistoria. Vile vile, nimshukuru Naibu Spika, naye pia alichaguliwa kwa kura zilizokuwa hazina mfano na wenyeviti wako wakapita bila ya kupingwa, nawashukuru na nawapongeza sana.

Tatu nikishukuru sana Chama changu cha Mapinduzi ambacho ndicho kilichonifanya mpaka nikawa mwakilishi leo, na pia chama hicho ndicho kilichosimama imara bila ya kutetereka na *In shaa Allah* hakitotetereka tukachaguliwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuliokuwepo hapa hamsini na nne (54) na viti maalum ishirini na mbili (22) nakishukuru sana Chama cha Mapinduzi.

Nne niishukuru Tume Huru ya Uchaguzi chini ya Mwenyekiti wake Jecha Salim Jecha nayo ilisimama imara kuangalia kanuni, Sheria, taratibu na Katiba ya Zanzibar mpaka kufikia baada ya kuona madudu yaliyofanywa wakafuta uchaguzi naishukuru sana.

Baada ya kufutwa uchaguzi huo tukaingia kwenye uchaguzi, baada ya kuingia kwenye uchaguzi mgombea wa Chama cha Mapinduzi ndugu Ali Mohamed Shein akashinda kwa kura za historia tangu 1957 mpaka uchaguzi wa

juzi hakuna kiongozi aliyepata asilimia 91.4 ila sisi tumefanya sasa asilimia 91.4 hii tunapaswa sisi Wawakilishi sote kuilinda, kuienzi na kuangalia mustakbali ujao kwa miaka hamsini (50) ijayo, *percentage* hii isishuke. Kwa hivyo nampongeza kwa kupata ushindi wa kishindo. *(Makofi)*

Tano nawapongeza wananchi wangu wote wa Jimbo la Mkwajuni ambao wamesimama imara wakashirikiana na wana-CCM na waliokuwa sio wana-CCM, tuna imani kwamba walikipa kura Chama cha Mapinduzi, hususan wananchi wa sehemu za Matemwe Kusini, Matemwe Kaskazini, Mfurumatonga, Chutama, Gamba na Vita Moga.

Naendelea kupongeza ushindi wa Dkt. Ali Mohamed Shein umahiri wake, ukakamavu wake, ustahamilivu wake na utendaji wake wa kazi wa Ilani ya uchaguzi ya 2010/2015 alivyoitekeleza vizuri na sera za Chama cha Mapinduzi ndio maana akachaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar, na kwa hiyo kutokana na umahiri na utekelezaji wake bila ya kuyumba, bila ya kujali matusi ya mchana na asubuhi magazeti kila siku yalikuwa yanamtusi Seif Ali Iddi lakini Dkt. Ali Mohamed Shein kamuona yeye ndio mtekelezaji wa Ilani ya uchaguzi 2015/2020 kwa hivyo kamteua na yeye nampongeza sana ndugu Seif Ali Iddi.

Mhe. Spika, napata faraja na matumaini ya hotuba hii aliyotoa Mhe. Ali Mohamed Shein akiwa jemadari mkuu wetu, na jemedari huyu ameonesha umahiri wake katika kipindi kizito sana cha kufutwa uchaguzi hakuyumba, hakutetereka, amekuwa kama mithili ya muwanzi, umekuja upepo umekwenda mpaka chini baadae umeinuka kainuka na ushindi na kainuka na moto ule ule wa Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Spika, hotuba hii imesheheni hekima, busara na imelenga sekta zote sina haja ya kuchangia sekta moja baada ya moja, kwani Mwenyezi Mungu akijaalia kwenye bajeti wale watakaopewa dhamana za sekta mbali mbali kuna mengi sana ya kuja kuchangia hasa ukifika wakati huo nitajitahidi kufanya hivyo.

Mhe. Spika, kipindi cha miaka mitano iliyopita kimemalizika sasa tunakwenda kipindi kijacho tunapaswa Wawakilishi tuliomo ndani humu jambo la kwanza ni kushikamana. Hii hotuba ina matumaini ya wananchi wa Zanzibar, matumaini haya yatapatikana kwa kushikamana Wawakilishi wa Chama cha Mapinduzi humu ndani na nje ya ndani.

Mhe. Spika, kila mwakilishi ambaye ana jimbo, mwakilishi mwengine ambaye si jimbo lake aone jimbo lake asibague, na wenzetu hapa zaidi kutoka Pemba nimewafahamu vizuri sana, na ni kweli wenzetu wana matatizo ya majimbo yao Pemba, majimbo yale tuyachukulie sisi tuliokuwa Unguja ni yetu na wao wachukue ya Unguja ni yao *(Makofi)*

Mhe. Spika, kuna taarifa tuna Wawakilishi wa Baraza hili zaidi ya awamu mbili tatu kutoka Kisiwani Pemba lakini hawana habari ya maendeleo ya Pemba, maendeleo yote yamefanywa na Chama cha Mapinduzi wao hawana habari, hata kuitumia ile Ofisi ya Pemba ya Baraza la Wawakilishi hawaitumii.

Sasa nawaasa wenzangu, ndugu zangu, dada zangu, wanangu wao wajali zaidi majimbo yao na watu wao na sisi wa Unguja tutakuwa pamoja nao, tukifanya hivyo na lazima tufanye hivyo, kwanza tutatekeleza hii hotuba ya Mhe. Rais, pili yale matumaini ya wananchi wetu wanayosubiri kwa dhati kabisa yatapatikana.

Kwa hivyo, bado Majimbo ya Pemba pamoja na misaada iliyotolewa ni wajibu wetu Wawakilishi sote, ni wajibu wa Serikali kama inavyofanya kwa barabara, kama inavyofanya kwa maji, kama inavyofanya kwa elimu, waingilie na wasaidie majimbo ya wenzetu wa Pemba kadiri inavyowezekana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naendelea kwa kumalizia kwa kumuhakikishia Mhe. Rais, aliyetoa hotuba hii tunamuunga mkono kwa dhati kabisa, na asiwe na hofu Baraza hili liko pamoja naye. Muhimili huu uko pamoja naye na yeye tuna hakika yuko pamoja na Baraza hili. Nasaha zetu tutakazozitoa, michango yetu tutakayoitoa aingalie kwa dhati kabisa, na tuna hakika tutashirikiana kwa kulinda Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2015/2020.

Mwisho kabisa, namshukuru kwa dhati Mhe. Rais busara aliyoitumia kuteua Wawakilishi ndani ya chama chetu na kuteua nje ya chama chetu ni busara kubwa sana, tena sana, na busara hii aiendeleze kwa miaka yake yote mitano na Wawakilishi hawa waliokuwa nje ya Chama chetu matumaini yangu kwa sababu mmoja ni rafiki yangu sana tulikuwa pamoja benki pale tumezungumza sana Ndugu Hamad Rashid, nina hakika atakisaidia Chama cha Mapinduzi na kupata ushindi.

Ndugu Hamad Rashid tusimshangae kuja CCM, *ng'ombe akiumia mbugani anakimbilia zizini*, zizini kwa Hamad Rashid ni CCM wala asikudanganye mtu, huko alikuwa anahangaika tu lakini amefika kwao tumempokea nimeona dalili ya kofi hapa pamoja na mwenzake ndugu Said Soud na ndugu yangu Juma Ali, kwa hivyo, tumekupokeeni na wenzetu huko wanayoyasema sisi tusijali, na hatujali kwa sababu wanayasema mengi wao wanashangilia kwamba sisi tutakula ukoka kwa sababu tutanyimwa misaada, hawana habari hayo wameshayafanya miaka iliyopita na hatukula ukoka tuko hapa hapa, washayafanya haya washakwenda duniani huko tusipewe misaada na leo hii zile nchi ambazo zilisema zinanyima misaada zimekanusha zimesema sisi hatujasema hivyo. *(Makofi)*

Kwa hivyo, ndugu zanguni tusiwe na wasi wasi, Serikali hii itakwenda kwa miaka mitano, uchaguzi mpaka 2020, na sisi tushikamaneni twende kazini.

La mwisho kabisa ndugu zangu Wawakilishi wa vyama vyengine na CCM tujitahidini kulinda Muungano, bila ya Muungano hatupo hapa, kama hakuna Muungano hakuna Baraza la Wawakilishi, watavunja tu wale Muungano, chama chochote ambacho kitakamata Serikali Zanzibar si CCM, basi Muungano hakuna, na kama hakuna Muungano hatuna Baraza la Wawakilishi, pengine tutaitwa *Majlis tashrii*, kabla ya Mapinduzi kulikuwa na *Majlis tashrii*, Baraza la kutunga sheria la mabwana wakubwa huko, na lugha yake ilikuwa inataka itumike Kiarabu, si Kiswahili, na walikuwa wanafanya mafunzo watu wa Redio Zanzibar nilikariri mafunzo madogo Redio Zanzibar, *"tantahi baramijana ala mawjatayn twuulal- uula ala khamsu miat mitrat"*. Walikuwa wanafunzwa hayo ili kuondoa kabisa kabisa utawala wa mtu mweusi, tukazaneni. Muungano wa Serikali mbili ndio suluhisho letu na ndio suluhisho la watoto wetu hawa wengine wadogo wameanza kuja kwenye Baraza la Wawakilishi, tuwapeni taaluma na misingi ya chama chetu. *(Makofi)*

Kwa hayo machache sana kwa leo naomba nisite hapo, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia hotuba hii mahususi aliyokuja nayo juzi Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Spika, kwanza naomba nianze na shukurani kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uhai, uzima afya na mimi Hassan Khamis Hafidh kuwa miongoni mwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi la Tisa la Zanzibar. Baraza ambalo la aina yake la peke yake, lina lengo mahususi na kushirikiana pande zote baina ya Serikali na wananchi katika kuiletea Zanzibar maendeleo.

Kadhalika naomba nichukue fursa hii kuwashukuru familia yangu wake zangu, ndugu zangu, kaka zangu kwa kunistahamilia katika kipindi kigumu cha kampeni. Wagombea tisa na Hassan Khamis Hafidh kutokea mshindi katika jimbo la Welezo, tangu kura za maoni mpaka kura za uchaguzi mkuu; chaguzi zote mbili.

Kadhalika naomba niishukuru CCM Chama cha Mapinduzi kuanzia Ofisi Kuu, Mkoa, hadi Wilaya. Kadhalika walionilea Ikulu kuanzia Mhe. Rais, Katibu Mkuu Kiongozi, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Ikulu, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi yangu ya *Diaspora* na watendaji wenzangu wote wa Ikulu naomba niwashukuru.

Kadhalika naomba niwashukuru jamaa zangu wa Mchangani na Dunga walioniombea dua na kuniambia utakuwa Mwakilishi wa Jimbo la Welezo na utakuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi la Tisa, pamoja na ndugu, jamaa na marafiki wote wamechangia Mhe. Spika, naomba niwashukuru.

Naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kipindi chake cha pili, kipindi ambacho sote tunaamini kwamba hichi ndicho kipindi kitakacholeta jawabu la Mapinduzi matukufu ya 1964, maana yake Mapinduzi ya Zanzibar 1964 hakuna maana nyengine bali maana yake ni maendeleo kwa wanyonge, wakwezi na wakulima wa Zanzibar.

Aidha, naomba nimpongeze Mhe. Rais na watendaji wake; kuna Katibu Mkuu wa Rais, Katibu Haroub, Naibu Katibu Mkuu wa Rais Maryam, Afisi ya faragha yote napenda niipongeze hawa wote ni watendaji wenzangu napenda niwapongeze sana.

Sasa napenda nichukue fursa hii adhimu kumpongeza Mhe .Rais juzi alipokuja alikuja kwa kujiamini, kwa mbwembwe alikuja na kitabu hichi, lakini yeye alikuja na karatasi za kijani zimeandikwa hotuba ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein katika uzinduzi wa Baraza la tisa la Wawakilishi la Zanzibar.

Hotuba hii ukiichukua ukiisoma ina mambo matatu makubwa. Jambo la kwanza hotuba hii Mhe. Rais amesema wazi wazi kwamba imekuja kuomba ushirikiano, ukifungua ukurasa unasema kazi tuliyonayo mbele yetu, hakusema Mhe. Rais kazi aliyonayo mbele yake, maana yake nini, maana yake Mhe. Rais kaja kutuomba ushirikiano. Mahatma Gandhi amesema *"United we stand divided we fall",* Obama amesema *together we can, sure we can!*

Mhe. Rais kutaka kuipeleka mbele nchi hii muarubaini wake ni mashirikiano tu, *nothing else,* kitabu hichi Mhe. Rais alichokuja nacho ukifungua ukurasa wa tano maneno ya mwisho, Mhe. Spika, pana pahali panasema umoja wetu na mshikamano wetu *these are golden chances.* Ukienda mbele inasema bila ya kujali ubaguzi wa aina yoyote, ukurasa wa tano huo halafu mwisho kabisa kinasema kasi ya maendeleo nchini.

Mhe. Spika, tunahitaji nini, hotuba ya Rais ya juzi imemaliza kila kitu. Lakini Mhe. Spika mimi kama Hassan nilipata bahati ya kuishi nje kidogo, lakini nilipokuja Zanzibar nikafanya kazi Ofisi ya Rais katika kusikia yangu kila siku tunasikia ooh, ooh, malawama tu Zanzibar. Basi nasema Mhe. Rais kaja na kitabu kizuri, kina maelekezo yote, kina mambo yote lakini nimepatwa na wasi wasi, kweli Wazanzibari sisi tutaweza kuyatimiza haya! Kwa sababu ya mambo tuliyonayo.

Naomba niyataje baadhi ya mambo tuliyonayo mabaya na lazima sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuweze kujihakiki na tuhakikishe tunaweza kuwatimizia wananchi kile wanachokitegemea, kama si hivyo sote ni mashahidi na sote tutabeba dhima. Naomba niyataje baadhi yao.

Mhe. Spika, tukitaka tusitake baadhi ya mambo sisi tuliyonayo kwanza ni wabinafsi. Pili tuna muhali maana ya neno hili muhali sijui maana yake nini, sijalipatia jawabu bado mpaka leo natafuta kila *dictionary*, hatupendi kufanya kazi. Halafu kingine kibaya zaidi hatujali na mwisho kabisa miongoni mwa *research* zangu Mhe. Spika sisi baadhi yatu ni wanafiki. Kwa hivyo, ninaomba Mhe. Rais amekuja na kitabu kizuri chenye maneno ya dhahabu, amekuja kutwambia kazi iliyokuwepo mbele yetu tushirikiane nae.

Mhe. Spika, nchi yetu ni Zanzibar, Zanzibar ni miongoni mwa nchi masikini duniani, lakini je, kweli sisi ni masikini. Nanukuu maneno ya Nelson Mandela 1996 pale *London Trafalgar Square* Mandela aliitwa kuwa mgeni rasmi wa *to make a poverty history*, katika *speech* ya Mandela alisema: *"Poverty is a manmade"* Mungu kumbe hakutuumbia sisi umasikini. Sisi wenyewe ndio tunaoleta umasikini, sisi wenyewe ndio tunaouweka umasikini, kwa nini tunauweka umasikini? Kwa sababu ya zile sababu sita nilizozitaja, wengi wetu ni wabinafsi, wengi wetu ni wanafiki, wengi wetu hatujali kazi lakini sasa mheshimiwa kule alisema mwarubaini wa safari hii madamu Mhe. Rais kaja mimi shahidi nimemuona na nimemshuhudia kaja kusema kwenye ukurasa wa sita, hakusema kazi iliyo mbele yake, amesema kazi iliyo mbele yetu, maana yake tushirikiane nae.

Mhe. Spika, mimi nashangaa sana, hotuba hii ninachoshangaa ni kwamba Mhe. Rais karibu ataunda serikali, na atakapounda serikali ataunda na watendaji lakini chakushangaza kwamba kule Ikulu tulikuwa tuna msemo tunasema

mpaka hili pia ndio mpaka aende Rais. Maana yake hapa Zanzibar Mhe. Rais kasema hataki kuwaona ng'ombe kila siku wanataka kutuua huko mitaani, bado ng'ombe wamo hivyo tena mnataka Rais aseme nini! Nitakupeni *story* moja ya Kiingereza.

Aliyekuwa Mfalme wa Uingereza kabla ya *Queen*, vita vile vya dunia alimwita Winston Churchill, alipomwita Winston Churchill akamwambia Churchill unawaona Wajerumani wanavyotusumbua hao, akamwambia; *Yes, I can see them, So, Can't you? Yes, I can*, akamwambia umewaona tutawafanyaje wanapitia angani, akamwambia; *Sir, your wish is my command*, akarudi nyuma akasaluti, *what can I do?* Wamepitia juu nitapita chini. Baada ya wiki mbili tulichoshuhudia ni kimoja, Mjerumani alikiona kilichomfanya kuku asikojoe na maji anakunywa. Mpaka leo historia duniani, Mjerumani aliisha. Kinachonishangaza hapa Rais anatoa *order* nani wa kufatwa nchi hii kama si Rais, kwenye *Qur-an* ametwaja. Basi baadhi ya watu pia hawajali lakini nawaambia Baraza la Tisa ndio *solution* tumeingia vijana, wana mapinduzi tutahakikisha maana yake mimi nashangaa wanasubiri Rais atumbue jipu. Hivyo kama sisi si watumbuaji majipu, yuko mwengine, hakuna. Sisi ndio watumbuaji majipu tena naomba sana nisimsikie mheshimiwa kusema majipu yatumbuliwe, majipu tutumbue.

Mhe. Spika, wakati umefika sasa wa Zanzibar kuwa baada ya pepo iwe Zanzibar. Kuna mwandishi mmoja anasema *Zanzibar is motherland of East Africa, Paradise of Africa, yes, it is!* Lakini tukishikamana kama alivyosema Rais, tukifanya kazi kwa pamoja Baraza la Wawakilishi na kila mwananchi Mhe. Rais kasema ukurasa wa sita kazi iliyo mbele yetu, sio kazi iliyo mbele yake ni iliyo mbele yetu, tushirikiane.

Mhe. Spika, kwenye hotuba ya Rais unaweza ukatafuta japo kosa la kidoto *and you can't find it*, huoni imeanza na uchumi. Hivyo nani asiyejua kama Zanzibar sisi sio masikini. Bilioni mia tatu sitini na ngapi nafikiri kama sikosei tunapata kwa mwaka, *wallahi* Mhe. Spika tusidanganyane kama tutaweza kuyadhibiti mapato, tutaacha muhali, tutaacha kila kitu basi mapato yatazidi mara mbili. *TRA, ZRB* bado mapato yanavuja, hakuna asiyejua.

Mhe. Spika, Uingereza ukiwa hujalipa mapato anayekushitaki ni *Queen* inakuja hasa Hassan *vis-a-vis Queen* basi utaona kilichomfanya kuku asikojoe. Lakini hapa nimeomba kujua juzi niko pale nimewapelekea barua *Revenue Board* kujua watu wangapi wamekuwa *convicted* kwa kutokulipa mapato, au wangapi wamefungwa huwezi kupata hizo data kwa sababu *we are not serious and our roles to make those people serious and this is the time, this is the moment to make sure*, kila mtu nchi hii sasa anafanya kazi, anawajibika, tunashirikiana kwa maslahi ya wananchi na maendeleo ya Zanzibar, ubinafsi ufe sasa ni kazi tu. Tuache kabisa kufanya kazi kwa mazoea, tubadilike, tufanye kazi kumsaidia Rais.

Mhe. Spika, pia, hotuba imetaja viwanda; mimi tangu napata fahamu yangu naishi Amani kuna viwanda vidogo vidogo, lakini leo vimekufa ni wazi tukiweka viwanda Mhe. Spika nchi hii lazima vijana watapata ajira, wenye majukumu yao wasilale wafanye *research* wahakikishe wanawaleta watu hapa.

Mhe. Spika, lakini kingine cha kushangaza nchi hii Mhe. Rais anaunda serikali anachagua Wakurugenzi basi *wallahi* nchi hii jinsi ya watu walivyokuwa hawajali na hawaogopi na hawataki kufanya kazi, eti Mkurugenzi Mhe. Spika anaingia kazini saa mbili na nusu, akifika kazini saa mbili na nusu anatizama kwenye *come in* ma-*file* anaandika maneno matatu yanaitwa kwa hatua zako, ikifika saa tatu ameshamaliza anaanza kucheza *game, can the directors play game in the computer, the game*! katika nchi ya mapinduzi kama Zanzibar. Hivyo ndivyo baadhi ya watendaji wetu Zanzibar walivyo, lakini mwarubaini wao ni BLW la Tisa na sanda yao ni Katiba na ubao wao ni sheria, Mwanasheria Mkuu yupo lazima tuwaondoshe.

Mhe. Rais pia ametaja mifugo katika hotuba yake, imetaja uvuvi aibu kabisa Mhe. Spika nchi imezungukwa na bahari lakini tunakula *Perdue fish* lazima tufanye kazi.

Mhe. Spika, kingine kabla hujaniambia kitu ni kuhusu kilimo, tunahitaji mchele tani 82,000 kwa mwaka, sisi tunaweza kuzalisha tani 15,000 tu. Mhe. Spika, mabonde Zanzibar hapa Unguja tunayo 25, Pemba tunayo 18 hata robo yake hatufiki pesa chungunzima zinapelekwa…

Mhe. Spika: Una dakika mbili Mheshimiwa, endelea.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Spika, ahsante naendelea kidogo kuhusu mazingira ni kwamba nchi hii watu hawajali, mtu anakata tu miti, kwa sababu yote hayo Mhe. Spika ni ajira hakuna.

Mhe. Spika, jambo la mwisho uone hotuba hii kwamba ime-*contain* kila kitu, kuna watu wanaitwa *Diaspora*. *Diaspora* ni wale watu wanaoishi nje ya nchi lakini ujue Mhe. Rais jinsi gani wanavyotaka kuiletea maendeleo Zanzibar basi kwenye hotuba hii amewaweka, na watu hao ndio juzi tumewaona wameandamana kula Ulaya waliko. Lakini ujue Rais wa maendeleo Dkt. Ali Mohammed Shein pia amewaweka na amewaahidi kwenye hotuba hii Agosti atawafanyia kongamano. Nini tunajifunza, ni kwamba Rais huyu anataka kuiona Zanzibar iwe baada ya pepo iwe Zanzibar, iwe *Paradise of Africa,* iwe *motherland of East Africa.*

Mhe. Spika, kuna kitu kimoja kinaniuma sana katika nchi hii kinaitwa maji, kwenye majimbo yetu hasa ya Welezo na kwengine kinaniuma, naomba nimalizie kukisema. Maji kweli ni kidogo, maji kweli hatuna lakini kuna watendaji wamo katika taasisi ya maji mheshimiwa wanafanya kazi kutokana itikadi za kisiasa. Jimboni kwangu mheshimiwa nimemkuta mtu kayafunga maji kwa makusudi, basi nililomwambia kwamba *wallahi* Iran kitu kama hiki unakufa lakini bahati yako uko Zanzibar.

Mhe. Spika, pia ardhi nchi hii imekuwa *soft touch,* kuna migogoro ya ardhi. Mhe. Spika, kwa kumalizia naomba kusema Mhe. Rais juzi alikuja na hotuba hii, hotuba iliyojaa kila kitu, alikuja kutaka ushirikiano na Wazanzibari, kutaka ushirikiano na *Members* wa Baraza la Wawakilishi tushirikiane tusimfiche mtu, tusioneane haya kwa maslahi ya Zanzibar, kwa maendeleo ya Wazanzibari, kwa Muungano wetu, kwa umoja wetu.

Narudia kwa kumalizia kusema maneno ya Rais Obama wa Marekani "*together we can, definitely"* tukishirikiana tutafika, mtu umepewa kazi ya uwaziri usimngoje Rais kuja kutumbua jipu, anza wewe. Mhe. Spika, nitoe mfano kama mtu ni waziri, katibu mkuu hafai ukienda kwa Rais ukipiga timamu ukimwambia Mhe. Rais Katibu Mkuu wangu hafai bila ya kuwa na lolote katika kifua chako, kwa sababu hafai ana moja, mbili, tatu, nne naomba umtoe, kuna tatizo…

Mhe. Spika: Mheshimiwa Hassan Khamis…

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Baada ya hayo machache mheshimiwa mimi naitwa Hassan Khamis Hafidh, mwakilishi wa kudumu wa Welezo naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

Mhe. Mtumwa Peya Yussuf: Mhe. Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia tukiwa wazima wa afya jioni hii. Lakini pia Mhe. Spika, sina budi kuwashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Bumbwini kwa kuweza kunipigia kura nyingi nikaweza kushinda na nikawa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi. Aidha, naishukuru sana familia yangu, nawashukuru sana wanangu kwa kunipa mashirikiano mpaka nikaweza kufanikisha suala hili nikaweza kuwa mshindi na mimi nikawa mwakilishi wa Jimbo la Bumbwini. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nampongeza sana Mhe. Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuweza kurudi tena kuwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Na pia nampongeza Mhe. Rais kwa kumchagua Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kuwa Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika, nakupongeza na wewe kwa dhati kabisa kwa kuweza kuchaguliwa kwa kura nyingi, kuweza kuliongoza Baraza hili. Pia nampongeza sana Mhe. Naibu Spika, kwa kupata kura nyingi kuweza kuwa Naibu ukizingatia ni mwanamke na wanawake tumo wengi ndani ya Baraza la Wawakilishi, nampongeza sana.

Mhe. Spika, na mimi naomba kuchangia kwa ufupi hotuba hii ya Mhe. Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, hotuba hii ya Mhe. Rais kwa kweli imebeba kila kitu na sisi wawakilishi tuliomo humu ndani tunatakiwa tumuunge mkono Mhe. Rais kuyatekeleza yale yote yaliyomo humu ndani ya hotuba yake hii. Mimi nitachangia kwa ufupi, nakuja kwenye suala moja la afya.

Mhe. Spika, Mhe. Rais kazungumzia suala la afya kwamba kuziboresha huduma za afya hususan hospitali zetu za rufaa. Lakini sisi tunatoka ndani ya majimbo na ndani ya majimbo yetu kuna vituo vya afya, vituo vya afya hivi kwa kweli vimejengwa kila eneo lakini ukiangalia hivi vituo vya afya tulivyonavyo havikidhi haja kwa sababu vina

mapungufu. Mimi ndani ya jimbo langu nina vituo vya afya vitatu, ndani ya vituo vya afya hivi kituo cha afya kimoja kinatakiwa kifanye kazi masaa 24, kwa sababu kina mama kituo hicho ndicho ambacho wanapata huduma zao za uzazi. Lakini kuna tatizo ukiangalia kwamba madaktari waliopo pale hawatoshi. Unakuta kituo kile kinafanya kazi asubuhi tu mpaka saa 10, ikifika hapo kituo kile kinafungwa, kwa kweli kina mama wetu wanapata matatizo makubwa.

Mhe. Spika, mama akipata tatizo kuanzia saa 12 jioni anashindwa kwenda kwenye kituo cha afya kujifungua hatimae kina mama wanajifungulia nyumbani, wanapoteza uhai wao pamoja na watoto. Aidha, mama yule afate kituo cha afya ambako ni mbali sana hivyo mama yule anapata matatizo makubwa, inawezekana anaweza akapata salama inawezekana akapoteza uhai wake. Kwa hivyo, naiomba serikali tukishirikiana na wawakilishi tulisimamie kwa kina suala hili, tuweze kupata madaktari wa kutosha ili kuweza kukidhi haja na hawa kina mama wapate huduma inayostahiki.

Mhe. Spika, nakuja kwenye suala la vijana kama tunavyotambua kwamba vijana ni rasilimali ya taifa, lakini vijana hawa hawa ndio wenye matatizo mengi kuliko kitu chochote. Vijana wanazururа, vijana hawana ajira inawapelekea vijana hawa wanakosa mwelekeo, wanajiunga na vijiwe ambavyo havina faida na wao. Chakufanya Mhe. Spika sisi wawakilishi tuliomo humu ndani tuhakikishe kwanza vijana wetu tunawafikia popote pale walipo.

Mhe. Rais, amelizungumza suala la vijana kwamba vijana hawa watapatiwa mitaji na pia watapatiwa elimu kwa ajili ya kujiendeleza ili waweze kujikwamua kiuchumi. Hili suala nawaomba wenzangu wawakilishi lisiwe linazungumzwa ndani ya vitabu, hili suala tulisimamie kwa sababu vijana tunawategemea. Mimi kwenye jimbo langu nina vijana karibu asilimia 75 na vijana hao wote wanatuhitaji sisi kwa sababu ndio viongozi wao ili tuweze kuwaongoza, tuweze kuwatatulia matatizo yao na waweze kupata maslahi yao.

Mhe. Spika, ukiangalia jimbo langu mimi vijana wengi shughuli zao ni uvuvi lakini uvuvi huo wanakwenda hawapati tija yoyote kwa sababu mtu anachonga kingarawa chake anakwenda mtu mmoja au wawili anarudi pale, kwa kweli haikidhi haja. Kwa hivyo, ninachoomba vijana hawa wasimamiwe kwa kina sio kukopeshwa fedha tu hata kukopeshwa vifaa vya uvuvi wakaweza kwenda kuvua uvuvi wa mbali na wakaweza kujiendeleza kiuchumi. Endapo tutashirikiana, tutalifanya hilo basi vijana wetu watajikwamua kiuchumi. Tatizo la ajira litapungua na kusema vijana watukutu litaondoka kwa sababu vijana watatuelewa.

Mhe. Spika, nakuja na suala la wanawake, namshukuru sana Mhe. Rais kwa kuwaona wanawake nakuweza kuanzishwa hivi vikundi vya ujasiriamali kwa kupatiwa mafunzo na kupewa hii mikopo. Ninachokiomba mikopo hii itakapotolewa iende kwa walengwa waliokusudiwa, sio kunatoka mikopo lakini wale walengwa hasa waliokusudiwa inakuwa haiwafikii. Hivyo, naomba tulisimamie kwa kina, tuhakikishe kina mama wetu wanapatiwa mikopo, wanapewa elimu waweze kuendeleza vikundi vyao. Kwa sababu kama utampa mkopo bila ya kumpa elimu bado hujamsaidia, lakini ukimuwezesha mama mmoja ukimpa elimu akipata na mtaji wa kutosha mama huyu ataweza kukidhi mahitaji yake yeye mwenyewe, lakini pia ataweza kuendeleza familia yake.

Mhe. Spika, nawashukuru sana na niwaahidi wananchi wangu wa Jimbo la Bumbwini walioweza kunichagua kwamba ahadi zote nilizozitoa ndani ya kampeni basi ninaahidi nitazitekeleza. Na niko tayari kufanya nao kazi bega kwa bega, namuomba Mwenyezi Mungu anisaidie na aniwezeshe kuwatumikia wananchi wangu wa Jimbo la Bumbwini.

Waheshimiwa Wajumbe, wenzangu tumeomba kazi na tumepata kazi, kwa hivyo ninachowaomba tusione kazi kufanya kazi, turudi majimboni mwetu tukafanye kazi. Mwisho kabisa naiunga mkono hotuba hii ya Mhe. Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar asilimia mia kwa mia. Ahsante sana.

Mhe. Chum Kombo Khamis: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii adhimu na mimi kuchangia hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Lakini kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai wake na kutufikisha hapa katika Baraza hili tukufu tukiwa katika hali ya uzima na afya njema jioni hii ya leo.

Pia, nikushukuru wewe Mhe. Spika na uongozi wako wote ambao umechaguliwa kwa kura nyingi, nakutakieni kila la kheri kwa kuliongoza Baraza letu hili tukufu. Vile vile nimpongeze Mhe. Rais kwa uteuzi wake wa kiongozi wetu wa shughuli za serikali katika Baraza hili, nampongeza sana.

Mhe. Spika, sina budi kuishukuru familia yangu kwa kuni-*support* na kuniwezesha kufika hapa nilipofikia akiwemo mume wangu mpenzi, namshukuru sana. Vile vile, nimshukuru Maalim Seif Sharif Hamad kwa kutupigia kampeni na kuchukua majimbo yote kisiwani Pemba. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad aendelee na kampeni zake hizi hizi tuendelee kuchukua haya majimbo kisiwani Pemba. *(Makofi)*

Mhe. Spika, niendelee kwa kusema kwamba, napongeza hotuba hii ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Hotuba hii imejaa mashiko na hekima ndani yake, kazunguka, kapita nyanja tofauti katika hotuba hii na kuwa na nia safi ya kuitekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Spika, mimi nitajikita zaidi katika sehemu ya wanawake. Nimpongeze Mhe. Rais kuona kwamba wanawake ndio chachu ya maendeleo na hii naamini kwamba Mhe. Rais ana upendo mkubwa sana kwa akinamama. Kazi iliyopo mbele yetu sisi Wajumbe wa Baraza hili tukufu na wananchi wa Zanzibar ni kum-*support* Mhe. Rais kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Lakini nataka kusema kwamba masuala ya wanawake pia nawalenga na kinababa. Akina baba tuna kazi kubwa ya kum-*support* Mhe. Rais suala la akinamama kwani mwanamama bila mwanamme maendeleo hayawezi kukaa sawa, ingawaje tunasema kuwa wanawake tunaweza bila ya kuwezeshwa na hili ni sahihi, lakini nasema hivi kwa maana sisi wanawake tunaweza bila kuwezeshwa.

Kwa mfano, baba mchana kutwa anakuwa hayupo lakini mama unamuacha ndani na ulezi wakati mwengine wanaume wengine wanatoka nyumbani hawamuulizi mama nini kitapikwa chai au pengine na mchana chakula cha watoto hawaulizi, lakini anapokuja anawakuta watoto wako salama wamekula, wamekoga, wamevaa. Kwa hiyo, nasema kwamba wanawake tunaweza bila ya kuwezeshwa.

Vile vile, niseme akinababa tumsaidie Mhe. Rais hii kazi kutokana na kuwapa mzigo mkubwa kinamama wa ulezi. Kwa sababu inaonekana kuna baadhi ya wanaume hawataki kuwajibika na familia na hatima yake wanawapa kinamama mzigo mzito kiasi ambacho wanashindwa hata kushiriki katika shughuli za maendeleo. Kwa mfano ni juzi tu, tumetoka katika Uchaguzi Mkuu wa Zanzibar. *(Makofi)*

Kisiwani Pemba sijui kwa huku kwenu lakini sisi kisiwani Pemba wapo akinamama walioachwa kwa sababu eti wamekwenda kupiga kura na wanawake hawa ukimfuatilia utakuta kaachwa ana watoto tisa. Hivi kweli huyu baba anatarajia nini mbele yake mwanamama aliyefanya maendeleo wakati keshaitelekeza familia?

Mhe. Spika, vile vile, niombe kwamba tumsaidie Mhe. Rais kutekeleza ilani ya Chama kwa kupitia Baraza hili tukufu, tuzipitie upya sheria zetu kwa kutunga sheria madhubuti tuone kwamba sheria hizi zinafanya kazi vizuri kwa kuwasaidia kinamama na watoto. Watoto wetu wanadhalilika, watoto wanadhalilishwa na wanaowadhalilisha ni kinababa.

Mhe. Spika, bahati nzuri mimi natokea katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Micheweni haichukui wiki moja tunapokea zaidi ya kesi 20 mpaka 30. Kesi hizi zote zinakuja kuwa ni matatizo ya kinababa wanaowafanyia kinamama wanawapiga, haji mwanamme kushtaki kama kapigwa kesi nyingi zinazokuja wanawake ndio wamepigwa na wanaume. Wamewatelekeza na watoto, mwanamme hapiti. Kwa hiyo, niliombe Baraza hili tukufu tuzipitie sheria zetu na hasa zinazohusu watoto ili tuwajenge watoto wetu waweze kupata elimu ya kutosha.

Mhe. Spika, pia nichangie sehemu ya uimarishaji wa bandari. Mhe. Rais sehemu hii tunamshukuru *Alhamdulillah*, hii miundombinu kachangia vizuri sana na katekeleza kiasi ambacho tunamshukuru na kumpa pongezi aendelee kuitekeleza ilani ya CCM.

Mhe. Spika, Mhe. Rais, najua kwamba anawapenda wananchi wake na hataki kuona wanapata tabu na ndio maana akasema atafanya uimarishaji wa bandari. Kwa upande wa miundombinu Mhe. Rais amejitahidi ambapo sasa hivi kisiwani Pemba ni sisi wenyewe tu lakini mpaka saa mbili za usiku ndege zinaendelea kutua pale uwanjani, zinafanya kazi na tumefarijika wananchi wa Pemba. Hili pia nimpongeze Mhe. Rais.

Mhe. Spika, sehemu ya bandari kuna matatizo madogo madogo ambayo tunahitaji kuyafanyia marekebisho. Niwaombe mawaziri Mwenyezi Mungu atakaowajaalia wakipata uteuzi basi tuhakikishe kwamba tunamsaidia Mhe. Rais kwa hili. Kwa sababu pale bandarini pana matatizo madogo madogo au changaomoto ndogo ndogo. Kwa mfano, abiria wetu wanaposafiri ama kutoka Pemba au kutoka Dar-es-Salaam wanapokuja pale panakuwa na usumbufu kidogo, panakuwa na msongamano baada ya kuteremka badala ya kuwa abiria waende nyumbani kupumzika hatima yake wanakuwepo pale mizigo yao kwa kupekuliwa kwa njia ya mikono. Hii Mheshimiwa ni changamoto, tunaomba mawaziri watakaochaguliwa kupitia serikali hii basi kitafutwe kifaa ambacho kinafaa cha usalama zaidi au kutafuta usalama wetu wa nchi na wananchi wetu pia ili isaidie kuondosha ule usumbufu kwa abiria hawa na wananchi kwa jumla.

Vile vile, naomba kwamba kifaa hiki kitakapopatikana itakuwa ni vizuri kwa usalama kwa sababu mimi nahisi ule upekuzi unaofanyika kwa njia ya kufungua mabegi na kutiwa mkono basi ikiwa mfano mtu kaficha silaha au kuna baadhi ya vitu vyengine kama kaficha huwezi ukaligundua kirahisi, kwa sababu ukifika unatia mkono huku na huku katikati hujui kilichowekwa. Kwa hiyo, hili naliomba Mhe. Spika, lifanyiwe kazi kupitia Baraza hili tukufu.

Mhe. Spika, niendelee kuchangia kuhusu mazingira. Kila mwananchi ana haki ya kutambua umuhimu wa mazingira katika nchi hii, lakini mimi niwapongeze wananchi wetu wameitikia wito huu kiasi fulani kwa kuimarisha mazingira yetu ya Zanzibar kwa kuitikia wito wa upandaji wa miti ya mikoko, mivinje na kadhalika. Kwa hiyo, kuhusu hili naomba tuendeleze na sisi kutunza mazingira kupitia Baraza hili au na wale ambao watachaguliwa kupewa hizi wizara zinazohusika na mazingira. Kwa sababu ardhi yetu ni ndogo sasa hivi maeneo ya kilimo yamekuwa madogo hususan Wilaya ya Micheweni. Kule wananchi wetu wanatoka Micheweni na kulima maeneo mengine ambayo ni masafa marefu na wanapata tabu sana. Kwa hiyo, naomba wanapokuja wakandarasi tunajua kwamba unapotaka kujenga lazima patakuwa na uharibifu.

Kwa hivyo, kuhusu hili pale wakandarasi wanapokuja wa kutengeneza barabara basi tuwaekee mikataba kwamba wakishamaliza kazi zao yale mashimo wafukie, wasiyaache wazi, mashimo yale ikiwa sehemu ile ya ardhi watairejesha uhalisia wake wananchi wataweza kuendelea kupanda vilimo vyao angalau kuwasaidia japo miti wanaweza wakapanda. Hivyo basi, kupitia Baraza hili na taasisi husika lisimamiwe wanapokuja hawa wakandarasi basi tuwape mikataba wasifanye ile kazi baadae kuondoka na kutuachia uharibifu wa mazingira.

Mhe. Spika, pia naomba nichangie...

Mhe. Spika: Mheshimiwa, una dakika mbili.

Mhe. Chum Kombo Khamis: Mhe. Spika, bado naomba niendelee suala la mazingira. Suala la mazingira limekuwa ni kikwazo katika jamii zetu za Kizanzibari, inaonekana utunzaji wa mazingira pamoja na kwamba nilipongeza kuwa wananchi wetu kidogo wameitikia wito, lakini bado ni tatizo. Kwa sababu wananchi wetu wanakata miti ovyo na wakishakukata miti na taratibu tunaambiwa kata mti, panda mti, lakini hatima yake wananchi wetu hawafanyi hivyo. Kwa hiyo, kupitia Baraza hili tukufu pia nawaomba wananchi wetu tumsaidie Mhe. Rais kwa utunzaji wa mazingira kwa sababu yeye mwenyewe kaliona hili kwamba mwisho wake linaweza likaleta madhara na ndio maana akasema tuimarishe mazingira.

Mhe. Spika, mwisho nasema naunga mkono kwa asilimia mia moja hotuba ya Mhe. Rais, ahsante.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Mhe. Spika, kwanza na mimi nitoe pongezi kwa kupata fursa hii kwa sababu nilikuwa nimeshakata tamaa ya kupata nafasi ya kuchangia. Kwa hivyo, nakupongeza kwa jioni hii na mimi kupata fursa japo kidogo angalau kuchangia hotuba hii.

Mhe. Spika, kwanza na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwepo hapa jioni hii tukiwa katika hali ya usalama.

Mhe. Spika: Samahani Mheshimiwa, Waheshimiwa mnaotoka nadhani utaratibu ni kwamba huwezi kukatisha baina ya Mjumbe mwenye kuzungumza na Spika. Kwa hiyo, naomba mlizingatie hilo ikiwa kuna mjumbe anazungumza basi mtu atafute njia mbadala ya kupita. Endelea Mheshimiwa.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Mhe. Spika, na mimi nimpongeze Mhe. Rais kwa ushindi wake mnono alioupata kwa uchaguzi wa marudio uliopita. Vile vile, nikupongeze wewe Mhe. Spika, Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Baraza kwa kuchaguliwa kwenu kwa kura nyingi mlizozipata za Waheshimiwa.

Mhe. Spika, baada ya shukurani hiyo vile vile niwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Kiwani kwa kunichagua kwa kura nyingi, nikianzia Shehia ya Mtangani, Kiwani, Mwambe, Jombwe na Shehia ya Shamiani Mwambe. Baada ya maelezo hayo nianze kuchangia hotuba ya Mhe. Rais.

Mhe. Spika, mimi nitaanza shughuli za nishati ya umeme. Kwanza nimpongeze Mhe. Rais kwa maelezo yake aliyoyatoa kwenye hotuba, amesema jambo la kwanza tutalibadilisha Shirika la Umeme ili liendane na ushindani wa kibiashara. Hili mimi naliunga mkono sana na kwanza nipongeze kwa jitihada za serikali kwa Unguja na Pemba na sisi zaidi kule Pemba tumeondokana na ule umeme tegemezi wa kutegemea majenereta. Kwa hivyo, tunamshukuru Mwenyezi Mungu sasa Pemba na sisi tuna umeme wa uhakika.

Mhe. Spika, vile vile, tushukuru kwa Wilaya yetu ya Mkoani mpaka visiwani; wilaya yetu hii tuna visiwa vitatu navyo pia umeme umeshafikishwa na wananchi wanaendelea kupata huduma hiyo. Kwa mfano Kisiwa Panza, Makoongwe na Kisiwa cha Shamiani Mwambe hivi sasa umeme umeshafika.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo kidogo nina masikitiko kwenye Shirika letu hili la Umeme. Sikitiko la kwanza ni kwamba wananchi wanapokwenda kwenye shirika kutaka huduma ya kuungiwa umeme muda unakuwa mkubwa. Kwa mfano mtu anakwenda kutaka huduma hii anachukua miezi minne au mitano bado huduma haijafika, kuna tatizo gani, kuna nini na wao watu wa shirika ili wapate fedha nyingi ni kupata wateja wengi. Sasa hili ni moja wapo katika yale mambo yatakayofanyiwa mabadiliko basi Shirika la Umeme suala hili na wao wajitahidi ili alau basi iwe mwezi mmoja. Mwezi mmoja mtu anaanza *process* ahakikishe ukimalizika mwezi mmoja basi ile huduma tayari ameshaipata.

Halafu vile vile kwenye Shirika hili hili la Umeme Mhe. Spika, kwa vile wana uhakika wananchi watakapowakopesha pesa yao wana uhakika wataipata wananchi wetu wengine wengi wao ni wanyonge. Kwa hivyo, na wao watoe mkopo kwa wale watu watakaokuwa wanataka huduma hii ya kuungiwa umeme kwa sababu wana uhakika pesa yao wataipata.

Baada ya kutoka hapo Mhe. Spika, niende sasa katika kumpongeza Mhe. Rais alipozungumzia suala la Muungano na yeye Mhe. Rais alisema kwamba Muungano wa Serikali mbili kwake yeye halina mjadala wala halina mzaha. Kwa hivyo, niendelee kumpongeza kwa sababu bado ana msimamo ule ule wa waasisi wetu wa Muungano Marehemu mzee Abeid Aman Karume na Marehemu Julius Kambarage Nyerere, wao walipoanza kutaka kuunganisha nchi zetu waliangalia muundo gani ambao utatuvusha katika nchi yetu ili nchi yetu ibaki iwe na amani na utulivu. Waliuangalia mfumo wa Serikali moja, wakaangalia mfumo wa Serikali tatu na wakaangalia mfumo wa serikali mbili. Kwa wakati huo na mpaka hivi sasa bado msimo wa serikali mbili ndio utatuvusha katika nchi yetu hii ya Tanzania. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kuna watu wanaokejeli Muungano huu lakini watu hao hao usiku ukicha wameshafika huko upande wa pili na watu hawa hawa ndio wale ambao wanaofaidika na Muungano huu. Sasa mimi bado nampongeza Mhe. Rais aendelee kuwa na msimamo huu huu na nadhani tuna kiporo chetu tulichokibakisha cha Katiba inayopendekezwa, pale palipobakia kwa vile tumeshamaliza uchaguzi sasa Mhe Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. John Pombe Kagufuli na Mhe. Rais wa Zanzibar kiporo kilichobakia kimalizwe ili tuendelee na msimamo wetu wa Muungano wa serikali mbili. (*Makofi*)

Mhe. Spika, baada ya hapo vile vile nichangie suala la zao la karafuu. Mhe. Spika, Mhe. Rais katika hotuba yake amesema kwamba bado serikali itatoa asilimia 80 ya bei ya karafuu katika soko la Ulimwengu ili wananchi waendelee kufaidika.

Mhe. Spika, mimi nampongeza Mhe. Rais kwa sababu leo karafuu inapozaliwa Pemba tunafaidika sana na nchi yetu inapata mapato mengi. Sasa hapa mimi nitoe tu shukurani kwamba mara nyingi serikali imekuwa ikitoa miche ya mikarafuu ili wananchi wetu waendelee kupanda mikarafuu mipya na inatoa bure wananchi hawatozi fudia ya

kununua ya miche ya mikarafuu. Lakini bado naendelea kusema kwamba serikali ijitahidi zaidi kuzalisha miche ya mikarafuu kwa sababu wananchi wetu wameshajiika na suala hili la kupanda mikarafuu mipya.

Kwa hivyo, bado unapofika wakati wa kugawa hiyo miche inakuwa kidogo. Kwa hivyo, ni vyema kwa vile wananchi wameshajiika ni vyema serikali ikajianda kwa kuandaa vitalu vilivyokuwa vingi ili kila mwananchi anaetaka kupanda miche ya mikarafuu basi asihangaike na kutafuta iwe ana uhakika wa upatikanaji wa miche hiyo.
Mhe. Spika, baada ya mada hiyo niende mada ya miundo mbinu. Mimi nitagusia miundo mbinu ya barabara. Mhe. Spika, kwanza tunaishukuru serikali yetu na Mhe. Rais vile vile amesema kwamba kuna barabara nyengine ambazo zitajengwa kwa kipindi hiki cha muda huu tulionao muda wa miaka mitano.

Kwanza nimpongeze Mhe. Rais katika hotuba yake alipoitaja barabara ya Mgagadu Kiwani, kwa sababu iko katika jimbo langu. Vile vile nishukuru kwamba Pemba tumepata barabara nyingi mpya na tumshukuru Mwenyezi Mungu tafauti na tulivyokuwa kama miaka kumi iliyopita kwa sababu hali ilikuwa si nzuri zaidi kisiwa cha Pemba kuhusu usafiri wa barabara. Lakini tunamshukuru Mwenyezi Mungu hivi sasa afadhali.

Hata hivyo tuna masikitiko makubwa Mhe. Spika, kwa mfano ilipojengwa barabara ya Mtambile Muambe, Mtabile Kangani, Mizingani Wambaa, Kenya Chambani. Barabara hizi zilipojengwa wananchi wengi waliharibiwa vipando vyao, lakini kwa masikitiko makubwa mpaka hivi sasa wananchi wale bado hawajalipwa fidia. Kwa hivyo, tunaiomba serikali na kwa wale watakaobahatika Mhe. Waziri atakaebahatika na wizara hii basi vile vile achukuwe juhudi ili wananchi wale tuone kwamba haki yao inapatikana mapema iwezekanavyo. (*Makofi*)
Mhe. Spika, kwa vile wenzangu wamechangia mengi, wamechangia mazuri tu na ndio kwanza tunaanza hii ngwe. Kwa hivyo, baada ya maelezo hayo kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kiwani na mimi naiunga mkono hotuba ya Mhe. Rais mia juu ya mia. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi hii angalau na mimi niseme machache kuchangia hutuba hii ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kati ya Wajumbe 84 waliokuwa humu ndani Mhe. Spika, hotuba hii imechangiwa na Wajumbe karibu 50. Kwa hiyo, ni mwanzo mzuri tu na nawaomba Waheshimiwa Wajumbe waendelee na kasi hiyo hiyo ya kuchangia michango yao. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kama ilivyo kawaida yetu kwa neema zake ambazo anaendelea kuturuzuku za uhai na afya na leo tunaendelea kutimiza na kutekeleza majukumu yetu ndani ya Baraza hili tukufu.

Pili, Mhe. Spika, nichukuwe fursa hii kwa dhati kabisa na kwa heshima kubwa kumshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa imani yake kwangu na kuniteuwa tena kuendelea kumsaidia katika kazi hii ya Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar. (*Makofi*)

Baada ya kufanya kazi hii kwa miezi karibu 18 natambua umuhimu wake, natambua uzito wake na natambua unyeti wake wa kazi hii. Lakini kwa kuwa Mhe. Rais ameniamini na akanikabidhi tena dhamana hii basi naomba nimuhakikishe kwamba nitaendelea kumshauri na kwa kushirikiana na wenzangu tutaendelea kushirikiana nae ili kutimiza yale ambayo ameyaeleza ndani ya kitabu chake cha hotuba aliyokuja kuzindua Baraza hili tukufu. (*Makofi*)

Pia, niwashukuru wale wote kuanzia wewe Mhe. Spika, na wale wote ambao wanaokufuata kwa uteuzi wenu. Ni dhahiri kwamba wale ambao wameweka imani kwenu wameweka imani hiyo wakizingatia uwezo wenu na maarifa yenu ambayo mnayo na naamini kabisa na wao wanaamini kwamba mtatuvusha salama kwenye kipindi hiki cha miaka mitano ya Baraza hili. (*Makofi*)

Nimshukuru na nimpongeze Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa kutangazwa wa pili baada ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Naamini na yeye kwa utendaji wake mzuri wa kipindi cha miaka mitano Mhe. Rais hakuwa na haja ya kutizama majina mengi. Tunamuahidi tutaendelea kushirikiana nae na wale ambao watakuja kuungana na sisi maana nasikia Ikulu kuna jengwa mashamiana. Kwa hiyo inaonekana siku haziko mbali. (*Makofi*)

Kwa hiyo, niwatakie kila la kheri wale wote ambao watapata fursa ya kuteuliwa na Mhe. Rais kuunda Baraza lake la Mapinduzi, sifa ya kuwa waziri ni kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi. Kwa hivyo, Wajumbe wote mliokuwa humu mmeshatimiza sifa hiyo lakini kwa sababu Wajumbe ni 80 na haiwezekani kukawa na nafasi 80 za Mawaziri

basi wale ambao watapata fursa kazi wameshaiona na naamini kati ya wale wengi waliochangia naamini miongoni mwao watapata nafasi hiyo na kazi yenyewe ndio hii ambayo imeanza kuzungumzwa na Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Spika, Mhe. Rais katika hotuba yake kama ambavyo Waheshimiwa Wajumbe wamesema katika ukurasa wake wa sita ameanza hotuba yake kwa maneno "Kazi iliyopo mbele yetu". Ameanza na kuelezea uchumi na amemalizia kwa kuimarisha Muungano. Ukihesabu kuanzia uchumi mpaka kuimairisha Muungano ni sehemu 35 ambazo Mhe. Rais amezielezea na kuzifafanua.

Hakuna kundi ambalo ameacha, hakuna eneo ambalo hakuligusia. Ameelezea maeneo yote kwa ufasaha na kwa uwazi kabisa na sisi ambao tumepewa dhamana hii ya kumsaidia tutahakikisha kwa dhati kabisa kwamba hotuba hii ya Mhe. Rais tunaitengenezea jaduweli wanaita "Bango Kitita" ili kuhakikisha kila waziri ambaye atapata fursa ya kuteuliwa na Mhe. Rais anakabidhiwa eneo lake na kuhakikisha kwamba analifanyia kazi. Hayo ndio maagizo ambayo Mhe. Rais ameyatoa katika hotuba yake. Kwa hiyo, niwaombe sana Waheshimiwa Mawaziri kama katika yale mengi watakayobidhiwa basi hii itakuwa ni sehemu yake.

Mhe. Spika, ninaamini kabisa katika kikao kijacho cha Baraza wakati waziri mwenye dhamana ya mipango atakapokuwa anawasilisha mpango wa serikali kwa mwaka ujao wa fedha. Naamini kabisa mengi ambayo yamezungumzwa na mengi ambayo yamechangiwa na Waheshimiwa Wajumbe, watapata fursa ya kuyachangia vizuri ziadi na kuuliza maswali, ili sasa yapate kujibiwa kwa ufasaha zaidi na waziri mwenye dhamana hiyo.

Sasa mimi sina haja ya kuzungumza mengi kwa sababu najua Mkuu wa shughuli za Serikali atakuja kuhutubia na kulifunga Baraza hili. Lakini naomba nitambue maeneo ambayo Waheshimiwa Wajumbe wameyazungumza kwa dhati kabisa:-

(1) Uwajibikaji na nidhamu

Hili Waheshimiwa Wajumbe, wamelizungumza kwa sauti kali na wamelizungumza wengi kwa pamoja, wamelizungumzia eneo hili. Lakini na mimi nataka niengeze kama hakuna uzalendo basi nadhani haya mengine yote hatutoweza kufanikiwa. (*Makofi*)

Sasa na mimi nazidisha langu "Uwajibikaji, Nidhamu na Uzalendo" lazima tuweke uzalendo mbele. Kama hatuweki uzalendo mbele, haya mengine yote Mhe. Spika, tutayapigia kelele na yataishia humu humu.

(2) Usimamizi wa sheria

Nalo hili wamelizungumzia kwa dhati kabisa, naomba niwahakikishie hata sisi serikalini maeneo haya pia tumekuwa tunayazungumzia na kuyatafutia sasa muaarubaini wake tatizo ni nini. Nini hasa tatizo la kwamba watu sasa wamekuwa sugu katika kusimamia na kutekeleza na kutii hizi sheria. (*Makofi*)

(3) Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato

Waheshimiwa Wajumbe, wamelizungumzia hili kwa dhati kabisa na mifano mingi wametoa. Kwa hivyo, na hili pia tunalichukuwa na kutambua kwamba ni eneo muhimu ambalo Waheshimiwa Wajumbe wamelizungumzia. Na jengine al-maarufu rushwa. (*Makofi*)

(4) Rushwa

Nalo Waheshimiwa Wajumbe, wamelizungumza kwa dhati kabisa kama rushwa hii ifike pahali iwe ni mwisho. Na hili sisi tumelisikia na tutahakikisha kwamba tunalifanyia kazi kwa kushirikiana na Waheshimiwa Wajumbe.

(5) Huduma za Jamii

Wajumbe, wameelezea namna gani serikali izidi kuboresha huduma hizi za jamii; ukianza afya, elimu na hayo mengine yote kwa dhati kabisa Waheshimiwa Wajumbe wameyazungumza. Lakini kubwa ni kupunguza matumizi na hasa ya serikali. Wengi wa Wajumbe walifurahi sana Mhe. Rais aliposema atakata safari za watendaji, naona

makofi yalikuwa mengi. Hiyo ndio dhana na ndio dhamira ya serikali kama katika miaka hii mitano tunayokwenda nayo basi angalau zile safari sio zisiwepo lakini kwa kiasi kikuwa zipungue ili sasa watu watakapokwenda kwenye safari hizi waende kwenye safari ambazo zina tija na lile jambo ambalo wanaliendelea.

(6,7) Amani na Utulivu

Waheshimiwa Wajumbe, wamelizungumzia hili na kupongeza sana Vikosi vyetu vya Ulinzi na Usalama kwa kushirikiana na Idara zetu Maalum za SMZ. Naomba niwahakikishie kama hili ni eneo ambalo serikali itazidi kulisimamia kwa nguvu zake zote. Hakuna mtu ambaye anafurahi kuyaona yunayotokea Syria, Burudi, Somali nadhalika. Kwa hiyo, wajibu wetu sote sisi tuliokuwa humu ndani na wale ambao wako nje kuhakikisha kwamba tunaitunza hii amani maana hiki ni kisiwa, tunaona kwenye *TV* wenzetu wa Syria wanavyohangaika na wengine wanazama kwa kuhama eneo moja kwenda eneo jengine. Sasa hili si la mtu mmoja wala si la serikali peke yake, hili ni letu sote. (*Makofi*)

(8) Mazingira

Waheshimiwa Wajumbe, nalo wamelizungimzia kwa dhati kabisa eneo la mazingira. Na sisi ambao tumelipata kwenye Baraza la Mapinduzi lililomalizika tunajua namna gani eneo hili lina ugumu wake, watu wanapopita Mwanakwerekwe na kuona magari ya mchanga yamesimama mtu unaweza ukadhani tu ni jambo la kawaida. Lakini ukipata taarifa ya jinsi gani kama hatukuwa waangalifu tunaweza na sisi tukaagiza mchanga nje ya nchi, kwa hivyo nadhani hili ni jambo ambalo inabidi tulizingatie.
Sasa kwa ujumla Mhe. Spika, naomba kwa niaba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, niwaambie Waheshimiwa Wajumbe wote, kwamba yale ambayo wameyaeleza sisi serikali tumeyasikia, tumeyapokea na tutahakikisha kwamba tunayafanyia kazi kwa kumkabidhi kila waziri eneo lake, ili pale Mhe. Spika, utakapounda Kamati za Baraza, Waheshimiwa Wajumbe watapata fursa ya kuwakumbusha Waheshimiwa Mawaziri, juu ya utekelezaji wa ahadi hizi na utekelezaji wa maagizo ambayo Mhe. Rais ameyazungumzia.

Mhe. Spika, la mwisho sina haja ya kulizungumza Mhe. Rais amelizungumza vizuri, jinsi ya muundo wake wa serikali, nadhani inatosha na waliosikia wameshasikia na waliofahamu wameshafahamu kwamba huo ndio utakuwa muundo wa serikali kwa kipindi hiki cha miaka mitano ijayo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo Mhe. Spika, naomba kuunga mkono hotuba hii ya Mhe. Rais kwa asilimia mia moja. Mhe. Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nichukuwe nafasi hii kwanza kukushukuruni sana kwa michango yenu ambayo mmeitoa juu ya hii hotuba ya Mhe. Rais aliyoitoa humu ndani. Pia, nichukuwe nafasi hii kuwashukuru wale wote ambao watakuwa hawakupata nafasi na kuweza kustahamilia, kwa sababu ya muda ambao tulionao hautoshi. Walioomba walikuwa wengi na waliobaki wanafika karibu wajumbe 20 hawajapata kuchagia. Lakini waliochangia kama mlivyomsikia Mhe. Mwanasheria Mkuu walifikia wajumbe 50, kwa hivyo kila mjumbe aliyehudhuria atakuwa amechangia, kwa sababu nia alikuwanayo ya kuchangia lakini hakupata nafasi tu, lakini karibu kila jina la mjumbe lilifika hapa kwa ajili ya kuomba nafasi ya kuchangia.

Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijamwita Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa ajili ya kuja kutoa hoja ya kuliahirisha Baraza, basi naomba nimwite Katibu kama kuna shughuli nyengine inayofuata.

Katibu wa Baraza: Mhe. Spika, naomba kukupa taarifa kwamba kwa mujibu wa orodha ya shughuli za leo, tumemaliza shughuli zote zilizopangwa kwa ajili ya Baraza hili, kwa leo na kwa hatua hii ya sasa tumemaliza shughuli zote zilizopangwa kwa ajili ya Mkutano huu wa Kwanza wa Baraza la Tisa la Wawakilishi la Zanzibar. Mhe. Spika, naomba kukupa taarifa. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Katibu. Waheshimiwa Wajumbe, labda naomba pia nikumbushe kabla sijamwita Mhe. Makamu wa Pili kwamba tutakapomaliza hizi shughuli na kabla hatujatoka tutapiga wimbo wa Taifa kama utaratibu ulivyo, kwa sababu tulivyoanza tulianza kwa wimbo wa Taifa. Baada ya kutanabahisha hivyo, basi nitawataka Waheshimiwa Wajumbe, wabaki ili tumalize kabisa hizi shughuli, baada ya hapo tena tutaweza kutoka kwa utaratibu. Sasa nichukuwe nafasi hii kwa heshima zote nimwite sasa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ili aweze kutoa

hoja ya kuliahirisha Baraza, ambayo bila shaka itatanguliwa na hotuba ndogo ambayo tuko tayari kukusikiliza. Mhe. Makamu wa Pili tafadhali sana. *(Makofi)*

KUAHIRISHA BARAZA

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais: Mhe Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu na Mwingi wa Rehma kwa kuendelea kuweka nchi yetu hii katika hali ya amani, utulivu, umoja na mshikamano mkubwa. Hali ambayo imeiwezesha Serikali na wananchi kuendelea na shughuli zao za kila siku bila ya mtafaruku wa aina yeyote. Aidha, tunaendelea kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufanya uchaguzi katika hali ya amani na utulivu, jambo ambalo sote tuliomo humu Barazani pamoja na wananchi wote ni mashahidi wa hilo. Ninawaomba wananchi waendelee kuitunza na kuithamini amani iliopo nchini.

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutukutanisha hapa tukiwa katika hali ya uzima na afya njema na kutuwezesha kufanikisha vizuri Mkutano wa Kwanza wa Baraza hili Tukufu la Tisa la Wawakilishi, ulioanza tarehe 30 Machi, 2016. Nimefarijika kuwa kazi zote zilizopangwa katika ratiba yetu tumezikamilisha kwa wakati na kwa ufanisi mkubwa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba nitumie fursa hii kwa niaba yangu na Waheshimiwa Wawakilishi, kutoa pongezi za dhati kwako wewe Mhe. Spika pamoja na Naibu Spika, Mhe. Mgeni Hassan Juma, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuliongoza Baraza letu hili Tukufu. Vile vile, nampongeza Mhe. Riziki Pembe Juma, Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi wa Viti Maalum na Mhe. Shehe Hamad Mattar, Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi Jimbo la Mgogoni, Pemba kwa kuchaguliwa kuwa Wenyeviti wa Baraza letu hili. Hii inaonesha imani kubwa waliyonayo Waheshimiwa Wajumbe juu yao. Ni mategemeo ya Waheshimiwa Wajumbe kwamba mtaliongoza Baraza hili Tukufu kwa hekima, busara, uadilifu na umakini mkubwa ili kuliwezesha Baraza kutekeleza majukumu yake yakiwemo ya kuisimamia Serikali kwa ufanisi na kupeleka maendeleo endelevu kwa wananchi wetu na nchi yetu kwa ujumla. *(Makofi)*

Aidha, nachukua fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Hamza Hassan Juma, Salha Mohamed Mwinjuma, Rashid Ali Juma, Lulu Msham Abdulla na Hamad Abdulla Rashid kwa kuchaguliwa kwao kuwa Wajumbe wa Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi. Kuchaguliwa kwao kunadhihirisha imani kubwa ambayo Waheshimiwa Wajumbe aliyonayo juu yao, kwani Kamati hii ni muhimu sana kwa maendelezo ya Baraza letu. *(Makofi)*

Aidha, napenda kuwapongeza wenzetu saba walioteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na hivi karibuni tu uliwaapisha. Wajumbe hao wakiwa Mhe. Mohamed Aboud Mohamed, Mhe. Amina Salum Ali, Mhe. Maudline Castico, Mhe. Ali Abeid Karume, Mhe. Hamad Rashid, Mhe. Juma Ali Khatib na Mhe. Said Soud Said. Kuteuliwa kwao kunaonesha imani kubwa ambayo Mheshimiwa Rais anayo juu yao na kwamba michango yao italisaidia sana Baraza lako Tukufu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, napenda kutoa pongezi maalum kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa kuchaguliwa kwa ushindi wa kishindo wa zaidi ya asilimia 91, kushika wadhifa huo katika muhula wa pili wa Serikali ya Awamu ya Saba kupitia uchaguzi wa marejeo uliofanyika tarehe 20 Machi, 2016.

Aidha, pamoja na pongezi hizo, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa imani kubwa aliyoionesha kwangu kwa kuniteua kuwa Makamu wa Pili wa Rais kwa mara nyengine tena. Namuomba Mwenyezi Mungu atubariki na kutujaalia afya njema na nguvu ya kuwatumikia wananchi wote hapa Zanzibar bila kujali rangi, jinsia, dini au itikadi zao za kisiasa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, aidha, kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, napenda kutoa pongezi za dhati kwa Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi sana. Hii imeonyesha imani na upendo kwa wananchi wa Tanzania walioayo juu yao. Pia nampongeza Mhe. Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuteuliwa kushika nafasi hiyo. Hii inaonyesha imani ambayo Mhe. Rais Magufuli aliyonayo juu ya Mhe. Kassim Majaliwa. *(Makofi)*

Ni matumaini yetu kwamba viongozi wetu hao watalitumikia Taifa letu, kwa hekima na busara ili kuwapatia wananchi wetu maendeleo ya dhati. Tunampongeza Rais Magufuli kwa kasi aliyoanza nayo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein tarehe 05 Aprili, 2016 alilituhutubia Baraza hili Tukufu kwa mujibu wa mamlaka aliyonayo Kikatiba. Pamoja na mambo mengine, katika hotuba yake amefafanua kwa kina kuhusu wajibu wetu kama Wajumbe wa Baraza hili, na ameeleza masuala muhimu katika kuijenga Zanzibar yetu.

Mhe. Spika, hotuba ya Mheshimiwa Rais itakuwa dira na mwongozo wetu katika kutekeleza majukumu yetu ndani na nje ya Baraza hili, kwani hotuba hiyo iligusa kila Sekta ya maendeleo yetu. Wajumbe mlipata nafasi ya kuijadili hotuba hiyo kuanzia tarehe 6 Aprili, 2016 hadi leo hii.

Michango ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu ilijikita zaidi juu ya uwepo wa amani na utulivu, kuboresha na kuimarisha maeneo huru hasa ya Fumba na Micheweni, vita dhidi ya rushwa na udhalilishaji wa kijinsia, wanawake na watoto, uendelezaji wa elimu na Vyuo vya Amali, mazingira, ajira kwa vijana, ukusanyaji wa mapato na ulipaji wa kodi kwa kutaja machache. Naliahidi Baraza lako tukufu kuwa Serikali itachukua hatua ya kuyashughulikia mapendekezo yote yaliyotolewa. Kama Mwanasheria Mkuu alivyosema, michango yote hiyo itawekwa kwenye jeduali maalum (Bango Kitita) na kusambazwa kwa Mawaziri wote watakaohusika. Baadhi yao wamo humu ndani na wamesikia yaliyozungumzwa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nichukuwe nafasi hii sasa kuwapongeza Waheshimiwa Wawakilishi wote, kwa ushindi mkubwa katika majimbo yao. Najua mlifanya kazi kubwa pamoja na mimi hadi kupata ushindi huu, na leo tumo ndani ya Baraza hili tukufu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Baraza hili Tukufu la Wawakilishi lina jukumu muhimu na kubwa la kutunga Sheria. Napenda kuwakumbusha Waheshimiwa Wawakilishi kwamba hiyo itakuwa ndiyo kazi yetu ya msingi, inayotakiwa kufanywa kwa busara, hekima na umakini mkubwa. Pia, tunalo jukumu la kuisimamia na kuishauri Serikali ili kuhakikisha kuwa matatizo na kero mbali mbali za wananchi, zinatatuliwa kwa ufanisi na mafanikio makubwa.

Tunapaswa kuhakikisha kuwa Serikali inatoa mchango wake kikamilifu katika kuyafanya maisha ya wananchi wetu kuwa bora zaidi kwa kutumia nguvu kazi na rasilimali tulizonazo. Ni matarajio ya Serikali kuwa itapata taarifa na ushauri kutoka kwa Waheshimiwa Wawakilishi juu ya maeneo yanayohitaji kupewa msukumo, ili kuongeza kasi ya maendeleo ya Zanzibar. Kwa upande wake, Serikali itaifanyia kazi taarifa na ushauri utakaotolewa na Baraza hili Tukufu.

Mhe. Spika, sambamba na majukumu hayo, naomba kuwashauri Waheshimiwa Wawakilishi tuwe karibu na wananchi waliotuchagua. Sisi ndio macho na masikio ya wananchi hao. Tumepewa heshima kubwa na wananchi hao kwa kutuchagua kuwa Wajumbe wa Baraza hili. Wananchi hao wana mategemeo makubwa kwamba tutawasaidia kutatua changamoto zao mbali mbali za maendeleo zinazowakabili.

Ni wajibu wetu kufikisha mawazo ya wananchi hao Serikalini kwa kupitia mikutano na vikao vya Baraza hili pamoja na njia nyengine zinazofaa. Aidha, tunapaswa kuwaeleza wananchi wetu kile ambacho Serikali imepanga kukifanya na jinsi ya kutumia fursa, rasilimali, mipango na taratibu zilizopo za Serikali ili kuweza kuboresha maisha yao.

Mhe. Spika, napenda kuwaomba kwa mara nyingine tena, wananchi wote kuendelea kudumisha amani na utulivu katika visiwa vyetu na nchi yetu ya Tanzania kwa ujumla. Bila ya kuwepo Amani na Utulivu, hakuna maendeleo. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea kusimamia suala la amani na utulivu kwa nguvu zake zote ili kutekeleza mipango yetu ya kujiletea maendeleo zaidi ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Hakuna haja tena ya kukumbusha mambo yaliyopita, ila Serikali inatambua wapo baadhi ya wananchi wakorofi wanaojihusisha na vitendo vya kuvuruga amani na utulivu uliopo.

Kwa mfano, wakati tukielekea katika uchaguzi wa marejeo uliomalizika hivi karibuni, wakorofi hao walijihusisha kutega miripuko inayosadikiwa kuwa mabomu na kuchoma moto mashamba ya mikarafuu, nyumba na makaazi na maskani za CCM. Vyombo vya Dola vinaendelea na hatua za uchunguzi wa matukio hayo na baadae kuchukua

hatua kwa mujibu wa Sheria. Hakuna mtu atakayepona kuchukuliwa hatua kali za kisheria ikiwa atabainika kutishia amani na utulivu tulionao. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tunasikitishwa na mambo yanayotokea huko Pemba ambapo baadhi ya wafanya biashara kuwanyima wananchi wenzao huduma za kibiashara, kama vile kuwauzia bidhaa au kuwapa huduma za usafiri kwa sababu za kiitikadi za kisiasa. Jambo hili siyo zuri na ingefaa liachwe mara moja. Serikali inalifuatilia kwa karibu sana suala hili na haitasita kumchukulia hatua mfanya biashara yoyote atakaye liendeleza jambo hili ikiwa ni pamoja na kumfutia leseni yake. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kuhusu uchaguzi wa marejeo uliofanyika tarehe 20 Machi, 2016, nachukua fursa hii kuipongeza Tume ya Uchaguzi Zanzibar kwa kazi nzuri ya kusimamia na kufanikisha uchaguzi huo kwa mafanikio makubwa. Uchaguzi huo ulikuwa huru na haki, na ulipelekea ushindi mkubwa kwa Chama cha Mapinduzi kupitia kwa aliyekuwa mgombea wake, Dkt. Ali Mohamed Shein, ambaye kwa sasa anaendelea kuiongoza nchi yetu akiwa ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kipindi cha pili cha miaka mitano (2015 – 2020). *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa vile uchaguzi umekwisha, tunapaswa tuzidishe ushirikiano, mshikamano na umoja wetu katika kuijenga nchi yetu. Kwa upande wetu Waheshimiwa Wawakilishi turudi Majimboni mwetu ili tukashirikiane na wananchi kusukuma gurudumu hili la maendeleo. Aidha, napenda kutumia fursa hii kuwaomba watumishi na watendaji wote wa Serikali watakaoteuliwa hapo baadae, kuwatumikia wananchi wote bila ya kujali itikadi zao za kisiasa.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inahimiza uwajibikaji zaidi na usimamizi mzuri wa fedha na rasilimali nyengine za umma katika ngazi zote. Wafanyakazi kujituma na siyo kufanya kazi kwa mazoea jambo ambalo Rais wetu alilipigia kelele sana katika kipindi kizima cha kwanza. Na hata hotuba yake aliyoitoa wakati akilizindua Baraza hili alisisitiza jambo hilo. Nikimnukuu alisema:

> "Wapo baadhi ya watumishi wenye tabia ya kutoroka kazini, kuchelewa na hawazijali kanuni ziliopo za utumishi wa umma. Wao hujifanya wababe mbele ya viongozi wao. Wafanyakazi wenye sifa mbaya nilizozielezea katika kipindi hiki tutawachukulia hatua watakapobainika na kama hapana budi tutawafukuza kazini. Hatuwezi kuwa na wafanyakazi waliokuwa hawana nidhamu. Sasa basi, imetosha". *(Makofi)*
>
> "Waliopewa dhamana ya kuziongoza Idara mbali mbali za Serikali, watapaswa watekeleze wajibu kwa kuwasimamia wafanyakazi walio chini yao. Pindi kama hawatawawajibisha wafanyakazi wao, basi watawajibishwa wao. Lengo letu liwe kutoa huduma kwa wananchi, kwani sote tunawajibika kwao; kwa kuzingatia misingi ya utawala bora."

Haya ni maneno ambayo aliyasema hapa juzi Mhe. Rais, kwa hiyo, tusijetukaoneana haya. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi najua ziko Idara na Mashirika ya Umma ambayo hayako vizuri kiutendaji na ambayo yanalalamikiwa sana na wananchi, kwa sababu ya kutowajibika kwa watendaji wao. Nawaomba watendaji watakaoteuliwa pamoja na kazi zao za maofisini, watenge muda kuzitembelea taasisi zilizo chini yao ili waone uwajibikaji wa viongozi wanaozisimamia taasisi hizo. Naahidi kumsaidia Mhe. Rais katika kuyatumbua majipu yatakayojitokeza. *(Makofi)*

Nitamuomba Mhe. Rais aniunge mkono kwa uamuzi wowote nitakao uchukua dhidi ya mtendaji yeyote ambaye ataonekana hawajibiki vipasavyo, kwa sababu ya ama uvivu, uzembe, dharau au ubadhirifu. Wako watendaji, Mhe. Spika, wanakataza jambo la maendeleo kwa sababu ya ubinafsi. Watendaji hawa nao hatutawavumilia. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naamini siyo baada ya muda mrefu Mhe. Rais atateua Baraza la Mawaziri. Ni imani yangu kwamba tutashirikiana pamoja na watendaji watakao teuliwa, ili kulisukuma gurudumu la maendeleo kwa manufaa ya wananchi wetu. Natoa wito kwa watakaoteuliwa kuwa mawaziri nao wasikae maofisini sana, wakipepewa na

mafeni na viyoyozi, bali watenge siku maalum waende vijijini wakaangalie wananchi wenye matatizo na waone namna gani wataweza kuwasaidia. Kila waziri kwa eneo linalomhusu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, migogoro ya ardhi imekuwa changamoto kubwa kwa serikali yetu katika kipindi kilichopita. Migogoro mingi imekuwa ikisababishwa na baadhi yetu viongozi kwa sababu za kitamaa. Kama hiyo haitoshi, baadhi ya wananchi wanaendesha ujenzi wa nyumba kiholela bila ya vibali vya kujengea na wakati mwingine katika maeneo yasiyo ruhusiwa kama vile kwenye maeneo ya vianzio vya maji na maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya ujenzi wa miji ya kisasa. Tunawatahadharisha waliojenga katika maeneo hayo. Katika hotuba yake aliyoitoa wakati akilizindua Baraza hili, Mhe. Rais alilizungumzia sana suala hili. Niwakumbushe aliyosema, namnukuu:

> **"**Napenda nitoe indhari kuwa serikali haitomvumilia kiongozi wa ngazi yoyote ambae atajijengea tamaa na akajiingiza katika migogoro ya ardhi au akashindwa kutatua migogoro iliyopo katika dhamana yake. Si siri, kwani wapo baadhi ya viongozi waliojiingiza katika matatizo ya ardhi na kusababisha mzozo mkubwa kwenye jamii. Migogoro ya ardhi ni kadhia ambayo tunataka tuimalize katika kipindi hiki cha miaka mitano ijayo. Kwa hivyo, nawatahadharisha viongozi watakaopewa dhamana ya kushughulikia masuala ya ardhi wayazingatie maelezo yangu haya". *(Makofi)*

Mhe. Spika, mnamo siku za hivi karibuni kumekuwepo na upandaji wa bei za bidhaa bila ya sababu za msingi. Serikali inalifuatilia suala hili kwa karibu sana, na atakaye gundulika kupandisha bei kiholela atafungiwa leseni yake ya kuendeshea biashara mara moja. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ninachukua nafasi hii kutoa wito maalum kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu, kushirikiana na wananchi katika kuendeleza usafi wa mazingira na kutekeleza maelekezo yote ya wataalamu wa afya, ili kujikinga na maradhi ya miripuko kikiwemo kipindupindu, kwani ugonjwa huo bado upo, na namna moja ya kuuepuka ni kuweka mazingira yetu katika hali ya usafi.

Pia, ninaomba niwakumbushe Waheshimiwa Wawakilishi na wananchi tuzitumie vizuri mvua zinazoendelea nchini kwa kuendeleza shughuli za kilimo cha mazao ya chakula na biashara kwa lengo la kupata mavuno mengi zaidi na kujiongezea kipato. Sambamba na hayo, serikali inaendelea kuwataka wananchi wanaoishi sehemu za mabondeni waendelee kuchukua hadhari wakati huu wa mvua zinazoendelea, ili tuweze kuepuka athari na majanga yasiyo ya lazima. Tunawasihi wananchi hao wahame kutoka mabondeni humo na kuhamia sehemu za juu, ili kuepuka uharibifu wa mali zao na hata upotevu wa maisha yao.

Mhe. Spika, mwisho, ingawa si kwa umuhimu, napenda kumshukuru sana Spika wetu Mstaafu, Mhe. Pandu Ameir Kificho kwa kuliongoza Baraza hili kwa umahiri mkubwa kwa muda kwa miaka 20 mfululizo. Mhe. Kificho alilionguza Baraza hili kwa hekima, busara na uvumilivu mkubwa. Ninamtakia kila la kheri na mafanikio mema katika shughuli zake za baadae. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitawashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Mahonda kwa imani kubwa walionipa kwa kunichagua kuwa Mwakilishi wao. Nawaahidi kuwa nitawapa utumishi ulio bora na kutekeleza ahadi zote nilizozitoa wakati wa Kampeni. Nawaomba wanipe ushirikiano wao ili tuweze kuendeleza Jimbo letu na kujiletea maendeleo.

Mhe. Spika, kwa kumalizia niwatakie Waheshimiwa Wawakilishi kila la kheri na mafanikio mema katika kuwatumikia wananchi wao majimboni mwao. Aidha, nawatakia safari njema na ya salama ya kurudi majimboni mwao, na hasa wawakilishi wenzetu kutoka Pemba kwa sababu wao wana safari ndefu zaidi kuliko wenzao wa Unguja. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu liahirishwe hadi siku ya Jumatano tarehe 18 Mei, 2016, saa 3.00 barabara za asubuhi.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa na sote ni mashahidi kwamba imeungwa mkono. Lakini kabla sijawahoji naomba nizungumze mambo machache. Kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa hotuba yake ambayo imemalizia kwa hoja ambayo nitaihoji muda si mrefu sana. *(Makofi)*

Kwa kweli, hotuba yako ni nzuri na hivyo inazidi kutoa msisitizi zaidi kwenye hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar. Kwa hiyo, wale wenzetu ambao watabahatika kuwemo kwenye serikali ambayo itateuliwa hivi punde, basi wajue kwamba wanayo kazi ya kufanya, na mambo mengi sana yameelekezwa na yamo katika hotuba ya Mhe. Rais pamoja na hii ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais.

Waheshimiwa Wajumbe, pia, kuna matangazo mafupi tu. Kwanza kesho kutakuwa na mafunzo elekezi ya wajumbe hapa katika Afisi ya Baraza la Wawakilishi, naomba niwakumbushe nafikiri tayari mumeshapata taarifa. Vile vile, munakumbushwa kwamba Waheshimiwa Wajumbe wote ambao wamejisajili kwenye mazoezi, kwamba mazoezi yapo na yatakuwa kwenye uwanja wa polisi Ziwani kwa ajili ya Waheshimiwa Wajumbe wote.

Baada ya matangazo hayo mafupi sasa naomba nichukue nafasi hii niwahoji kwamba hoja iliyotolewa na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ya kuahirisha Baraza la Wawakilishi hadi siku ya Jumatano tarehe 18/05/2016 saa 3:00 za asubuhi, wale wanaounga mkono wanyooshe mkono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijaahirisha naomba sote tusimame, ili uweze kupigwa wimbo wa Taifa na baada ya hapo nitaweza kuahirisha hadi tarehe iliyopagwa.

WIMBO WA TAIFA

(Wimbo wa Taifa uliimbwa kuashiria kuahirishwa kwa Mkutano wa Baraza)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa natangaza rasmi kwamba naliahirisha Baraza la Wawakilishi hadi siku ya Jumatano tarehe 18/05/2016 saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 12:47 Mkutano uliahirishwa mpaka tarehe 18 Mei, 2016 saa 3:00 asubuhi)